7 FEBRUARI, 2015

**BUNGE LA TANZANIA**

___________________

**MAJADILIANO YA BUNGE**

_______________________

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Kumi na Moja - Tarehe 7 Februari, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

Spika *(Mhe. Anna S. Makinda)* Alisoma Dua

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu tuendelee!

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

***Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa wa Mwaka 2015 (The National Payment System Bill, 2015).***

***Muswada wa Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania wa Mwaka 2015 (The Youth Council of Tanzania Bill, 2015).***

*(Miswada yote miwili iliyotajwa hapo juu ilisomwa kwa mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Katibu tuendelee!

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI TEULE YA BUNGE**

**Kamati Teule Iliyoundwa Kuchunguza na Kuchambua Sera Mbalimbali Zinazohusu Masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji na Uwekezaji ili Kubaini Kasoro Zilizomo Katika Matumizi ya Ardhi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Haya mambo ya kufanya tafrija kabla ya kazi ndio matokeo yake haya. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nimemwona hapa naangalia waliopo na wasiokuwepo! Mheshimiwa Moses Machali, nimekuona! Anza Machali kwanza nitaendelea kuangalia wengine.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa nami nichangie taarifa iliyowasilishwa na Kamati Teule ya Bunge, ambayo inachunguza masuala yanayohusiana na kilimo, ardhi, maji, pamoja na mazingira.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo kwanza kabisa naunga mkono taarifa ambayo imeungwa mkono taarifa ambayo imewasilishwa na Kamati Teule chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Ole Sendeka.

Kimsingi kama ambavyo taarifa imeweza kutuelekeza kwamba, kuna tatizo la msingi ambalo linajitokeza, ni kukosekana kwa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi. Kama ambavyo tunajua kwamba, kumekuwa kuna *crisis* kati ya wakulima na wafugaji hapa nchini, pamoja na watu wengine ambao wamekuwa wanakuja kwenye nchi yetu kwa lengo la kuwekeza, wakiwemo pia wazawa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi ukienda katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa ikiongezeka siku hadi siku. Tumeisikia sana kwenye maeneo kama ya Morogoro, tu ni kwa sababu kuna vyombo vya habari vingi kuliko maeneo mengine.

Lakini migogoro hii tunaikuta hata katika maeneo mengine, sema tu kwamba inakuwa hai-ripotiwi, kutokana na kukosekana kwa vyombo vya habari ambavyo vinaweza vikafika katika maeneo *specific* na hatimaye kuweza kushuhudia matatizo haya yakijitokeza.

Mheshimiwa Spika, lakini ukija kuangalia kwenye ripoti, imetuonyesha kabisa kwamba tatizo kubwa, ni utendaji usioridhisha, kwa maana ya Maafisi wa Serikali, ambao wamekasimiwa mamlaka ya kuweza kusimamia sheria, sera na taratibu mbalimbali, ambazo zingeweza kuhakikisha kwamba hakuna matatizo ya namna hii, ambayo yanajitokeza miongoni mwa makundi hasa mawili, ambayo yanazidi kuheshimiana kadiri siku zinavyoenda.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kuwa na programu maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabia za Watendaji Serikalini, ili kuhakikisha tunaweza kuwa na *Human Resource Capital,* ambayo inaweza ikasimamia na kuratibu mambo haya vizuri, tofauti na ilivyo hivi sasa.

Taarifa imetueleza kwamba, maeneo mengine inaonekana kuna vitendo vya kifisadi, makosa mengine ni ya kimakusudi! Lakini suala la viongozi kuweza kuchukua hatua, dhidi ya watu ambao wamezembea na matokeo yake watu wanapoteza maisha, ni suala ambalo ndio linapelekea matatizo haya kuzidi kuongezeka kadiri siku zinavyoenda.

Mheshimiwa Spika, pengine tuna wajibu wa kuhakikisha, tuwe na sheria maalum ambazo pengine zitawafanya viongozi wakishindwa kuwajibika waweze kuchukuliwa hatua kali. Kama hatuwezi tukachukua hatua dhidi ya viongozi au Watendaji ambao ni wazembe, hata tukae hapa, tulale na tukizungumza mambo haya, itaendelea kuwa kama ambavyo imezoeleka kila siku.

Mheshimiwa Spika, pengine tuulize Serikali kwa sababu najua baadaye Mawaziri nao watakuja kuchangia. Watuambie, tatizo hili ambalo limekuwa *reported* kwenye ripoti yetu, kwamba kuna uzembe wa utendaji, huko Serikalini, unasababishwa na nini? Kwa nini hali hiyo? Sheria zipo, za kuweza kushughulikia watumishi ambao wameshindwa ku-*perform* vizuri, lakini kazi imekuwa ni kulindana.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wazi, unapoona ya kwamba Waziri anamlinda mtu, anamlinda Katibu Mkuu wake! Katibu Mkuu wake anamlinda labda Mkurugenzi fulani, ni wazi kuna *chain* ya dili, wote wananufaika katika mambo ambayo hayakutarajiwa kwa mujibu wa sheria. Sasa watu wa namna hii, hawakupaswa kuweza kuvumiliwa.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wakati mwingine, tunafanya makosa kwa sababu inapokuja kwenye suala la kutaka tuiwajibishe Serikali, au viongozi fulani, fulani, tumekuwa ni kama dhaifu hivi.

Mbunge anaweza akawa na hoja nzuri tu, wengine wanampinga kwa sababu anatoka Chama fulani. Matokeo yake ndiyo hayo unasikia huko Mvomero watu wanachapana, Waziri wa Mifugo yupo! Waziri wa Mambo ya Ndani yupo! Ukifuatilia sana sehemu nyingine, kwa mfano imetokea kwetu huko. Mkuu wa Wilaya tumepata kueleza ni janga.

Ilipata kutokea Mkuu wa Mkoa amekutana na kundi kubwa la ng'ombe. Ng'ombe wanaingia bila utaratibu! Mkuu wa Mkoa anamwuliza yule mtu aliyekuwa anaswaga wale ng'ombe, Mkuu wa Mkoa alimwuliza, akasema mimi siongei na nyie, Mkuu wa Mkoa anajibiwa naongea na Wakuu wa Nchi.

Mkuu wa Nchi anayetajwa ni nani? Ni Mkuu wa Wilaya ya Kasulu Bwana Dani Makanga. Sasa akamwambia hebu chukua simu uongee na huyu! Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kanali Machibya, anapokea simu alivyosikia ni sauti ya *DC* ikabidi amrudishie simu yake.

Sasa unaweza kuona kwamba ni mambo gani yanayoendelea katika nchi hii. Kuna watu wamepewa nafasi lakini nafasi hizo wanazitumia kwa maslahi binafsi. Huko kwetu wanatajwa watu kwamba kazi yao ni kuongwa ng'ombe, Watendaji wa Vijiji wanahongwa ng'ombe, Maafisa Tarafa wanahongwa ng'ombe, baadhi ya Wakuu wa Wilaya wanahongwa ng'ombe, Wakurugenzi wanahongwa ng'ombe na pesa juu.

Sasa mambo haya lazima tuyaangalie. Eneo ambalo tunajua ni kwa ajili ya kilimo, liachwe kwa ajili ya shughuli za kilimo. Maeneo ambayo ni kwa ajili ya wafugaji, liachwe kwa ajili ya wafugaji! Sasa Serikali ituambie, maana yake Kamati ime-*propose* kuwe na mpango wa muda mfupi na mpango wa muda mrefu, ili kuweza ku-*rescue* hii *situation* ambayo inajitokeza hivi sasa.

Watuambie kwenye mpango wa muda mfupi, watachukua hatua kwa kasi ya kiasi gani ili kuhakikisha wafugaji wanakuwa na maeneo yao kwa ajili ya Wafugaji na wakulima hawaingiliwi kwenye maeneo yao ya Kilimo ambayo watakuwa wanayatumia kwa ajili ya kilimo. Kama hatuwezi tukafanya hivyo, itakuwa ni kazi bure

Serikali ituambie. Muda mfupi iwe ni miezi mingapi? Watuambie hapa *specifically*! Mipango ya muda mrefu, itachukua muda gani?

Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, Waziri ambaye alipatwa na ajali juzi juzi hapa kwenye sakata la Escrow, imekuwa ni wimbo! Wanatuambia tatizo ni kukosekana kwa mipango mizuri ya matumizi ya ardhi. Kwamba hapa ni kwa ajili ya wafugaji, hapa ni kwa ajili ya wakulima, hapa ni kwa ajili ya sijui shughuli gani na kadhalika.

Lakini tumekuwa na Mawaziri wa maneno maneno walio wengi na ndio maana yote haya yanajitokeza na yataendelea kujitokeza. Kama hatuwezi tukawa na mpango maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabia za viongozi na watendaji katika nchi yetu, tunahitaji kuwa na *program* maalum kwa ajili ya mabadiliko ya tabia za watu.

Tabia hizi Waziri anakuja hapo anaulizwa swali, anajibu majibu ambayo anajisikia. Halafu baadaye ukikutana naye nje ukimwuliza, usishangae anakujibu tofauti na kile alichokwambia. Kwa sababu watu wanajibu jibu tu vile ambavyo wanajisikia! Halafu wanajua wanajua hapa, utajibu baadaye ukishaondoka, umechomoka.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana ilijitokeza hata hapa maswali ambayo aliuliza Mbunge wa Mbeya Mjini, kuhusiana na masuala ya umeme. Mwaka jana swali hilo hilo walimjibu kwa namna nyingine. Juzi hapa tena walikuja wakatoa swali lile lile, wakamjibu tena kwa namna nyingine.

Sasa hii inadhihirisha kwamba tuna watu ambao hawako *serious* Serikalini. Eh! Bwana, leo utasikia wanakuambia jambo hili kwa namna hii, kesho watakuambia kwa namna nyingine. Sasa haya matatizo ya wakulima na wafugaji, ambayo yanajitokeza, watu wanapigwa, tumeshuhudia hapa wakati wa taarifa ya Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, kama haya ambaayo yamependekezwa kwenye taarifa ambayo imewasilishwa chini ya Mwenyekiti wa Kamati Teule, hayatafanyiwa kazi, tutegemee kuona watu wataendelea kuchinjana tu huko mitaani. Wataendelea kuuwana, kwa sababu tu ya uzembe wa baadhi ya watu.

Kwa hiyo, tunaitaka Serikali, tuitake Serikali kama Bunge tuhakikishe wanachukua hatua ambazo zinastahili, kuliko kuwa ni watu wanakuja wamekuwa ni Mawaziri ningetumia neno bla bla lakini hawapendi. Lakini tumekuwa na Mawaziri wa bla bla humu ndani. Watakuja hata baadaye….........*(Hapa Mzungumzaji Alikatishwa)*

**SPIKA:** Hebu ondoa hayo maneno hayahitajiki.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nayaondoa maneno hayo, najua hawayapendi. Lakini tunalazimika wakati mwingine tuwaambie. Kwa sababu siyo ajabu kumsikia Waziri anakuja kujibu hapa leo kwa namna fulani, halafu kesho atakuja kukujibu kwa namna nyingine. *(Makofi)*

Sasa maneno haya ni lazima wakati mwingine, *chloroquine* ni chungu lakini ili kusudi upone ni sharti lazima uimeze. Lazima tuwaambie hawa Mawaziri tuweze kuwa na Mawaziri ambao wanatimiza wajibu wao. *(Makofi)*

Kwa sababu, ni aibu na ajabu kuwa na viongozi ambao hawawezi kutumia *brain* zao vizuri, tukahakikisha kwamba matatizo haya yanakoma. Wanajua kwamba tatizo ni kutokuwa na matumizi mazuri ya ardhi. Sasa nani afanye?

Tunawapitishia Bajeti hapa, kama hicho ndicho kipaumbele, kwanini wasiseme kwamba katika mwaka wa fedha 2015/2016 tunaomba kiasi cha shilingi bilioni labda tano kwa ajili ya kupima ardhi, tupate maeneo ya wafugaji, pamoja na wakulima.

Mheshimiwa Spika, usishangae pamoja na tunachangia hapa, sasa hivi tupo kwenye *budget process*. Usishangae hili suala, lisije kwenye Bajeti ya mwaka 2015/2016, kwa sababu hawa ni watu ambao tumekuwa tunawaambia lakini wanasikia wanajifanya hawasikii.

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru tunaomba wahakikishe wanayafanyia kazi mambo haya.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Taarifa ya Kamati Teule. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliotangulia kuipongeza Kamati Teule imefanya kazi nzuri na kazi kubwa, nami naiunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kusema kwamba, migogoro iliyopelekea vifo kati ya wakulima na wafugaji, baina ya wananchi na hifadhi, baina ya wananchi na Taasisi za Serikali, ifike wakati tuseme imetosha.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya msingi ambayo yamekuwa yakiongolewa kwa muda mrefu. Lakini kwa kuwa Mipaka mingi ya Hifadhi haitambuliki, na wananchi katika maeneo mbalimbali wamejenga nyumba zao, wamejenga shule, wamejenga zahanati, kuna misikiti, kuna makanisa, kuna miundombinu ya maji!

Mheshimiwa Spika, swali la kujiuliza! Serikali muda wote ilikuwa wapi, wakati wananchi wakijenga nyumba zao, wakijenga misikiti pamoja na makanisa, miundombinu ya maji, pamoja na mambo mengine. Sasa inapofikia wakati wakaambiwa wananchi wale wahame tunawaonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa leo wananchi wale inafikia wakati ndani ya maeneo hayo ya Hifadhi wamesajiliwa na wanapiga kura. Hasa hili ni jambo kubwa sana hivi sasa. Cha msingi tuandae mazingira yaliyo mazuri, kwamba ndani ya maeneo yale na uhifadhi wenyewe katika maeneo hayo sio hifadhi tena, basi Serikali angalau itoe unafuu fulani ambao wananchi wale wataendelea kubakia na sio kuhamishwa.

Suala la pili, taarifa ya Mheshimiwa Ole-Sendeka ya Kamati Teule inasema: Kigoma, Rukwa, Kagera kuna uvamizi mkubwa wa wageni kupeleka mifugo. Hili halitokomeshwa kwani Wenyeviti wa Serikali za Vijiji hawa ndio matatizo. Wenzangu wengi wamesema kwamba hapa rushwa ilitawala. *(Makofi)*

Nami nataka niseme tu hapa kwamba, katika Mikoa hii ya Mipakani, tuwe makini sana kupita kiasi. Kwa sababu hivi sasa, hata Operesheni Tokomeza baada ya kufanikiwa kwa kiasi fulani, lakini bado baadhi ya nchi jirani wale wahamiaji haramu wanarudi katika nchi yetu. Wanapata msaada kwa wenyeviti wa Serikali za Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linachosha, linatia nchi katika aibu kubwa kupita kiasi. Uhamiaji nao wapo wanaangalia mambo haya. Hata kama kuna njia nyingi za panya, lakini na hao Wahamiaji sasa wanataka wafungue makucha yao zaidi.

Taarifa hii katika yote ilikuwa ni sampuli, lakini kwenye Mikoa ile ya Kusini, vifo navyo kule Rufiji vilisikitisha. Mkoa wa Ruvuma hata mwaka 2014, Tunduru kule nako vilevile! Watu wengi wamepoteza maisha kama nilivyosema mapema kwamba hii inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana ulituasa kwamba tulitaka suluhisho na mimi kuna masuluhisho manne makubwa, hakuna tatizo! Uhamishaji wa mifugo nalo limekuwa tatizo kubwa. Kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Hili nalo mbali ya kuharibu mazingira, lakini wananchi wamekuwa hawafahamiani.

Mheshimiwa Spika, jambo moja kubwa kuliko yote ni kwamba, wananchi waliochukuliwa maeneo yao na Serikali, hasa Jeshi la Wananchi Tanzania, muda wa miaka saba Serikali katika kitabu chake, taarifa ya utekelezaji wa haki za Serikali Mwaka 2007 iliahidi maeneo yale yote waliyoyachukua basi wataweza kuyapima kutathmini na kutoa fidia.

Ni mara kadhaa hapa, wananchi wale watafika wapi jeshini, wanaogopa jeshi watapata mkong'oto, wanaogopa kupigwa! Naomba nitoe maelezo yafuatayo maeneo maalum. Mkoa wa Arusha Oldani Nyasambu Tanganyika Perkers 1977 KJ, Mkoa wa Dar-es-salaam kuna *Kunduchi Transit Company, Kunduchi Rafel Ranch*.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dodoma, Matokopora Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Nakombania *Rader* Dodoma. Katika maeneo mengine, Mkoa wa Kagera kuna Biharamula 23 KJ. Nako vilevile kuna malalamiko wananchi hawajapewa haki zao.

Mkoa wa Kigoma Bulombola na JKT nako manung'uniko yamejaa. Mkoa wa Lindi Singino *Rader* nako wananchi wafikapo jeshini subutu! Mkongoto mkubwa tu. *(Makofi)*

Mkoa wa Mara, Ramkoma JKT, Kiabakari nako vilevile Buhemba JKT, Mkoa wa Morogoro, Chita nako na ngerengere huko maeneo ya Nachiku ya zamani Serikali iliahidi bado hamjatoa. Wananchi waende wapi na sisi ndio sauti zao pengine mtasikia mwaka huu 2015.

Mkoa wa Mtwara *Umoja Camp* nako wamechukuliwa ni hatari sana. Mkoa wa Ruvuma Mlale JKT na Tunduru *TPDF,* nako vilevile wananchi wanalalamika muda wa miaka mingi mliahidi na hamjawapa wenyewe! Mkoa wa Rukwa ni Kasanga *TPDF detached,* nako tatizo kubwa lipo. Mkoa wa Tanga Maramba JKT, Mgambo JKT na Songa KJ.

Mheshimiwa Spika, Kisarawe huko hatusemi maeneo kadhaa yamechukuliwa, hasa ni tatizo baina ya wananchi na Jeshi. Jeshi ndiyo Jeshi mwananchi atakwenda wapi? Sisi ndio sauti zao za wanyoge humu, ndio wawakilishi wao. Wametupa dhamana ya kuwaambieni ninyi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nini kifanyike, naomba mnisikie kwa makini sana kuhusu suluhisho la suala hili.

Mheshimiwa Spika, jana ulisema tulete suluhisho. Ombi langu la kwanza tatizo kubwa tulilonalo hivi sasa Serikali inasema haina fedha, sasa basi. Kwa kuwa kipindi hiki cha Bajeti kinamalizika Bajeti inayofuata ya 2015/2016 itabidi mambo ya msingi sasa tuyaangalie na fedha hizi zipatikane ili ziende vijijini, ardhi iweze kupimwa.

Kwanza kwenye *item 220400 Hospitality and supplies* fedha kwa ajili ya viburudisho, vitafunwa, chakula na vitu vitamu vitamu, mwaka huu Bajeti inayokuja katika Wizara zote na Idara zote fedha za viburudisho, vinywaji, mambo ya chakula na vitu vitamu vyote asilimia 75 iondolewe iende kwenye shughuli za upimaji wa ardhi. Ndiyo suluhisho la kwanza.

Mambo ya kula Wizarani mara hii ni maji tu kama kweli Tanzania ni nchi ya amani na utulivu. Tunataka watu wetu wasiendelee kufa basi tufunge mkanda, mambo ya kula, kuku, nyama, hakuna mwaka huu 2015/2016. Fedha hizi asilimia 75 zikatwe ziende huko kwenye kupima ardhi.

Mheshimiwa Spika, hilo ni la kwanza kama ulivyotusihi jana.

Mheshimiwa Spika, Pili; fedha za mbio za mwenge, kazi ya mwenge tumesema kwamba tunamulika maadui na pale penye chuki, kuweka upendo. Kuna chuki baina ya wakulima na wafugaji, utaratibu wa kuchangia kwa hiari fedha za mwenge zote pamoja na utaratibu mwingine mara hii mwenge usitembezwe, fedha zake kwenye Bajeti ya mwenge zichukuliwe ziende kwenye kupima ardhi.

Hakuna haja mara hii kufanya shughuli kubwa sana ya shughuli za mbio za mwenge, wanaochangia kwa hiari wachangie kwa hiari, fungu lake lililotengwa basi fedha za mbio za mwenge ziende kwenye kupima vijiji ili watu wetu wakulima na wafugaji wasipigane na wasife tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sherehe basi mwaka huu, tarehe 9 Disemba, 2015 mwaka huu sherehe ya uhuru ifanywe tu kama angalau katika asilimia 20, asilimia 80 ya fedha za sherehe za uhuru za mwaka huu ziende kwenye kupima ardhi ili watu wetu ajue haki zao na wapate maeneo yao.

Sambamba na hilo mwaka 2016 ikifika tarehe 26 Aprili, 2015 fedha zilizotengwa kwa ajili ya sherehe za Muungano zisifanyike kubwa kama ilivyo kawaida yake, fedha zote za sherehe za Muungano basi.

Sherehe zikafanywe kidogo tu kule Pemba mara moja tusikatae, angalau kwa asilimia 20 itoshe kama kweli tuna nia ya kweli kuweza kuwalinda wakulima na wafugaji wasipigane na vifo vikatoea tuwalinde kweli kuna haja gani ya kufanya sherehe kubwa ya Muungano? Sherehe za nini?

Kama kweli tuna nia ya dhati, kama tunapiga maneno tu ya kisiasa sawa, lakini kama tuna nia ya dhati kuwalinda kweli wakulima na wafugaji wetu wasipigane, sherehe za Muungano ziwe kwa asilimia 20 tu inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, safari za nje kila wakati ambazo hazina ulazima, mwaka huu 2015 itoshe zikatwe kwa asilimia 70, fedha zilizobakia zote ziende kwenye kupima vijiji huko ili mambo haya kidogo imekuwa ni aibu kubwa. Kisiwa cha amani! Ya nini sherehe kubwa kubwa kama tuna nia ya kweli?

Mheshimiwa Spika, sisi tunafuata utaratibu wako wa jana kwamba leteni suluhisho, hapa ni mapendekezo kama mkiyakubali kweli, mkiyakataa haya kumbe hamna nia njema kweli ya kuwalinda watu wasipigane na kuuana. Itakuwa mnapiga bla bla, mnapiga maneno siyo mazuri ambayo itakuwa hayaleti tija.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi mambo ya kwenda mkaleta Wawekezaji wengi ambao wawekezaji wenyewe hawana tija yeyote hii ni tatizo. Katika haya kila mmoja mara nyingi amekuwa akieleza suala zima la maafa ambayo yametokea.

Viashiria hivi na mataifa jinsi ambavyo yanatuthamini sisi Watanzania, kisiwa cha amani na kwa sababu sisi siyo kisiwa cha amani tena. Bunge letu linaonekana na taarifa zinasikika kwamba vifo vimetoka hapa, vifo vimetokea pale, vile vifo vya Kiteto ni aibu, Kilosa ni aibu, Rufiji huko ni aibu na Tunduru 2014 ni aibu.

Aibu hii mimi naona imetosha. Ni lazima tukae pamoja tuone hali halisi ilivyo na mambo kama haya ambayo yapo hivi sasa yasiweze kuendelea tena.

Mheshimiwa Spika, mwenzangu Mheshimiwa Machali aliongelea, rushwa na watendaji walio katika mipaka na vijijini. Katika watu ambao ni wa kuangaliwa kupita kiasi ni watendaji waliopo vijijini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Ushauri wako umekuwa mzuri mpaka nimesahau saa imeshapita.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Pauline Gekul atafuatiwa na Mheshimiwa……..! Mheshimiwa Pauline Gekul endelea. Kwanza nitamwita baadaye, wote muwe tayari. Nafanya kutafuta watu humu ndani.

**MBUNGE FULANI:** Sisi tupo.

**SPIKA:** Naona siyo kwamba sioni, ninaona. *(Makofi/ Kicheko)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikupongeze kwa namna ya pekee wewe kuunda Kamati hii Teule ambayo imetufikia katika maeneo yetu wakaona hali halisi wa yale mambo ambayo siku zote tumekuwa tukiyazungumza humu Bungeni.

Pia niipongeze Kamati hii ambao walijitolea usiku na mchana wakifanyakazi bila kujali itikadi zao za siasa, wakawa wamoja na niwapongeze ile timu ambayo ilikuwa Babati Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Joseph Selasini na Makatibu wao na wengineo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati yako ilifanyakazi nzuri sana na kwa namna ya pekee nilitegemea kwamba hii kazi ingekuwa imefanywa na Serikali na ndiyo maana ninakupongeza kwa sababu umesikia kilio cha Wabunge na ukaona kwamba kuna hatua ya kuchukua ili haya matatizo ya wafugaji na wakulima wa nchi hii yafikie mwisho.

Ili haya matatizo ya Wawekezaji na wananchi katika nchi hii yafikie mwisho. Ndiyo maana tunapochangia tungetamani sana Wabunge tuone Mawaziri ambao wanaguswa na Wizara hizi wanatulia na wanawahi katika nafasi zao ili wachukue michango yetu na wayafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, kama kuna Wizara imetendewa haki kipindi hiki kwa *document* hii ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, naamini kwamba hii *document* umeifurahia sana.

Wenzio wamekufanyia *research* ya bure na wamekuletea mambo mezani na ninategemea baada ya hapa Mheshimiwa wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, atazunguka maeneo haya ambayo pia yametajwa kwenye ripoti hii ya Kamati ili aone jinsi gani ya kutatua kero hizo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi yaani umeletewa ni mteremko ushindwe mwenyewe baada ya miezi sita tunakuja kukuuliza umefanya nini kwa sababu mambo yapo hadharani, ni wewe kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, napongeza Kamati hii kwa sababu wamegusa matatizo ambayo nimekuwa nikiyasemea katika Mkoa wa Manyara, wamegusa Kiteto, wamegusa Hanang', wamegusa Babati, wamegusa Simanjiro, Mkoa mzima wa Manyara. *(Makofi)*

Nategemea Waziri ziara yako ya kwanza itakuwa Mkoa wa Manyara kwa sababu Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa ambayo ina mashamba mengi pori, lakini pia ina mashamba mengi ya Wawekezaji ambayo hayapo *active.* Yamegeuka huko kuwa mashamba pori lakini wananchi wamekuwa wakikodishwa hayo mashamba na Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeeleza vizuri. Mfano wa mashamba haya yanapatikana katika ukurasa wa 51, naomba ninukuu katika ukurasa wa 51 wa kitabu chao. Hili jambo limekuwa likitusumbua sana pale Babati, ni suala zima la mashamba ya *RIVACU,* Kamati inasema:

"Kamati inapendekeza kuwa Bunge liitake Serikali kufuta umiliki wa mashamba ambayo Wawekezaji wanayakodisha kwa wananchi kama vile mashamba ya *RIVACU* yaliyopo Wilaya ya Babati".

Mheshimiwa Spika, ninapenda sana kuwapongeza Kamati hii kwa sababu wamezungumza kitu ambacho sisi Wabunge wa Babati tumekuwa tukikizungumza kwamba mashamba haya ya *RIVACU* zaidi ya heka 3000.

Mfano shamba ambalo lipo katika Vijiji vya Endasago, shamba ambalo lipo katika vijiji vya Dudie, Vijiji vya Ari, Dohomu, shamba hilo limekuwa likikodishwa kwa wananchi kwa muda mrefu sana.

Lakini leo ninafarijika kwa sababu Kamati imeeleza wazi wazi kwamba umiliki huu sasa uondolewe, wananchi wale wanaopakana na hilo shamba wapatiwe.

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema sana kwa Kamati yako kueleza bayana. Mimi nimefarijika sana kwa sababu sasa nategemea Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, utakwenda huko *RIVACU* uone hilo shamba, uone jinsi gani ambavyo Viongozi wa nchi hii wanalima hayo mashamba, wananchi wanakodishwa, mashamba ni ya Serikali!

Mheshimiwa Spika, tukifanya haya katika nchi hii hapatakuwa na migogoro ya ardhi kwa sababu vijana wengi watakuwa wameshapata hayo mashamba, hapatakuwa na kelele tena kuchinjana, nategemea kwamba hili Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi ataanza nalo.

Siyo tu shamba hili ambalo lipo kwenye Kata ya Ari, lakini Mheshimiwa Jitu jana amesema shamba la *RIVACU* ambalo liko Kata ya Mwada, huko Magugu, ambako pia Viongozi wanalima, Polisi wanalima hilo shamba kwa muda mrefu sana, lakini wananchi hawapewi.

Mheshimiwa Spika, binafsi nimefarijika kwamba sasa haya mashamba yanakwenda kuchukuliwa na Serikali na wanawapatia wananchi, maana yake wananchi wa maeneo hayo sasa wakae mkao wa kugawana hayo mashamba kwa sababu Bunge limeona hili na Serikali inakwenda kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo lingependa kusemea ni suala zima la Watendaji wa Serikali kutokufuata taratibu zilizopo. Ni dhahiri kwamba nchi hii tuna sheria za kutosha.

Yaani tuna sheria ambazo kwa kweli sioni kama kuna sababu ya kutuletea tena miswada humu ndani, kinachokosekana katika nchi yetu sasa ni utekelezaji wa hizo sheria, siyo kwamba watendaji wa Serikali hawafahamu wanachotakiwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 43 naomba ninukuu kwenye ripoti hii unasema hivi:-

"Migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Serikali, kipengele (b) Kamati inasema mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Kata ya Bagara Ziwani dhidi ya Halmashauri ya Mji wa Babati ni kutokana na baadhi ya wananchi hao kutokulipwa fidia stahiki".

Mheshimiwa Spika, taratibu na sheria za fidia katika nchi hii zipo, utaratibu wa kwamba mwananchi alipwe nini katika ardhi yake upo. Lakini Kamati imeeleza vizuri kwamba kinachokosekana nchi hii siyo taratibu na sheria ni utekelezaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka jinsi ambavyo Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Joseph Selasini walivyosikitishwa na huu mgogoro katika Kata hii ya Bagara na majibu waliyopewa Kamati ilivyofika katika Kata hiyo. Waliambiwa matatizo sasa Babati yamekwisha kwa sababu tuna *Sisal Estate* katika Kata Baisaka tunakwenda kugawa viwanja baada ya hilo shamba kurudishwa kwenye Halmashauri.

Lakini Mheshimiwa William Lukuvi Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi anisikilize, kinachoendelea sasa Babati katika shamba la *Sisal Estate*, watu wamegawana viwanja, wale mliowa-*qoute* kwenye ripoti yenu Mheshimiwa Jenista na Mhagama, Kamati yako hawajapewa fidia.

Madiwani wamegawana shamba hilo, wananchi wameachwa wakihangaika, wale ambao wamekuwa wakidai fidia katika Halmashauri ya Mji wa Babati.

Lakini kinachosikitisha viwanja hivyo vimegawanywa mwezi wa 12 ndani ya mwezi mmoja mwananchi auziwe alipe zaidi ya milioni mbili kwa kiwanja ilihali wale ambao walikuwa wakidai muda wote wakisubiri wapewe fidia wakiwepo wale wa Bagara Ziwani, waliokuwa wananyeshewa mvua *Police Barracks* wale wamama waliokuwa wanalia mbele yako. Mpaka leo hawana viwanja na watendaji wa Serikali wapo.

Mheshimiwa Spika, kama hilo halitoshi mimi niombe vyama vyetu pia viangalie kinachosababisha mgogoro wa ardhi Babati ni Madiwani tulionao na wewe ni Kiongozi katika Chama cha Mapinduzi. Nimeshawahi kusema hapa Madiwani wanachukua maeneo ya shule zaidi ya heka tisa Mheshimiwa Jenista Mhagama, ulisikia kwa masikio yako.

Lakini Diwani anahodhi maeneo na mashamba, shamba la Hanadeko Diwani anakanyaga hatua anawagawia watu mbalimbali, Serikali ipo, Mkuu wa Wilaya yupo, Mkuu wa Mkoa yupo. Ndiyo maana kuna wakati mimi ninasema nchi hii hatuna Serikali, Serikali iko wapi?

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Siasa viko wapi? Mwenyekiti wa CCM nikimwambia mfukuze huyu Diwani wanamlinda, wanachukua maeneo ya wananchi, watendaji wameungana na Madiwani, Chama cha Mapinduzi mko wapi? Migogoro kama hiyo ya wananchi mlitakiwa Chama msimamie kwa sababu Serikali yenyewe ni mkono wa Chama kilichoshinda.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakupongeza sana, Serikali tumewaeleza haya yote, wasipochukua hatua wananchi watachukua hatua.

Tunawapongeza Watanzania wameanza kuchukua hatua katika masanduku ya kupiga kura na mimi niendelee kuwasihi wananchi wangu wa Mkoa wa Manyara kama haya hayatatekelezwa, kama Serikali haitaingilia kati, kwa sababu *document* yenyewe tumeletewa ili wananchi wachukue hatua mikononi katika maamuzi ya demokrasia kwenye masanduku ya Kupiga Kura.

Mheshimiwa Spika, suala la Wawekezaji kutumia Jeshi la Polisi katika kutimiza matakwa yao, kuna wawekezaji ambao hawahangaiki kabisa kuendelezamashamba hayo, nitoe mfano wa shmba la *Singu Estate*. Mkuu wa Wilaya alishatoa kauli kwamba wananchi waachwe kusumbuliwa, lakini Jeshi la Polisi linachukuliwa na Mwekezaji, wananchi mazao yao yanafukuliwa wamelima msimu huu wa kilimo, Serikali inaangalia, hakuna mtu anayewanusuru wananchi dhidi ya Mwekezaji.

Wawekezaji wa nchi hii wanafahamu pia kuna Watanzania ambao wana uwezo wa kuwekeza. Hivi inawezekanaje Mwekezaji kubadilisha matumizi anaanza kupima viwanja na kuwauzia wananchi viwanja Serikali iko wapi?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesema Mheshimiwa William Lukuvi nategemea ataanza ziara yake kwenye Mkoa wa Manyara ili aone haya yote yaliyoandikwa kwenye *document* hii ayachukulie hatua, vinginevyo nchi hii imefikia hatua mbaya sana. Ukiona watu wanatoana roho, unaona mtu anamkata mwenzie, nimeona Kiteto watoto wadogo wamechinjwa, watu wazima wamechinjana, hii nchi imefika pabaya. Tukisema Serikali mko wapi?

Nimewahi kusema hivi Serikali mnakwenda *retreat*? Huwa mnakaa chini mkatafakari mlikotufikisha na Chama ambacho kinaongoza? Kama mnakaa mnategemea Bunge hili Spika ndiyo aagize kwamba haya ndiyo yafanyike? Kama sivyo mtuambie ndani ya miezi sita kabla ya Oktoba, 2015 ili Watanzania wajue ninyi mmeshindwa.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Wewe ndiyo umeharibu hali ya hewa. Waheshimiwa Wabunge naomba msiniandikie kuomba kuzungumza mtapata muda wote waliokuwepo hapa mtazungumza tu. Naomba msiniandikie nimechoka kusoma barua zenu.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Sara Msafiri, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia taarifa hii ya Kamati Teule. Kwanza niwapongeze Wajumbe kwa taarifa nzuri, na ninataka niseme tu kuwa kwa Mkoa wa Morogoro ambao umekuwa na migogoro ya Wakulima na Wafugaji kwa muda mrefu, kwa kweli Kamati imetenda haki imejaribu kugusa maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, ukisoma mapendekezo ya Kamati utaona kwamba walijikita sana kwenye hadidu ya rejea ambayo inagusia kuangalia masuala ya sheria na sera zote zinazohusu masuala ya ardhi na masuala ya ufugaji na maji na sheria zingine. Lakini ukiangalia migogoro ya ardhi imepita kiwango ni zaidi ya sheria, kwamba sheria ni jambo moja lakini usimamizi na utekelezaji wa sheria ni jambo jingine.

Kwa mfano, utaona kwamba kuna mashauri ya ardhi ambayo yamechukua muda mrefu sana kupatiwa ufumbuzi, kwa mfano kwenye Wilaya ya Morogoro Vijijini, kuna kijiji cha Kambala, mgogoro wa ardhi wa kijiji hiki ulianza tangu mwaka 1986, kipindi hicho Waziri Mkuu alikuwa ni Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba.

Mheshimiwa Joseph Sinde Warioba, alishatoa maelekezo kama Waziri Mkuu akaelekeza Mkuu wa Wilaya ashughulikie shauri hilo la mgogoro wa Wakulima na Wafugaji wa Kijiji cha Kambala. Lakini mpaka sasa tunavyoongea ni miaka 26 imepita hakuna ufumbuzi wa mgogoro uliopatikana.

Hivi tunavyoongea kuna kesi iko kwenye Baraza la Ardhi la Nyumba la Wilaya kuhusu kijiji hicho cha Kambala mpaka sasa hakuna suluhisho, wakulima na wafugaji wanapigana, wanauana, wanachinjana usiku na mchana. Kumekuwa na uhasama wa makundi haya mawili.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninaomba pamoja na kwamba tunataka kufanya marekebisho ya sheria na sera mbalimbali, lakini bado kuna wajibu wa kuhakikisha kwamba vyombo vinavyosimamia maamuzi vifanye utekelezaji wake kwa wakati.

Hatuwezi wananchi wa Mkoa wa Morogoro tunashuhudia migogoro ya miaka 28 kijiji kimoja, Serikali ipo, Uongozi upo, vyombo vya sheria vipo, lakini utekelezaji wake haujulikani utaisha lini. Ninaomba kabisa kwamba vyombo vinavyochukua maamuzi ni lazima viwe na muda wa kumaliza shauri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna tatizo la wananchi kutoheshimu sheria. Kwa mfano Kijiji cha Mabwegere kiko Wilaya ya Kilosa, Mkoa wa Morogoro.

Hiki kijiji kwanza upatikanaji wake haukufuata sheria za Serikali za Mitaa, haukufuata sheria ya Vijiji, wafugaji wanajua wenyewe wamepita njia gani kitongoji kikawa kijiji. Halmashauri haikushirikishwa, ikamega maeneo ya vijiji ambavyo vilikuwa halali.

Mheshimiwa Spika, Kitongoji kikawa Kijiji, Halmashauri haikushirikishwa, ikamega maeneo ya Vijiji ambavyo vilikuwa halali, ikachukua maeneo ya Kijiji cha Mfulu, Kijiji Mbigilo na sehemu ya Dumila ikajitangazia ni Kijiji.

Meshimiwa Spika, shauri limeenda mpaka Mahakamani, lakini tunashukuru kwamba, kwa sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeshaagiza kwamba maeneo yale yapimwe vizuri, Kijiji cha Mabwegere kichukue eneo lake na Vijiji vingine vichukue eneo lake halali. *(Makofi)*

Ofisi ya Waziri Mkuu imeishatoa agizo, Mkuu wa Mkoa aliyeondoka Mheshimiwa Bendera alishawakutanisha wadau eneo lipimwe, Mkuu wa Mkoa wa sasa hivi Mheshimiwa Rajabu Tendano, juzi amekaa na wadau wote wa Kijiji hiki, lakini cha kushangaza wananchi hawaheshimu maamuzi.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, wafugaji wamegoma kabisa kushiriki kwenye zoezi la upimaji pamoja na kwamba Kijiji kilipatikana isivyo halali, na wanafanya vurugu. Na hivi ninavyoongea, juzi wafugaji wamemjeruhi mwananchi wa Kijiji cha Mbigilo wamemkatakata mapanga, wafugaji wanatoka Kijiji cha Mabwegere wanaenda Vijiji vingine kufanya furugu. Ukifuatilia ni rushwa tupu kwa wafugaji wanatoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba kabisa kwamba lazima wananchi waheshimu sheria na lazima kuwa na *enforcement* ya hizi sheria. Kama maagizo yanatoka, wafugaji hawatekelezi, lazima itafutwe njia yoyote waondoe mifugo yao waache wakulima waendelee na shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kusikitisha, hivi ninavyoongea sasa hivi, Mkuu wa Mkoa ameagiza Jeshi la Polisi liwalinde akina mama wakienda mashambani. Wanakina mama wanaogopa kwenda kwenye shughuli za kilimo na tunajua kwamba wakina mama ndiyo wakulima wakubwa, ndiyo wanaoenda mashambani. Sasa nataka nikuambie, asilimia 80 ya watu wa Morogoro ni wakulima, tuna polisi wangapi wa Mkoa wa Morogoro kuwalinda akina

mama kwenda mashambani? Kwa hiyo, mimi nasema kabisa hili haliwezekani na halivumiliki. Lazima itafutwe njia ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kabisa kwenye ukurasa wa 8 wa Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mkoa wa Morogoro wamependekeza kwamba, kuwe na udharura wa kupima ardhi ya Mkoa wa Morogoro. Hili siyo pendekezo la muda mfupi. Hivi tunavyoongea, wakulima hawako mashambani, hawalimi, Serikali itapima lini ardhi ya Mkoa wa Morogoro ili hawa akina mama wakalime, wananchi wakalime. Lazima kuwe na *enforcement,* kama ni operesheni yoyote, hawa ambao hawatekelezi maagizo waondolewe, kwa njia yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba kuna agizo la Mheshimiwa Rais la mwaka 2002, Waraka Namba Moja, unazuia ufugaji wa kuhamahama. Tunakuwa kwamba kuna Sheria ya Ardhi ambayo ndiyo Sheria Mama, Sheria ya Mifugo, Sheria ya Maji na Sheria za shughuli zozote zile, Sheria Mama ni Sheria ya Ardhi, nayo inazuia ufugaji wa kuhamahama. Lakini, wafugaji wamekuwa wana kazi ya kuhama tu. Leo wako Ulanga, kesho wako kwenye Hifadhi, keshokutwa wako Kilosa, keshokutwa wako Mvomero.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nataka nikuulize, leo kuna mapendekezo hapa kwamba wafugaji wanahitaji majosho, wafugaji wana changamoto ya masoko, haya majosho yatakuwa ya kuhamahama? Leo hata Bunge likitoa hapa bajeti hayo majosho yajengwe, kwa stahili hii ya kuhamahama, leo wako kwenye Hifadhi, kesho wako kwenye Wilaya ya Kilosa, keshokutwa Mvomero, kweli zina uchangamoto kwamba wanahitaji majosho? Kuna josho la kuhama?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani, lazima kuwe na utaratibu, wafugaji waheshimu maagizo na sheria za nchi. Hapa haitawezekana wananchi wanauawa bila sababu, wakulima wanauawa bila sababu. Ukiangalia misingi ya hii migogoro ya wafugaji haipo Gairo. Iko kwenye Wilaya zingine

tu. Kimsingi robo tatu ya wananchi wa Gairo ni sungu sungu, ni askari wa jadi. Wanachofanya wao wakiona mfugaji ameingia shambani wanapiga filimbi, wanazunguka shamba, wanaua mfugaji, wanaua mifugo, na ndiyo maana hawakanyagi Gairo, wamebaki Kilosa, Mvemero, Ulanga.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tusiwalazimishe wakulima kutafuta njia yoyote ya kupambana na wafugaji. Lazima kuwe na operesheni maalum, maeneo ambayo yanajulikana ni ya wakulima lazima wafugaji waondoke hakuna njia yoyote. Tusiambiane kwamba tunakunywa maziwa, sijui tunakula nyama. Hapa tatizo siyo hilo, tatizo ni maeneo yatumike vipi!

Mheshimiwa Spika, leo unatoka Ulanga unahamahama unakuja unasema kwa sababu unauza maziwa, haiwezekani! Mnasema suala la soko! Mbona wakulima wao mazao yao wanakopesha mpaka Serikali, hawana masoko. Hata wakulima wana changamoto. Wafugaji ni watoa rushwa, ukisoma ripoti ya *RCC* utaona. wafugaji wana-*tamper* mpaka kutoa milioni 400 kuhakikisha mambo haya hayaendi.

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu sema siyo wote, unasema baadhi. Sasa wote tena! Hebu vizuri sasa. *(Kicheko)*

**MHE. SARA MSAFIRI ALLY:** Mheshimiwa Spika, baadhi! Lakini nikuambie hawa wafugaji leo wanalalamika wanataka Serikali iwasaidie majosho, lakini mfugaji mmoja wa Kijiji cha Kilosa ana mifugo 4,000 na ardhi ya Kijiji hicho ina uwezo wa kuchukua mifugo isiyozidi 800. Huyu mtu mwenye mifugo 4,000 anataka Serikali imjengee Rambo, mfugo mmoja anauza laki tano. Wakulima wameanzisha *SACCOS*, wanakopesheka, wanaungwa mkono…

**SPIKA:** Ahsante. Muda umepita. Mheshimiwa Halima Mdee atafuatiwa na Mheshimiwa Pareso. Mheshimiwa Pareso yupo?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, na mimi kama waliotangulia niipongeze Kamati Teule ya Bunge. Lakini nisikitike kwamba ukisoma ripoti yao wametumia taarifa zangu nyingi sana za miaka minne iliyopita kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, lakini wameshindwa hata kushukuru. Yaani nimewafanyia utafiti, wamekuja wamemeza, wameshindwa hata kushukuru. Kwa hiyo, narajia Mheshimiwa Ole – Sendeka aki-*wind up,* atashukuru Msemaji Mkuu wa Upande wa Upinzani ambaye… *(Makofi)*

**SPIKA:** Wamekushukuru pamoja na wewe. Haya tuendelee. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Mama wewe ndiye umeshukuru, hawajashukuru wao, kwa hiyo nilikuwa nawakumbusha.

Mheshimiwa Spika, la pili, kinachohitajika kutoka Serikalini ni dhamira ya kisiasa ya kutatua matatizo haya. Dhamira tu! Kwa nini nasema hivi, unakumbuka miaka minne iliyopita nilileta hoja binafsi hapa Bungeni. Hiyo hoja binafsi pamoja na mambo mengine, ilikuwa inahitaji mambo mawili makubwa. Lengo lilikuwa ni kutatua hali hii ya mivurugano ambayo inatokea sasa hivi na ambayo imekuwa ikitokea miaka kadhaa iliyopita.

Mheshimiwa Spika, tulisema, kwanza, Serikali isitishe kugawa maeneo kwa wawekezaji wakubwa wa ndani na wa nje ili tufanye tathmini ya ardhi tuliyonayo mkononi *(land auditing)*. Tukifanya tathmini tutajua mfugaji ana nini, mkulima ana nini, mwekezaji wa nje ana nini, mwekezaji wa ndani ana nini, raia wa kawaida wana nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ni mwaka wa nne hakuna kilichofanyika. Serikali ilienda kufanya utafiti, ilivyoenda kufanya utafiti, kibaya zaidi badala ya kwenda kufanya tathmini ya ardhi, aliyekuwa Waziri akaenda kukagua mashamba yaliyopo. Matokeo yake ni kwamba leo gharama za Serikali zimetumika, akatumia ndugu zake kuwaingiza

kwenye taasisi husika, pesa zimetumika, hakuna taarifa zilizo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukasema pia na ndiyo mapendekezo ambayo Kamati Teule tena inapendekeza, waende kuangalia ni kwa kiwango gani Vijiji vyetu vimekiuka Sheria Na. 5 ya Ardhi ya mwaka 1999, kwa sababu Serikali za Vijiji zinatoa maeneo kwa kiwango kikubwa kuliko hata mamlaka yao ya kisheria. Tukasema wakithibitisha yale maeneo yote yaliyotwaliwa kinyume na sheria yarudishwe. Hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza hapa kuwe na dhamira kwa sababu tunakoelekea kunatisha.

Mheshimiwa Spika, juzi Kamati ya Mambo ya Nje kwa mara ya kwanza ukurasa wa 21 wamezungumzia wimbi la uwekezaji katika ardhi ya Afrika na unyakuaji wa ardhi, Bunge la Afrika linajadili haya mambo. Mwaka 2012, 2014 baada ya sisi tumetoa hoja miaka minne iliyopita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo pamoja na upungufu, na nataka Waziri wa Ardhi anisikilize kwa makini, ukisoma hotuba zangu za miaka mine, ulikuwa hata huhitaji kusoma hii Taarifa ya Kamati Teule. Yaani nimeumiza kichwa, watu wanafanyia *thesis* ya *PhD,* lakini nyie mmekaa kaa tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na upungufu wa taarifa ya Serikali, imeonesha kwamba, kwa hayo mashamba yaliyofanyiwa utafiti, kwa wastani, raia wa kigeni wanamiliki shamba lenye ukubwa wa hekari 6,302, kwa wastani, raia wa kigeni. Wakati huo huo raia wa Kitanzania kwa wastani anamiliki hekari 280! *Shame!*

Mheshimiwa Spika, sasa leo tunazungumza hapa, kisa linakuja, hivi watekelezaji tuna dhamira toka moyoni? Taarifa ya Serikali inaonesha maeneo ya Dakawa kwa mfano, watu waliotumwa na Serikali yenyewe wameshindwa kwenda kupata taarifa sahihi kwenye mashamba 28 makubwa, kwa sababu haya mashamba yanamilikiwa na vigogo. *(Makofi)*

Sasa leo uende umkute kwa mfano, natoa mfano, Lowassa labda ana shamba, Sumaye ana shamba, Mkapa ana shamba, Lukuvi ana shamba, hivi tutakuwa tuna dhamira dhati? Nimesema kwa mfano Lukuvi, naona unanyanyuka nyanyuka inawezekana unalo. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumeambiwa hapa na ukienda kaangalie vile vitabu vinne, vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza, tafuteni wataalam wawatafsirie, vitabu vinne vilivyofanyiwa utafiti na aliyekuwa Waziri Tibaijuka pamoja na upungufu wake. Inasema kwamba mashamba makubwa 28, taarifa zimeshindwa kupatikana kwa sababu ni mashamba ya vigogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana una dhamira njema, lakini hii dhamira njema itatimia? Mwaka jana… kengele ya kwanza! Mwaka jana amezungumza hapa Mheshimiwa Gekul kwamba ni kweli ipo dhamira? Mwaka jana nashangaa Mheshimiwa Ole - Sendeka hajataja kwenye Kijiji cha Roiborosoti sijui, Simanjiro huko majina yao ni magumu. Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya, Brown Ole - Suya, amepora eneo la Kijiji, hekta 3,425, nyaraka za Serikali zipo, zinaonesha kwamba amechukua kinyume na utaratibu. Nyaraka kuanzia ngazi ya chini mpaka Wizara ya Ardhi, anatakiwa arudishe eneo, harudishi eneo. Na tunavyozungumza kampa eneo hilo Mzungu, ameishauza kwa mwekezaji wakati tunajua Sheria zetu za Uwekezaji zinasema nini!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tutaandika maandiko, lakini ni kweli haya maandiko tuna dhamira ya kuyatetea? Hiyo ndiyo *challenge*. Lazima tuamue sasa.

Mheshimiwa Spika, juzi kwenye Sensa tunaambiwa Watanzania itakapofika mwaka 2050 tutakuwa milioni 130. Hivi hii ardhi ambayo sasa hivi tuko milioni 48 tunapigana hivi, hiyo 2050 hao watoto tunawaandalia nini? Hivi fursa ya kilimo akili zetu zinafikiria mwaka mmoja, miwili, ama tunafikiria Tanzania miaka ijayo? Tunaambiwa ikifika 2050 mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa asilimia 70,

mahitaji ya chakula duniani yataongezeka kwa asilimia 70, kwa sababu tutaongezeka kutoka bilioni 7 mpaka bilioni 9.

Mheshimiwa Spika, hivi kama Tanzania yenye ardhi lukuki ya rutuba kama tunavyojiaminisha, hatujui akina nani wamechukua nini, tumejiandaa nini hivi? Hivi hao vijana tunaosema kuondoa, kupunguza ajira kwa vijana, bila ku-*focus* kwenye kilimo, bila ku-*focus* kwenye viwanda, hili tatizo la ajira litaishaje?

Mheshimiwa Spika, inasikitisha, Tanzania kwa mwaka mmoja tunaagiza chakula nje chenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 646…

**SPIKA:** Muda. Kengele imegonga bwana, tuendelejee. Haya Mheshimiwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Ole – Sendeka, ashukuru hapa, iwe kwenye *record. (Makofi)*

**SPIKA:** Aa kwa nini tunasema ovyo ovyo? Ukisema vizuri unaharibu maneno ya ovyo ovyo mwishoni.

Mheshimiwa Marombwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sabrina Sungura. Nimesema wote walioomba wanapata nafasi, kwa hiyo, msiendelee kuniandikia andikia mimi hapa.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika nashukuru na mimi kwa kunipatia nafasi kuchangia Taarifa hii ya Tume uliyoiunda kuhusiana na migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, nianze kusema tu naunga mkono kwa asilimia 100 mapendekezo yaliyotolewa. Lakini na mimi nina mapendekezo yangu mengine pengine nimwombe Mheshimiwa Ole - Sendeka aweze kuyaingiza katika taarifa yake wakati anapohitimisha.

Mheshimiwa Spika, kwanza kwenye hadidu ya nne imeeleza matatizo mbalimbali yanayotokana na suala zima

la ardhi yetu kuwa jangwa kutokana na ardhi kuwa... samahani.

Mheshimiwa Spika, kwenye hadidu ya nne ambayo inatokana na uchambuzi wa mikakati wa kulinda vyanzo vya maji. Katika Wilaya yetu ya Rufiji, chanzo kikubwa sana cha maji kwenye Wilaya ya Rufiji inatokana na Mto Rufiji. Napenda kukufahamisha pamoja na Watanzania, nilishatoa maelezo nilipoitwa kwenye Tume hii kwamba huu Mto Rufiji ambao ni miongoni mwa mito mikubwa kabisa kwa nchi yetu hii, baada ya miaka mitano inayokuja utakuwa ni mto *seasonal,* sio mto tena wa mwaka nzima. Utakuwa mto wa majira, kuna kipindi maji yatakuwepo wakati wa masika na wakati wa kiangazi maji yatakatika.

Mheshimiwa Spika, kwa nini maji yatakatika? Bonde hili la Mto Rufiji ambalo kwa kiasi kikubwa sana ni eneo la kilimo, limevamiwa na wafugaji kiasi ambacho hata yale mabwawa ambayo yalitokana na Mto ule kupinda pinda, *Oxbow Lake* zile, mabwawa yote manane yaliyokuwa katika Bonde la Mto Rufiji yamekauka, yote yalikuwa ni mabwawa makubwa mengine yalikuwa na uwezo wa kufikia mpaka kilometa 5. Sasa hivi ninavyozungumza kipindi hiki cha kiangazi hayo mabwawa yote yamekauka na yataendelea kukauka.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo linguine, wafugaji wamehama sasa hivi. Wafugaji wamehama kwenye mabwawa baada ya mabwawa kukauka, wamevamia mto Rufiji. Wanachimba njia ya kwenda kupeleka mifugo yao kwenye Mto Rufiji. Mto Rufiji una kingo ndefu, kwa hiyo, wanachimba ili wapate njia ya kupitisha ng'ombe waingie ndani ya Mto Rufiji kunywa maji ya Mto Rufiji. Kinachojitokeza ni nini? Yale maeneo ambayo wanayochimba kwenda kunywa maji, ng'ombe wale, wanaingizwa zaidi ya ng'ombe 3,000/4,000, wanaingizwa, wakati wa kuingia, mchanga unasombwa, unaingia kwenye Mto Rufiji.

Wanaingiza tena, wakati wa kutoka wanapandisha juu ule mchanga, wanauingiza tena kwenye Mto Rufiji. Kuna

baadhi ya maeneo unaweza ukavuka kwa mguu kwenye Mto Rufiji, jambo ambalo halikuwepo kwa miaka yote, ni kutokana na athari kubwa sana ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, sasa hili ni tatizo kubwa. Mimi nilikuwa na pendekezo la kwanza:-

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kwanza ni kwamba ni lazima Serikali itambue maeneo yote ya kilimo na yasiingiliwe na wafugaji likiwemo Bonde la Mto Rufiji, hilo la kwanza kabisa. Hatuwezi tukaendelea kuwapeleka mifugo tu watu wote tuwe wafugaji tu, haiwezekani. Na sisi tunahitaji kulima, na hili bonde ni la kilimo. Siyo bonde la kufuga hili, wafugaji waende maeneo yao na wakulima wakae maeneo yao. Hili siyo eneo la ufugaji. Hilo pendekezo langu la kwanza ambalo nalitoa.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, kuna kesi nyingi sana za wakulima. Kule Rufiji sisi tumeshazoea kwa miaka mitano hii, tumezoea kesi baina ya wakulima na wafugaji na mauaji yanatokea. Juzi juzi tu mwezi wa Desemba zimetokea fujo kubwa sana kwenye Kijiji changu cha Njia Nne pale Rufiji, kesi kubwa sana na mvurugiko. Wafugaji wameingiza mifugo yao kwenye shamba la mkulima, wamekula zaidi ya heka 30!

Mheshimiwa Spika, sasa suala hili kwa kweli, linaleta matatizo. Mimi naiomba Serikali kuhusiana na suala hili, wafugaji wote ambao wapo katika Bonde la Mto Rufiji ni lazima tuwe na hatua, sio za muda mrefu, hakuna sababu ya hatua za muda mrefu, tuwe na hatua za muda mfupi, kwa sababu, kila kesi inayopelekwa Mahakamani baina ya mkulima na mfugaji wanashinda wafugaji tu! Hakuna hata kesi moja aliyoshinda mkulima! Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna hata kesi moja aliyoshinda mkulima! Mazao yanaliwa na yanaonekana kuliwa. Mifugo inakamatwa, unapeleka Mahakamani, unapeleka Polisi, hakuna hata kesi moja mkulima ameshinda, haipo! Wanaoshinda wafugaji tu kwa sababu, wao wenzetu

wanapesa! Wakulima hawana pesa! Akiuza ng'ombe wake anaweza kutoa rushwa! Samahani Mheshimiwa alizungumza pale kwamba, wafugaji wote wanatoa rushwa, hapana, mimi siwezi kusema hilo, lakini kuna rushwa kubwa sana baina ya wafugaji wanapovamia mashamba ya wakulima, inapopelekwa Polisi au Mahakamani, hakuna! Nenda Rufiji, wapi palitokea wafugaji au mkulima akashinda kesi? Ni chache mno! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia, kuhamisha mifugo. Mpaka sasa hivi mifugo bado inahamishwa! Jamani hiyo *operation* bado inaendelea?

Mheshimiwa Spika, tarehe 31 mwezi huu, tarehe 30 mwezi wa Desemba, mimi nimeona kwa macho yangu malori matatu yamechukua ng'ombe, kutoka wapi sielewi! Yalikamatwa pale Kibiti Polisi yakawa yanasafirisha wanadai wanakwenda Kilwa! Malori matatu tena yana *semi-trailer* nyuma yake wamefunga, yana ng'ombe zaidi ya 200, wanachukuliwa wanadai wanapeleka Kilwa!

Mheshimiwa Spika, lakini hawa wote hawaendi Kilwa! Wakishavuka tu wakishafika Kilwa, usiku kwa usiku wanaingia kwenye Bonde la Mto Rufiji. Sasa suala hili mimi nilikuwa naiomba Serikali na Mheshimiwa Mwenyekiti Ole - Sendeka nakuomba sana kwamba, kuanzia sasa vibali vyote vya kusafirisha mifugo kupeleka maeneo ya Kusini vifutwe. Kusiwe na vibali vya kusafirisha hawa! Unasafirisha kwani tuna *operation?*

*Operation* iko wapi sasa hivi? Hatuna *operation* sisi! Hawa waliokuwepo huko tutafute njia ya kuwatoa, lakini isiwe tena, *operation* ilifanyika kwa ajili ya kuwatoa watu wa Ihefu, hivi mpaka leo inaendelea?

Mheshimiwa Spika, naomba sana vibali vyote ambavyo vinatumika kusafirisha mifugo kupeleka maeneo ya Kusini, sisi Wilaya ya Rufiji tulitakiwa tuwe na ng'ombe 30,000, tu tuliomba, lakini sasa hivi kuna ng'ombe zaidi ya

300,000! Wamezidishwa mara kumi zaidi, kwa nini? Hatuna hata mahali pa kuwaweka, ni migogoro tu! Hatulimi hatufanyi jambo lolote lile, maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba, nchi yetu hii inahitaji sana amani. Nchi yetu hii inahitaji sana utulivu. Sasa hivi maeneo ya Rufiji hakuna utulivu baina ya wakulima na wafugaji, haupo. Sasa hii amani tunayoipigia kelele kila siku inaishia wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini kibaya zaidi ukienda Rufiji sasa hivi, Kamati imefika kwenye Vijiji viwili tu, waende maeneo ya *Delta* waone athari ya ng'ombe waliokaa kwa miaka mitano tu, ni jangwa! Tutaendelea kuona majangwa mpaka lini? Wamemaliza Shinyanga kwao huko na maeneo mengine, wanakuja kutuletea sisi kule, hatutaki hiki kitu! Jangwa hili linalozidi kuendelea na nakuomba, mimi siongopi, kama kuna uwezekano tuondoke na watu sasa hivi Waheshimiwa Wabunge, twende Rufiji mkaone namna gani athari ya ng'ombe kwa miaka mitano tu walivyosababisha jangwa kwenye Wilaya ya Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mimi nimalizie kwa kusema, tunaomba sana Serikali iweke rasmi, itangaze rasmi, Rufiji ni Bonde la Kilimo na wala sio la ufugaji na wafugaji waondoke. Namshukuru sana Mheshimiwa Huvisa, alikwenda akaona, akakemea.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Sabreena, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Pareso.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwanza kabisa, ningependa niipongeze Kamati Teule iliyoteuliwa na Bunge, iliyoongozwa na Mheshimiwa Ole - Sendeka kwa kazi nzuri ambayo waliifanya. Nawashukuru sana kwa niaba ya Wabunge, angalau wametupa mwanga ni jinsi gani sasa tutaweza

kurekebisha sera yetu ya sheria mbalimbali kuhusiana na masuala ya ardhi, maji, mifugo na kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ningependa kuongelea suala zima la wawekezaji ambao wanakuja kuwekeza bila kupita kwenye Kituo chetu cha Tanzania *Investiment Centre* na hivyo basi kuifanya Serikali kukosa mapato.

Mheshimiwa Spika, ni suala la ajabu, ukiangalia katika Sheria zetu za Ardhi za Vijiji, Maafisa Ardhi Vijijini wanaruhusiwa kutoa ardhi isiyozidi heka 50, lakini mwekezaji anakuja anachukua heka 100, heka 1,000, heka 2,000, anapita juu kwa juu, anatoka Ulaya mpaka Kijijini anachukua ardhi, nchi haijui, Serikali haijui!

Mheshimiwa Spika, tukisema Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imelala, tutakuwa tunakosea? Kwa sababu, huu ni uzembe wa hali ya juu. Nchi ambayo ina viongozi kuanzia *level* ya Kijiji, *level* ya Mtaa, *level* Kata, tuna Maafisa Usalama kila Wilaya, inakuwaje watu wakubwa wanatoka nje ya nchi wanachukua ardhi, wanalima, wanavuna, wanasafirisha mazao! Tanzania *Investiment Centre* iko pale, hawapiti na kodi ya nchi hailipwi! Hii ni dosari kubwa sana kwa Serikali na ni lazima Serikali ijipange ni jinsi gani itakabiliana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, ukitoka hapa Dodoma ukielekea Morogoro kama unaenda Dar es Salaam, ukiangalia, kuna mashamba makubwa sana yanamilikiwa na viongozi wengine wako humu, Marais Wastaafu, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, wananchi wa kawaida, wana heka 5,000 mpaka 100,000, lakini heka hizo ni mapori, zinafugwa mbuzi, hamna kazi yoyote inayofanyika, lakini tukikaa tunasikia wananchi wanauwana kwa sababu ya heka mbili, tatu, nne mpaka tano! Hii ni kinyume na haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mtu mmoja umiliki ardhi zaidi ya heka 100,000 na mwananchi mwingine hata heka tano hana. Kila siki Watanzania tunasikia wanauwana

kwa sababu ya ardhi. Sasa kwa nini tunakuwa wabinafsi unamiliki ardhi kubwa, unaacha wananchi wa Tanzania ambao ni wanyonge wanapigana wanauwana kwa heka ambazo ni chache sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuangalie suala zima sasa la ugawaji wa ardhi na ikiwezekana tuwekeane kikomo tu, hata kwa sisi Watanzania. Unapewa heka za mfano, kwa mfano labda heka 50, umeshindwa kuziendeleza, unapunguziwa. Lakini tabia ya watu wa ardhi kutoa heka ma-elfu na uendelezaji hakuna, hiki ni kinyume cha haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongelee eneo la *EPZ*. Kule kwetu Kigoma kuna eneo la Katosho, wale wananchi karibia mwaka wa nne sasa hivi hakuna kinachofanyika. Watu wanasubiri fidia, fidia haiji! Serikali imekuwa na tabia siku hizi ikitaka eneo, kabla haijapata hela inahamisha wananchi! Huu ni usumbufu! Kwa nini, msiwe mnatafuta fedha kwanza, halafu ndio mnaenda kuwahamisha wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale Kigoma kuna Mlima unaitwa Mlole. Mwaka 2006 alipita Mheshimiwa Rais akatoa agizo akasema kwamba, Mlima huu u-*stop* kujengwa kwa sababu, michanga inayotoka kwenye mlima ndiyo inaenda kuzuwia kina cha maji cha Mto Tanganyika. Ni mwaka wa tisa fedha hakuna!

Mheshimiwa Spika, na pale kuna lugha ambazo zinakingana! Wenyewe wanasema kuna *two schools of thought,* kuna wanaosema kwamba, mchanga unaoenda kujaa Bandarini unatoka katika Mfereji wa Rubengela, lakini kuna wataalamu wengine wanasema mchanga ule unatoka kwenye mlima.

Mheshimiwa Spika, lakini japo kuna *schools of thought* ambazo ni mbili na zinatofautiana na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na ukiangalia ni miezi kadhaa imebakia Mheshimiwa Rais anaondoka madarakani! Ni mwaka wa 10

wananchi wana sintofahamu hawajui nini hatima ya maisha yao. Manispaa imekiri kwamba haina uwezo wa kulipa fidia ya bilioni tano, Mkoa na wenyewe haujatoa tamko lolote kuhusiana na fedha hizi; wenzetu wa Serikalini mnasemaje fidia zaidi ya miaka tisa? Wananchi wako *stranded!* Wanashindwa kuendeleza miji yao, wanashindwa kuendeleza nyumba ili wapangishe watu, wanataka kusikia majibu kuhusiana na masuala haya ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama fedha imekosekana, basi ni vyema wananchi wale waambiwe waendelee kuishi kama zamani. Kama fedha ipo angalau muwape matumaini wananchi hawa, lakini kwa kweli, fidia imekuwa ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, tuna eneo la *Airport* na lenyewe linahitaji fidia. Mradi ule ulikuwa unachangiwa na Serikali kwa 17% na *World Bank* walikuwa wanachangia kwa 83%, lakini hiyo 17% ya Serikali mpaka sasa hivi haijatoka!

Sasa ni lini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itaacha kuanzisha miradi kabla ya kupata pesa? Kwa hiyo, ni vizuri tujitathmini tunapoenda kwenye miradi tuhakikishe kwamba, tuna fedha mikononi na hivyo ndio tuwe tunaenda kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ningependa kuongelea ni kuhisiana na hizi aina za ardhi. Katika Ripoti hapa tumeona ardhi imegawanyika katika sehemu kuu nne; kuna Ardhi ya Kijiji *(Village Land),* tuna Ardhi ya Akiba *(Reserved Land),* tuna Ardhi ya Umma kwa *(Public Land),* lakini tuna ardhi hatari (*Hazard Land)*.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea hii ardhi hatari. Ukiangalia maeneo ya Dar esSalaam, maeneo ya mabondeni, Kigogo, Magomeni na maeneo mengine Kinondoni; kumekuwa kuna tabia mvua zinaponyesha na mafuriko yanapozidi kwenda katika maeneo ya mabondeni wananchi wengi kuathirika na hivyo Serikali kubeba mzigo wa kuwahamisha na kuwapeleka maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini cha ajabu katika hii ardhi ambayo tunasema ni hatari huduma za kijamii zote zinapelekwa. Ukiangalia, maji mabondeni yanapelekwa, umeme mabondeni unapelekwa, njia zinatengenezwa na Serikali, lakini hapohapo tunasema ardhi hii ni hatari! Sasa Serikali ina mkakati gani ili kuepuka hizi gharama za kila siku? Watu wako maeneo hatarishi! Ndio, utamlipa mtu gaharama aende mtu gharama aende eneo lingine, wale wanaopoteza uhai mtawalipa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii Serikali kama iko makini ni lazima hatua za makusudi zichukuliwe kuhakikisha kwamba, ardhi ambayo ni hatari yenye unyevu, yenye mafuriko, Watanzania wanakuwa wanaondolewa katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ambalo tunaliona ni utoaji wa hati. Wizara ya Ardhi imekuwa inachelewesha sana utoaji wa hati kwa wananchi. Ukiangalia sheria inasema Mtanzania anatakiwa apate hati ndani ya miezi sita, lakini watu wanaomba hati miaka mitano mpaka kumi! Hati hazitoki! Hapo Ardhi kuna shida gani?

Mheshimiwa Spika, ni lazima sasa wenzetu wa Ardhi, ili kuendelea kupunguza migogoro ya ardhi nchini wahakikishe wanatoa hati na kwa wakati. Kuna kesi nyingi sana ya nyumba moja ama kiwanja kimoja unakuta kina hati mbili mpaka tatu! Hapo mwenye hati atajulikana ni nani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vyema hati zitoke kwa wakati na zitoke zikiwa katika hali ya usawa, ili kuepusha migogoro baina ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini suala lingine ambalo ningetaka kuongelea ni kuhusu viwango vya fidia. Kumekuwa kuna tatizo, ukiangalia Sheria ya Ardhi inasema fidia stahiki na ya haki itolewe kwa wakati bila kucheleweshwa pale ambapo ardhi ya Watanzania inataka kutwaliwa, *either* kwa *public interest* ama kwa *interest* zozote nyingine ambazo Rais ataona zinafaa.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye ukokotoaji wa fidia kumekuwa kuna tatizo kubwa. Sheria ni ya zamani sana, kwa hiyo, kanuni zinazotumika kukokotoa zile fidia unakuta haziendani na bei ya soko. Kwa mfano, hapa Dodoma Mjini, tuseme Dodoma Kati, unaweza kukuta bei ya soko ya nyumba sasa hivi ni kuanzia milioni 60 mpaka 100, lakini Serikali inapokuja kulipa fidia wenyewe hawaangalii bei ile, wenyewe wanaangalia sheria, wanathaminisha nyumba, wanaangalia bei ya kiwanja kwa wakati huo, wanalipa fidia, lakini ile fidia inakuwa haitoshelezi. Kwa hiyo, ni lazima Serikali sasa ifanye marekebisho katika ukokotoaji wa fidia pale ambapo inakuwa inataka kuwalipa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu ya masuala ya ardhi. Wataalamu wetu wa ardhi kuanzia vijijini, wananchi, Mabaraza ya Ardhi, hawana elimu nzuri ya uelewa wa ardhi. Na nafikiri kama nchi, kama tuta-*invest* watu hawa wapate elimu ya masuala ya ardhi kwa kiasi kikubwa migogoro mingi itaweza kupungua. Na inawezekana hata hili jukumu la kusema kwamba, wenzetu wa vijijini wanatakiwa watoe mwisho heka 50, elimu hiyo watu wengine hawana!

Mheshimiwa Spika, Mtanzania anaenda kuomba heka 100, heka 200, uongozi wa Kijiji unakaa unampa zile heka! Kwa hiyo, mtu kama yule anakuwa hajapata elimu ya kutosha; kafanya kosa kisheria, lakini elimu hana! Serikali mnajipangaje kutoa elimu stahiki kwa viongozi wetu wanaoshughulikia masuala ya ardhi kuanzia *level* ya Vijiji, Mitaa, Kata na kuendelea?

Mheshimiwa Spika, ni wakati muafaka sasa Serikali iwekeze katika Mabaraza ya Ardhi; muweke Wataalamu wa kutosha, muwalipe mshahara, mtafute fedha muwalipe mshahara.

Mheshimiwa Spika, kama kila Mtanzania anayemiliki nyumba atakuwa na hati, na huyo Mtanzania baada ya kuwa na hati atakuwa na sifa ya kukopa benki na siku hizi mabenki kuna utaratibu ukienda kukopa mkopo ukipeleka

hati, unaulizwa kwanza kama umelipia kodi ya ardhi. Kwa hiyo, kama kila Mtanzania anayemiliki nyumba akiweza kuwa na hati na akalipia kodi ya ardhi, Wizara ya Ardhi itapata mapato ambayo hayajawahi kutokea nchi hii na hivyo wataweza kuendesha vyema Mabaraza yetu na kutoa elimu ya…

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa.

Waheshimiwa, naomba niwatambue baadhi ya wageni walioko hapa ndani. Tuna wageni wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi kutoka Kampuni ya *V One International Trading Company Ltd.* Inayofanya biashara mbalimbali ambayo Makao Makuu yake yapo Hong Kong. Huyu ni ndugu Deng, hapa itakuwa shughuli hapa! Deng Kuyang – *CEO,* Yuko Karo Du – *Sells Manager,* yuko Cheli Wang – *Sells Manager,* yuko Jackson Basu – *Tanzania Representative*. Naomba wageni hao wasimame! Ahsanteni sana karibuni. *(Makofi)*

Tuna wageni 80 wa Waheshimiwa Wabunge wa *CCM* Mkoa wa Mbeya kutoka Vyuo vya Mtakatifu Yohana *(St. John)* na *UDOM,* wakiongozwa na Mkuu wa Msafara Ndugu Godfrey Kibona. Naomba hawa nao wote wasimame walipo! Hawa wanafunzi wa *UDOM* na *St. John!*

Ahsante. Karibuni sana na nawatakieni kisomo chema.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Richard Ndassa, wanafunzi wa kutoka *Sumve Girls High School,* wakiongozwa na Mwalimu Herman Shingisha, Ester Nyanda na Mheshimiwa Diwani wa Sumve, Gervas Kitwala. Naomba hawa wageni wa kutoka…, hawa wasichana wa kutoka shule hiyo, wasimame! Ahaa! Kumbe ni wote! Alaa! Ahsante sana! Mmpendeza sana. Tunawashukuru Walimu kwa kuwafundisha na ninyi wenyewe msome. Mnaona hapa Waheshimiwa walioko hapa wamesoma, kwa hiyo, na nyie msome vizuri, tunawategemea sana. Sisi hiyo kwetu inaitwa mbegu! Kaeni!

Ahsante sana kwa kutuletea hawa wasichana wetu hawa.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Esther Matiko, ambaye ni Ndugu Charles Ihechi, ni mwanafunzi wa Chuo cha Utalii Musoma. Yuko wapi bwana Charles? Yuko wapi? Nadhani atakuja baadaye.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Stephen Masele, Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambao ni Ndugu Jumanne Maziku, Juma Derefa, Jackson Mhandi na Joseph Mpinginya. Wasimame walipo! Nafikiri tuliwatambulisha hata jana!

Tuna wageni wa Mheshimiwa Susan Kiwanga kutoka Mkoa wa Morogoro ambao ni Ndugu Shaban Mikongolo, Mwenyekiti wa Wilaya ya Kilombero – *CHADEMA*. Yupo Diwani Mheshimiwa Peter Lijualikali, halafu yuko Katibu, Ndugu Moses Kisemine, halafu yuko Mwenyekiti wa Wazee, Ndugu Henry Kanunga, halafu Katibu wa Wazee, Ndugu Niko Shaurimbele, Mwenyekiti wa Kijiji, Ndugu Renatus Mbamilo, yuko Mwenyekiti wa Kijiji, Prosper Komba na Katibu wa *BAWACHA,* Ndugu Mwanaidi Mpeta. Naomba hawa wasimame walipo. *(Makofi)*

Ahaa! Ahsante sana. Nimewataja wengi, lakini naona wako wachache.

Wageni wa Mheshimiwa Josephine Chagula, ni watoto wake, wasimame! Yuko Ndugu Emmanuel Chagula, yuko Francisco Chagula, yuko Rosemery Peter na Ndugu Lydia Sospeter, wasimame walipo. Ahaa! Ahsante sana. Haya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni 52 wa Mheshimiwa Rose Kamili, ambao ni Wajumbe wa Chama Cha Wafugaji Tanzania wakiongozwa na ndugu Edward Kwawoga. Naomba wasimame hawa wageni wa Mheshimiwa Kamili. Aa, ahsante sana! Karibuni sana. Karibuni sana, tumefurahi kuwaona.

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa John Shibuda ambao ni viongozi wa Chama cha Wafugaji kutoka Kanda ya Ziwa wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Juvenile Mrashani na Katibu wa Chama Ndugu Kusundwa Wamarwa, hawa wasimame walipo kama wapo naona wapo wachache, lakini karibu sana.

Matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo mara baada ya kuhairishwa Bunge hili kutakuwa na kikao kifupi kwa Kamati katika ukumbi namba 229 ni baada ya kuhairisha kikao leo ni jumamosi kwa hiyo baada ya kuhairisha kikao.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji Mheshimiwa Prof. Peter Msolla anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo mara baada ya Bunge kuhairishwa kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi namba 231.

Kwa hiyo tunaendelea nilimtaja Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika taarifa hii ya Kamati Teule ya Bunge na niungane na wenzangu kuwapongeza sana Kamati hii kwa kazi kubwa waliyofanya ya angalau kuibua baadhi ya matatizo yaliyo mengi ya ardhi hapa nchini, lakini pia na matatizo yaliyopo kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, ardhi ni utajiri mkubwa kwa nchi yoyote na ardhi hii ya Tanzania na ukubwa uliopo kama ingetumika vizuri nchi hii ingekuwa na utajiri wa kutosha, mkubwa na utajiri wa milele kwa maana ya vizazi kwa vizazi, lakini badala yake katika miaka 53 ya Uhuru tumeendelea kushuhudia matatizo makubwa ya ardhi, matokeo yake tunaendelea kuona wananchi wanataabika, matatizo makubwa ya ardhi kati ya wananchi mmoja mmoja na

mwingine, kati ya kijiji na kijiji, matatizo ya ardhi kati ya wananchi na wawekezaji, matatizo ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, matatizo ya ardhi kati ya wakulima, wafugaji, wananchi na hifadhi mbalimbali za Taifa.

Kwa hiyo, matatizo ya ardhi yanaendelea kukua badala ya kuona haya matatizo ya ardhi yanaendelea kupungua matokeo yake yanakua na leo tupo katika miaka 53 ya Uhuru wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba Serikali iliyopo madarakani imeshindwa kupangilia au kuwa na mipango bora ya ardhi kwa ajili ya wananchi wao. Kwa hiyo, wananchi huko walipo, wanavyoteseka kwa namna moja ama nyingine kuhusiana na matatizo yote ya ardhi mwaka huu ni mwaka wa kufanya maamuzi kwamba tupate Serikali nyingine ambayo itaweza kusimamia masuala ya ardhi kwa ujumla na waweze kunufaika na ardhi katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia taarifa hii wameonyesha baadhi tu ya migogoro ya ardhi. Kuna matatizo mengi mfano katika Jimbo la Karatu tuna matatizo kibao pia ya ardhi, mfano kuna wananchi wa shamba mojawapo linaitwa Shamba la Tembotembo wana matatizo ya ardhi kati ya mwekezaji. Wananchi wameishi pale karibia miaka hamsini leo anakuja mwekezaji anawatoa wananchi wale waondoke, mwekezaji anadai ardhi ni yake wakati ardhi ilitelekezwa maana yake ni kwamba hata Ofisi zetu za Halmashauri mbalimbali nchini kuna matatizo, kuna rushwa, mtu akiwa na hela, mwekezaji ana hela anahonga anafanya ujanja anapimiwa mwisho wa siku anamilikiswa wananchi wanataabika.

Mheshimiwa Spika, huu ni udhaifu pia katika mifumo yetu ya ofisi za ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini, kuna urasimu kwanza wenyewe hawakai ofisini hapa naongelea Halmashauri zote nchini, kuwapata ofisini huwapati, wananchi wanarudi mara mbili, mara tatu kupata huduma za ardhi hawapatikani lakini hata upatikanaji tu wa hati za ardhi kuna urasimu, kuna mlolongo, inachukua

muda mrefu, wananchi wanapata adha hiyo, lakini hapa pia kwa urasimu huu wa kupata hati za ardhi maana ndiyo tunapokaribisha rushwa. Kuna rushwa sana katika idara zetu za ardhi katika Halmashauri zetu, watu ambao au watumishi ambao wanakuwa na matatizo ya namna hii badala ya kuchukuliwa hatua ikithibitika wamepokea rushwa au wamefanya *double allocation,* ama tatizo lolote ambalo wamelisababisha katika nafasi zao matokeo yake anahamishwa.

Mheshimiwa Spika, hakuna Idara katika Halmashauri zetu ambayo watumishi wanahamishwa mara kwa mara kama Idara ya Ardhi. Anaharibu, *double allocation* kibao, anahamishwa Halmashauri nyingine au anahamishwa Mkoa mwingine.

Mheshimiwa Spika, tumechoka kuzungumzia hayo matatizo kama Wabunge, muda mwingi tumesema hatujawahi kuona hatua ya dhati ya Serikali kuondokana na matatizo haya yanayosababishwa na watumishi wa nchi hii ambao wanasababisha matatizo mbalimbali ya ardhi katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Sheria Namba 5 ya Ardhi inatambua ardhi za vijiji na kwamba mamlaka ya ardhi zote katika vijiji itakuwa ni kwa Mwenyekiti wa Kijiji na Serikali yake, lakini mwisho wa siku wanapotaka kugawa ardhi yoyote wataenda kwa mikutano mikuu ya vijiji. Sheria ile ni nzuri, lakini ikija kwenye utekelezaji hata hawa wenyewe Wenyeviti wa Vijiji hawana uelewa wa kutosha wa sheria husika na juzi tumefanya uchaguzi tumepata Wenyeviti wa Vijiji nchi nzima, tungefikiri ni vyema sana Serikali mkaenda kutoa elimu hawa Wenyeviti wa Vijiji na Wajumbe wao wote na ile Kamati ya Ardhi wakawa na uelewa mpana wa kusimamia Sheria Namba 5 ya Ardhi katika maeneo yao ya vijiji, hii itasaidia sana kuondoa urasimu, itasaidia kuwajengea uelewa matokeo yake hata wakienda kwenye mikutano mikuu ya vijiji kupata ridhaa au kupata kibali cha ugawaji wa ardhi katika maeneo yao waweze kugawa kwa haki ili kuendelea kupunguza matatizo ya ardhi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pia wawekezaji mbalimbali wanaokuja nchini wanapewa ardhi na tunashangaa sana Serikali hii ya CCM wanathamini kweli wawekezaji wanaotaka ardhi kuliko hata hawa wananchi ambao wanawapigia kura. Mnaona wawekezaji ni bora sana, wanachukuliwa kama miungu vile, mnawaona ni bora mnadharau wananchi, mnawapa ardhi kubwa, wanamiliki ardhi kubwa, wanapata hati kirahisi ya umiliki wa ardhi, wananchi hawawezi kusogea katika maeneo yao, wananchi wanaozunguka maeneo hayo wananyanyasika kwa kiasi kikubwa. Tutakuwa tunawashangaa sana mnathamini watu baki wanaotoka nje kuja kama wawekezaji kwa maana wasiokuwa wazawa halafu mnadharau wazawa, wananchi wanaozunguka katika maeneo ambayo wawekezaji wanapewa.

Mheshimiwa Spika, huu ni udhaifu mkubwa kwa Serikali iliyopo madarakani kuthamini wawekezji, kuwapa ardhi kubwa bila kuwashirikisha wananchi mwekezaji tu anakuja na kibali huko wanaambiwa wananchi wa eneo "X" hameni hapa muwekezaji amepewa eneo bila kuwashirikisha.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili tutapiga sana kelele, tutasema sana kama hamsikii nikatoa rai kwa wananchi mwaka huu ni mwaka wa kufanya maamuzi tufanye maamuzi katika maeneo mbalimbali tunapofika Oktoba siku ya kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, pia ardhi ikitumika vizuri maana yake utaweza kusaidia makundi mbalimbali katika jamii kwa maana ya vijana, wanawake waweze kutumia ardhi ile kujiajiri na kujipatia kipato na kuongeza uchumi wa kaya zao au uchumi wao binafsi na familia zao. Vijana wengi wanataabika, vijana hawana mwelekeo, vijana wako ambao wamekuwa na vyeti kwa maana ya kusoma vyuo, wana vyeti angalau wanatafuta ajira wanaweza labda kuajiriwa kwenye sekta binafsi au sekta ya umma lakini nazo ajira imekuwa ni changamoto, lakini kuna kundi kubwa la vijana ambao wanamaliza tu labda darasa la saba,

wanamaliza *form four* hawana uwezo wa kuendelea vijana hawa kama wangewekewa mkakati mzuri wa kutumia ardhi ya nchi hii vijana hawa wangeondokana na umaskini, vijana hawa wangejua hatma ya maisha yao, vijana hawa wangefurahia kuwa Watanzania matokeo yake vijana wa leo wanajuta hata kuwa Watanzania kwa sababu hawajui hatma ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaitaka Serikali kuhakikisha kutumia ardhi iliyopo katika nchi hii kuwasaidia vijana wa nchi hii waweze kujiajiri, kutumia ardhi iliyopo waweze kuona wananufaika na ardhi hiyo na inawezekana tukitumia Halmashauri zetu za Wilaya tukaanzisha Idara za Vijana kuna changamoto kubwa sana ya vijana kukosa ajira nchi hii, tukaanzisha hata Idara au Vitengo vya Vijana ikaona namna gani Halmashauri za Vijiji, Halmashauri za Wilaya, Manispaa inakaa na hiyo Idara, inakaa na vijana katika maeneo hayo kuwashirikisha, kuwaona vijana ambao wako tayari kupata na kuitumia ardhi kwa kuwaingizia kipato waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kumalizia nitoe rai kwa Watanzania pamoja na manyanyaso yote mliyopata ya matatizo ya ardhi katika miaka 53 ya Uhuru sasa ni wakati muafaka wa kwenda kuyakataa matatizo haya kwa kufanya maamuzi kupitia kura ikifika Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hiyo ime-*sound* kama lugha ya uchochezi hivi. Haya tulisema tujadili hotuba yetu. Nilimuita Mheshimiwa Mendrad Kigola atafuatiwa na Mheshimiwa Said Arfi.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi naungana na Wabunge wenzangu kwamba naipongeza sana hii Kamati Teule ambayo ilikuwa inashughulikia suala sugu la ardhi.

Tunajua kabisa kwamba ardhi ni msingi wa maendeleo kwa kila mtu, bila ardhi hatuwezi kuendelea. Tumeona mataifa mengi sana wengine wanapigana vita kwa ajili ya ardhi, wanagombania mipaka ili waweze kupata ardhi, lakini cha ajabu ambacho nakiona sisi Watanzania nchi nyingine zinapigana kugombania mpaka na mpaka, lakini sisi tunapigana ndani wenyewe kwa wenyewe wafugaji na wakulima ambayo hii naona tabia siyo nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lazima tukubali tukubali tukianza na mwaka 1961 idadi ya watu ilikuwa ndogo sana, Watanzania ilikuwa takribani watu milioni tisa na sasa hivi tumeshafikia watu milioni 48. Kwa hiyo watu wanaongezeka ardhi haiongezeki iko pale pale kwa hiyo lazima tukubaliane kabisa kwamba watu wanapoongezeka na mahitaji yanaongezeka na ukitaka kuangalia hata wafugaji sasa hivi kuna ongezeko kubwa sana la wafugaji na wafugaji sasa hivi katika Afrika Mashariki nadhani Tanzania ni wa kwanza kwa mifugo, tuna mifugo inafikia karibu milioni 22 na ukienda katika Afrika tunashika naasi ya pili nadhani nafasi ya kwanza inachukuliwa na Ethiopia kama sikosei.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima tuangalie kwamba kuna ongezeko kubwa sana la wafugaji. Kwa hiyo, mambo yote yameenda sambamba kuna ongezeko la wafugaji, kuna ongezeko la wakulima, sasa nini tufanye?

Napenda kuishauri Serikali lazima tuwe na mipango sahihi ya matumizi ya ardhi hapo ndiyo tatizo kubwa, kama hatutafanya mipango sahihi ya matumizi ya ardhi watu watakuwa wanagombana kila siku. Sasa hivi lazima tuhakikishe kwamba wafugaji wanakaa sehemu yao, wakulima wanakaa sehemu yao hii masuala ya kuingiliana ingiliana hii inatokea wapi?

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali kwanza nashangaa naona kama inachukua muda mrefu sana kwenye mpango sahihi wa matumizi ya ardhi. Nataka nimshauri Waziri wa Ardhi tunapoingia kwenye bajeti hii

inayokuja lazima tuhakikishe Wizara hii inapewa fungu kubwa, bajeti yake inakuwa kubwa ili iweze kufanya kazi vizuri, la sivyo sisi tutakuwa tuna vita kati ya wafugaji na wakulima na itaendelea.

Mheshimiwa Spika, nimeona niongee hilo kwa sababu sasa hivi inatokea mgongano mkubwa sana na hii ya kuhamisha wafugaji kupeleka kwa wakulima nalo ni kosa. Mfugaji huwezi ukapeleka kwenye sehemu ya wanaolima. Mfugaji mmoja anafuga ng'ombe 6,000 mpaka 10,000 kwa mtu mmoja, sasa mkulima akilima mazao yake mifugo ile inaenda kushambulia mashamba. Kwa hiyo hata mkulima hatakubali na yeye mkulima maisha yake yanategemea shamba kwa hiyo lazima tuweke *balance*.

Mheshimiwa Spika, halafu vilevile kwa ufugaji wa kitanzania mifugo inaongezeka kila siku lazima tuwe na ufugaji bora, mtu mmoja hawezi kuwa na ng'ombe 10,000 huo siyo ufugaji bora lazima tuwe na *minimum* ya mifugo, lazima hii shule lazima ipite, lazima elimu ipite kwa wafugaji kwa sababu mtu mmoja hawezi akamiliki karibu hekari 10,000 peke yake ya malisho haiwezekani na bahati nzuri wengine wamesema kwamba bajeti kubwa itaenda labda kujenga malambo.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niwashauri hata wafugaji lambo siyo lazima ujengewe na Serikali, unaweza ukauza mifugo ukajenga lambo wewe mwenyewe hii inaweza ikawa imesaidia.

Suala lingine ambalo nataka nisisitize kwenye Wizara ya Ardhi. Kuna migogoro kati ya kijiji na kijiji, kuna migogoro kati ya Wilaya na Wilaya, kuna migogoro ambayo inajitokeza kati ya ndugu na ndugu, lakini migogoro hii haiishi, kwa nini haiishi?

Mheshimiwa Spika, lazima tuangalie Sheria za Ardhi vizuri, unaweza ukaona kwamba kijiji na kijiji kinagombana lakini hakuna suluhu. Nataka nitoe mfano kwa mfano Kijiji cha Nyigo wanagombana na kijiji jirani cha Makambako,

lakini suluhu bado, sisi kwa sisi tunagombana kwenye mipaka hili linakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri aagize watendaji wake kwamba wahakikishe migogoro ya ndani haipo, wengine wanauwana ndugu na ndugu wanagombania mashamba, ndugu na ndugu, wengine wanauwana baba mmoja na mama mmoja wanauwana eti kwa ajili ya ardhi. Naomba sheria ichukue mkondo wake na tuhakikishe kwamba Wizara ya Ardhi inafanya kazi vizuri kutatua migogoro ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine nakuja kwa wawekezaji. Wawekezaji duniani kote wapo, hata Marekani kuna wawekezaji na sisi wawekezaji tunawapenda, hakuna nchi yoyote duniani inayowachukia wawekezaji hata siku moja, lakini lazima kuwe kuna utaratibu. Mwekezaji akiwekeza hawezi kusema ardhi yak wake, mwekezaji anakodisha ardhi ya Watanzania. Sasa sisi tunahamisha wananchi tunasema tunampa mwekezaji wakati kuna mapori makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini mwekezaji tunampa kwenye maeneo wanayoishi watu wakati kuna mapori makubwa yamekaa tu? Tunaomba sheria iangalie mwekezaji tunamuita lakini tumpe kwenye mapori awekeze, asiwekeze kwenye makazi ya watu. Sasa hii sheria naona bado kuna Sheria ya Vijijini ya mwaka 1999.

Mheshimiwa Spika, halafu ushirikishwaji kwa wanavijiji bado huwezi ukapeleka mwekezaji mwananchi hajui anatoka wapi, hatua wa kwanza lazima mwekezaji ashirikishwe na wananchi, wananchi kwa mfano hii Katiba Mpya ambayo tunaenda kuijadili kuipitisha kesho, wananchi wataipigia kura, imeelezwa vizuri sana kwamba mwananchi anapewa kipaumbele cha kumiliki ardhi, huwezi ukasema mwekezaji anamiliki ardhi miaka 99 ilitoka wapi na maisha ya binadamu tunasema ni miaka 70 sasa miaka 99 inatoka wapi hiyo?

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba Sheria ya Ardhi ya Vijiji lazima iheshimiwe na wananchi lazima washirikishwe vizuri na tunapopeleka mwekezaji wananchi wenyewe lazima wampokee, lazima tuitishe mkutano mkuu wa kijiji, wananchi wakubali na lazima tueleze mipango sahihi ya matumizi ya mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho naishukuru Serikali kwa upimaji wa ardhi kwenye vijiji lakini imetoa hati miliki tunasema hati miliki ile waliyopewa wananchi hawawezi kukopea benki. Sasa ile hati miliki bado haina faida kwa mkulima, ile hati miliki lazima mwananchi aweze kukopea benki kwa sababu mwananchi kumiliki ardhi maana yake impe manufaa sasa tumempa hati miliki, anamiliki ardhi lakini akienda benki anataka apate mtaji hawezi kupewa. Naomba sheria hii tuiangalie mwananchi aweze kukopea ardhi ili aweze kupewa fedha.

Mheshimiwa Spika, halafu suala lingine kwa vijana, vijana hawana ardhi sasa hivi watu wamekumbatia maeneo makubwa mtu mmoja unaweza ukaona ana eneo Arusha, ana eneo Dar es Salaam, ana eneo Iringa mtu mmoja ana maeneo makubwa sana vijana wetu hawana maeneo. Lazima Serikali ihakikishe kwamba vijana wanapewa maeneo, watu wamekalia maeneo makubwa sana, lakini vijana hawana maeneo tunasema vijana wapewe mitaji, hata juzi nilimuuliza swali hapa Waziri kwamba vijana hawana mitaji, tunasema tunawatafutia mitaji watafanyia nini kama hawana ardhi?

Mheshimiwa Spika, tunahamasisha kilimo kwanza, tunasema lazima watalima wapi kama vijana hawana ardhi. Vijana sasa hivi wanaanza kusaka maeneo wananunua, yaani kijana anaanza kununua kuna sehemu nyingine hapa nimesikia kwamba kuna mwekezaji mmoja anakodisha yaani mwekezaji anakodisha kwenye ardhi ya kwetu, hii mimi nashangaa sana hii, inatoka wapi mtu anakodisha ardhi?

Mheshimiwa Spika, yaani vijana wetu sisi wanaanza kukodi ardhi kwa mwekezaji hii haiwezi kutokea kabisa

kwanza kule kwangu haiwezi kutokea sijui inatokea wapi huko. Mwekezaji hawezi kwanza hata *terms* zile ukiangalia hawezi kukodisha ardhi kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kuamua na kuanzisha hii Tume ya Bunge kwa ajili ya kuzungumzia migogoro ya ardhi. Aidha, nitoe shukrani za kipekee kwa Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwa kazi nzuri waliyofanya.

Naomba nianze kwa kunukuu ukurasa wa 33 wa taarifa ya Mheshimiwa Ole-Sendeka aliyoiwasilisha jana, anasema kukosekana kwa mkakati mahususi wa Serikali. Kamati ilibaini kuwa Serikali haina mkakati mahususi uliyotarishwa, uliosambazwa na unaotumika kitaifa kwa ajili ya kutatua migogoro ya ardhi, hilo moja.

Lakini pia ukurasa wa 19 katika taarifa hiyo hiyo inasema uchambuzi wa sera umeonyesha kuwa kuna kutofautiana baina Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1997 na Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 katika suala la ufugaji wa kuhama hama, wakati Sera ya Ardhi ya 1997 inashawishi msisitizo katika kuzuia ufugaji wa kuhamama, Sera ya Mifugo ya 2006 inahimiza ufugaji wa kuhama hama, hii ndiyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hali ndiyo hivi kwamba hakuna mkakati wa kuondoa tatizo hili ndani ya Serikali ukiisoma hii taarifa huko mbele maana yake ni ndefu sikutaka kuinukuu yote inaeleza wazi kabisa baadhi ya viongozi wenye nyadhifa ndani ya Serikali hawajauona huo mkakati, hawajausoma wala hawajui, pengine miongoni mwao ni Mawaziri. Sasa kama Serikali haina mkakati, hili tatizo litaendelea kuwepo. Bunge hili ni lazima tufikie kuishauri Serikali tufikie mwisho sasa tuweze kumaliza tatizo hili linalowakumba wafugaji na wakulima katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, wenzangu wengi wametangulia kusema, lakini nataka nitolee mfano tu ambao ni mwepesi na ninaweza kuulezea vizuri unaohusu Wilaya ya Mpanda. Wilaya ya Mpanda au Mkoa wa Katavi, una jumla ya eneo la kilomita za mraba 45,000 na zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1967 wakati wa sensa Wilaya hii ya Mpanda ilikuwa na watu 51,000; ardhi tuliyokuwa nayo nzuri kwa matumizi ya kilimo ni asilimia 19 ya eneo lote, leo tuna watu 600,000 na zaidi. Ongezeko la watu limekuwa kubwa lakini ardhi haiongezeki imebakia vilevile, lakini eneo kubwa limekamatwa na hifadhi za wanyamapori na misitu.

Sasa kuna mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati nadhani ni muhimu Serikali ikayafanyia kazi mapendekezo yaliyobainishwa na Kamati ya Mheshimiwa Ole-Sendeka juu ya zile hifadhi ambazo zimepoteza hadhi sasa wapewe wananchi na katika hilo tutakuwa tumeondoa mgogoro katika Kata ya Itenka na Kata ya Kakese kule Mpanda. Kata ya Kakese ipo umbali wa zaidi ya kilomita 40 kutoka Hifadhi ya Taifa ya Katavi, lakini watu kwa ujanja tu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mstaafu na kwa sababu mke wake ni Afisa wa Maliasili pale wakaanzisha *WMA,* watu wa mjini bila kuwashirikisha watu wa vijijini wakatengeneza muhtasari, wamehodhi ardhi ya watu wanawazuia watu kulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *WMA* hii imekuja mpaka Kijiji cha Mwamkulu, kijiji hiki kinatambuliwa, kimesajiliwa, kina mradi mkubwa wa umwagiliaji ambao umechukua fedha nyingi za Serikali, matokeo yake Serikali imeweka fedha kwa ajili ya kuzalisha chakula, leo wanaondolewa wananchi kwa sababu ya kupisha *WMA*. Matatizo haya ambayo tunayo sasa hivi ni lazima yapate ufumbuzi, pamoja na Kamati imetoa mapendekezo kadhaa, nilikuwa nataka kuishauri Serikali kwamba mgogoro uliopo kati ya Jata ya Itenka na Kakese upate ufumbuzi kabla ya Oktoba, 2015 kwa sababu vijiji hivi vimekuwepo, vimesajiliwa watu tu kwa ubabe ubabe wanaamua kufuta usajili, wanatengeneza mipango yao ya ulaji, halafu kesho baada ya kuwa wameshafanya uchaguzi

wanakuja wanachomewa nyumba zao, jambo hili halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, ifikapo Oktoba muwe mmeshaamua kwamba vijiji hivi ni vijiji halali, wananchi hao wataendelea kuwepo, wataendeleza shughuli zao za kilimo au mnawaondoa ili wawe na maamuzi msiwabembeleze sasa mkaa kimya, mkafumbua macho mgogoro huu wa Kabage na Itenka kwa sababu tu mbele kesho kuna uchaguzi, tunataka tupate majibu kabla ya Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011 mimi nilileta hoja binafsi kuhusu migogoro ya ardhi. Kwa bahati mbaya sana hoja ile ikashindwa kufikishwa Bungeni kwa sababu za kiufundi, lakini pamoja na kushindwa kufikishwa ndani ya Bunge lako Tukufu nilichukua hatua za ziada kulikuwa na mkakati wa kugawa yaliyokuwa makazi ya Katumba na Mishamo kwa kampuni iliyokuwa inaitwa *AgriSol,* zaidi ya hekta za mraba kilomita 4000 ya makazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja yangu kushindwa kwa sababu za kiufundi kufika mbele ya Bunge hili nililazimika kutumia nguvu za ziada za kwenda kuwashawishi. Kwa hiyo, niwaombe viongozi wenzangu, pale tunaposhindwa kuishawishi Serikali kupitia ndani ya Bunge tuwatumie wananchi wenyewe wafanye maamuzi juu ya ardhi zao. Kwa sababu waathirika wakubwa ni wananchi na tulifanikiwa kuzuia mpango huo usiendelee katika makazi ya Mishamo na Katumba. *(Makofi)*

Lakini nini faida yake leo, faida yake leo tayari Serikali hii isiyokuwa na mitazamo imewapa uraia wakimbizi waliokuwa wanaishi katika maeneo hayo na wameshindwa kuwahamisha, mngewapeleka wapi kama hiyo ardhi mngekuwa mmewapa *AgriSol* mwaka 2011?

Kwa hiyo, jitihada za kuzuia kumilikisha ardhi zile za makazi ya Mishamo na Katumba kwenda kwenye kampuni binafsi imewastiri ninyi leo wale wakimbizi bado wanaendelea kukaa katika yale maeneo. Serikali iwe na mipango endelevu,

mtizame maslahi mapana ya wananchi maskini, ardhi imekuwa ikigawanywa kiholela. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba naungana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati na kubwa zaidi ni kufuta maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa. Maeneo mengi ya hifadhi yamepoteza sifa, wananchi wameweka makazi yao, wanaendeleza maisha yao katika maeneo hayo leo hamtakuwa mmewatendea haki wala ubinadamu kuwaondoa katika maeneo hayo kkwa mfano pale Kangeme au kule Mapili Inyonga ambao hawana ardhi, kabisa Masigo na maeneo hayo yote yamezungukwa na hifadhi ama mrekebishe mipaka iweze kutoa fursa kwa wananchi waweze kupata maeneo ya kuendeleza maisha yao.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la maeneo ambayo Serikali ya Vijiji imetoea kinyume cha sheria na kama tunazo sheria na Serikali ndiyo inayosimamia hizo sheria, sheria zinavunjwa mnachukua hatua gani, hawa wote waliopewa zaidi ya eka 50 na Serikali ya za Vijiji ni kinyume cha sheria. Serikali ina mpango gani wa kuchukua hatua katika kurekebisha dosari hii ambayo Serikali za Vijiji imetoa ardhi zaidi ya eka 50 na wakati mwingine kwa ushahidi kabisa mikutano ya kijiji ilikuwa haitimizi idadi inayohitajika kwa mujibu wa sheria ili kuweza kugawa ardhi. Ardhi zote hizi zimetolewa kwa ubatilifu, Serikali sasa hivi ni lazima ijipange.

Suala la mwisho kabisa niishauri tu Serikali kwamba ardhi yetu inataka kupimwa na tuwepo na mpango mahususi wa kuendeleza yaani wa matumizi bora wa ardhi, vinginevyo tusipokuwa na mpango wa matumizi bora ya kutumia ardhi migogoro hii itaendelea kuwepo siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba maeneo mengi katika nchi yetu yanaonekana kwamba ni mapori lakini lakini hatuna uhakika ni kiasi gani cha ardhi yenye rutuba ambayo tunaweza….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Maana ulikuwa unaokoteza wee mpaka…, nilisema Mheshimiwa Ester Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Napenda kuipongeza Kamati Teule ya Bunge kwa kazi nzuri iliyofanya na nina imani kwamba labda kulikuwa na *constrain* ya muda na fedha ndiyo maana hawakufika mkoa wa Mara, licha ya kwamba mkoa wa Mara una matatizo na migogoro mingi ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukizungumzia migogoro ya ardhi kwa muda mrefu, binafsi tangu nimeingia katika Bunge na kuna migogoro ya ardhi kati ya mwekezaji na mwananchi, *I mean* kati ya wananchi na hifadhi, lakini pia kati ya wananchi na ardhi imechukuliwa na Serikali kwa shughuli mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kimojawapo ambacho kinapelekea haya yote kumekuwepo na ucheleweshaji wa utatuzi wa migogoro. Kwa mfano kuna mgogoro mkubwa sana ambao unaendelea kwenye Hifadhi ya Akiba ya Ikorongo au *Grumeti* huko Serengeti ambapo inaonekana kabisa Kijiji cha Pakinyigoti kilichopo Serengeti kuna *GN* ilitoka ya 214 ya mwaka 1994 iliainisha mipaka ilivyo, lakini walivyoenda wahifadhi kuweka *beacon* zao ilikuwa ni tofauti. Kitu ambacho kikapelekea baadhi ya ardhi ya wananchi ikachukuliwa kwenda kwenye hifadhi na hii yote inatokana na kwamba wananchi hawashirikishwi, kitu ambacho ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwamba iliweza kukaa mamlaka husika Ofisi ya Wilaya, Kata na wananchi mwaka 2008 lakini mpaka sasa hivi wakakubaliana kwamba ile ardhi itaweza kurudi, lakini mpaka sasa hivi haijaweza

kurudishwa. Na madhara ambayo tunayapata tumekuwa tukishuhudia wananchi hawa maana yake katika hilo eneo ambalo limechukuliwa kuna sehemu ambayo kuna maji ambayo mifugo inaenda kunyeshwa mle, lakini pia kuna wakulima wanategemea yale maji. Kinachotokea wakienda kunywesha mifugo yao kwenye hayo maeneo aidha wanapigwa risasi wale wafugaji au ng'ombe zao zinakamatwa. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kushughulikia hiyo kero, wananchi wa Kijiji cha Pakinyigoti wapate haki zao na mtatue huo mgogoro umekaa kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini tangu nimekuwa Mbunge nikazungumzia suala la Wanajeshi kuchukua ardhi ya Lonsoti katika Kata ya Nyamisangula Wilaya ya Tarime na pia kuna ardhi ya Kinyabi Kata ya Nkendi, Waziri Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kipindi hicho alikuwa Waziri wa Ulinzi akaahidi atatua akapelekwa Wizara ya Afya, akarudi tena Ulinzi, lakini mpaka leo hii kuanzia mwaka 2007 wale wananchi hawajaweza kufidiwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwenye bajeti yake aliahidi kwamba wanaenda kufidiwa, wakatuma Halmashauri ikaenda, lakini mpaka leo hawajalipwa, wananchi wale wamezuiliwa wasifanye shughuli zozote za maendeleo, wasijenge nyumba zimeanguka, wasilime, sasa jamani Serikali ya Chama cha Mapinduzi hawa wananchi mnawatakia mema? Mambo ambayo ni rahisi kabisa. Tumetenga bajeti hapa mwaka jana Mheshimiwa Mwinyi na Waziri wa Ardhi, Mama Tibaijuka akaahidi kwamba ataenda mpaka Tarime kuhakikisha ameshughulikia hili tatizo la Lonsoti katika Kata ya Nyamisangula na Kinyabi Kata ya Ntende mpaka leo wananchi wale hawafanyi shughuli zozote zile mnavyojua Wanajeshi walivyo wakichelewa hata saa kupita mtaani wanawapiga, mnawatakia nini wale wananchi? Hawajishughulishi, nyumba zimeanguka kujenga hata choo hawawezi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiongea kwamba kuna uzembe na kama vile ambavyo Kamati Teule imeainisha kuwa kuna uzembe, kuna Tume iliundwa mwaka

1991, maazimio yao hayajatekelezwa mpaka leo, tunaunda Tume nyingi na maazimio tunatoa, lakini Serikali inafumba macho wananchi wanaendelea kuteseka, wananchi wanauwana, uchumi unarudi nyuma, tufanye nini? Tunakaa leo kama hapa tunatoa maazimio mwisho wa siku hayaendi kutekelezwa, wananchi wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, nilizungumzia pia kwa mapana sana kuna vijana walishawahi kuuwawa wa Gibaso, Kigunga, Masanga na hata Kamati yako ya Ardhi, Mazingira ilizungumzia hili. Kuna mgogoro mkubwa sana la Pori la Akiba la Nyanungwa ambayo Serikali mmeichukua bila kuwashirikisha wale wananchi na hata hamjaweza kuwahamisha na kuwaelimisha, badala yake mnakamata vijana wakienda kulisha mifugo mle, wanauwawa, wananchi wale bado wako kule wakati wa Operesheni Tokomeza tulijua adha zilizotokea mle walikuwa wanapigwa, wengine nyumba zinachomwa, wengine wanauwawa, mifugo inauliwa na mkaahidi hapa kwamba mifugo yote ambayo imeuliwa wakati wa Operesheni Tokomeza mngeweza kufidia, lakini mpaka leo hawajafidiwa mifugo na bado wanaendelea kukamatwa na kupigwa.

Kwa hiyo, naomba sana Kamati zimeiainisha, ripoti zimeainisha Kigunga, Masanga na Gibaso kule Nanyungu napo pia Serikali jamani fuatilieni mgogoro uliopo, Waziri wa Ardhi mkishirikiana na Waziri wa Maliasili na Utalii tatueni ule mgogoro uliopo wananchi warudishiwe ardhi yao kama ni hifadhi imeamua kuchukua muwa-*compensate* wananchi waweze ku-*re-allocate* waende sehemu zingine, msiendelee kuwatesa bila kutoa mbadala wake kama vile sheria ambavyo zinaainisha.

Mheshimiwa Spika, kingine ni mgogoro uliopo kati ya Kata ya Mwema Kijiji cha Korotambe, Wilayani Tarime, tunatambua kwamba kulikuwa mgogoro wa muda mrefu kati ya kata ya Mwema na Nyamalaga na Serikali mkaamua kwamba JKT wachukue ile ardhi. JKT wamechukua ile ardhi lakini hamjaweza kuwa-*compensate* wale wananchi, sasa tunajiuliza wananchi ambao wanakuwa wanaishi kwa muda

wote, mkienda mkachukua ile ardhi na bila kuwahamisha na kuwalipa fidia wanaenda wapi? Maana yake pale JKT wamechukua ile ardhi lakini hakuna mchakato wowote mpaka sasa hivi umefanyika, ni takribani miaka miwili, hao wananchi mnawapeleka wapi na wameishi pale kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ingawa umesema kwamba tunakuwa tunalalamika sana lakini tumekuwa tukishauri Serikali ya Chama cha Mapinduzi haisikii. Wananchi huko nje mtusikie mtuelewe, siyo kama tunapiga kampeni hapa tunaeleza. Mnavyokuwa mnakaa mtafakari Mungu anawapa tena mwaka huu wa uchaguzi chagueni viongozi wenye dhamira ya kuwasaidia.

**SPIKA:** Naomba ujadili hoja, nimekupa nafasi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, tunachoka tunaongea, tunaongea hamna utekelezaji, na sasa hivi ni wakati wa uchaguzi mwaka huu…

**SPIKA:** Endelea kujadili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Wananchi lazima tuwaelimishe.

**SPIKA:** Unawaelimisha huo ni uchochezi unaitwa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, natambua wewe ni mwanamke, na migogoro inavyopatikana na vita vikitokea….

**SPIKA:** Mimi ni Spika bwana, habari ya kuni-*describe* naomba msini-*describe,* mimi ni Spika nimekaa sina shughuli nyingine zaidi, kesho mtamuita mama watoto, hapana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, adha zote tunazozipata ni katika dunia yote ni nchi ya Tanzania tu ambako utaona watu wako wanauwawa, tunaona wakulima wanavyouwana na wafugaji lakini hamna Serikali

inawajibika, ni Tanzania peke yake duniani na nafikiri mtaingia *book of guiness* watu wenu wanauwawa lakini hamchukui hatua.

Mheshimiwa Spika, yaani leo wafugaji wanauwana na wakulima kwa sababu ya ardhi, lakini unakuta Mawaziri mnakula tu *AC* kwenye maofisi yenu. Leo tukisema wananchi wachukue hatua mnakataa, wananchi uchaguzi ni mwaka huu….

**MWONGOZO**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, dakika zangu zilindwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Namba 64(f) na (g) mjadala huu ni muhimu sana na mjadala huu unachukua sura ya Kibunge kwa maana ya Taifa kuishauri Serikali katika mambo muhimu sana ambayo amekuwa yakiendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mjadala huu katika ajenda hii hauna maudhui ya shughuli zozote zinazoendana na harakati za kisiasa. Mjadala huu hauna maudhui ya maneno ya kejeli ambayo wala hayana uzito wa jambo ambalo linajadiliwa hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, maneno ya kuudhi, mimi naomba mwongozo wako hivi aina hii ya mjadala tunaoendelea nao unahusiana kweli na ajenda tuliyonayo ndani ya Bunge kwa kutumia maneno hayo yenye kuudhi ambayo hayamo katika hoja tuliyonayo hapa ndani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, toka jana nimesema hili suala ni kubwa na muhimu. Nilipenda sana tulijadili kusudi tupate kitu angalau kizuri, ndiyo hicho tu nilitaka.

Kwa hiyo, sasa namuita Mheshimiwa Opulukwa atafuatiwa na Mheshimiwa…

**MBUNGE FULANI:** Hajamaliza.

**SPIKA:** Amemaliza, atafutiwa na Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Sijamaliza Mheshimiwa.

**SPIKA:** Si ulisema umemaliza?

**WABUNGE FULANI:** Hajamaliza.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Nikiwa naendesha kikao sipendi mnisaidie kuendesha sijawaomba.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri kwanza amaalizie Mheshimiwa Esther, mimi nilifikiri alikaa amemaliza, endelea.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Napenda kusema na siyo kwamba tunakuwa tunaongelea siasa…

**SPIKA:** Naomba uendelee umalize, hiyo siyo sehemu ya taarifa hii.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, namalizia, ni kwamba ukiangalia takwimu za wananchi waliouwawa kwa migogoro ya ardhi, leo hii nikiomba Serikali ilete takwimu za wananchi waliouwawa kwa migogoro ya ardhi hakuna takwimu. Kwa hiyo, tukiongea haya mambo tunaongea kwa masikitiko makubwa na ripoti imeainisha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, mapendekezo ya ripoti ya Kamati yako Teule yote ni mazuri, tunaomba kabisa maazimio ya Bunge yanavyoenda kupitishwa Serikali kwa sasa hivi mchukulie hii kitu ni *serious* muifanyie kazi. Tumechoka kupoteza Watanzania kwa migogoro ya ardhi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Meshack Opulukwa atafuatiwa na Dokta Pudenciana Kikwembe.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nami basi niungane na wachangiaji wengine waliopita kwa ajili ya kupongeza taarifa hii ambayo imekuja mbele yetu na ambayo tunaijadili hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, nitajaribu kwenda kifupi sana *and precise* ili angalau haya ninayosema yaweze kuwa *captured* kwenye taarifa hii na ikiwezekana yajumlishwe kwenye hii taarifa na Mwenyekiti wa Kamati na iwe ni sehemu ya maazimio.

Mheshimiwa Spika, ukurasa ule wa 46, napenda kuongezea kipengele cha (d) kinachosema:-

*"Kuruhusu maeneo yote ya WMA pamoja na mapori tengefu ili yaweze kuwa ni sehemu ya malisho ya mifugo kama ilivyo kwenye Ngorongoro Conservation"*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshauri Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba hii ni muhimu sana kwa sababu tuna maeneo mengi sana nchini ambayo yameshapoteza sifa. Ukiacha sifa kama ambavyo wewe mwenyewe umeweza kusema katika taarifa yako au katika taarifa yenu ya Kamati, ukiangalia maeneo kama kule Arusha, Ngorongoro *Conservation*, mifugo pamoja na binadamu wanashiriki katika kuishi kwenye hilo eneo lakini maeneo mengine imekuwa ni ngumu sana. Zamani sana Wasumuka pamoja na wafugaji wengine walikuwa wanakula sana wanyamapori lakini siku hizi wameacha kabisa. Sanasana wanakula ng'ombe pamoja na mifugo mingine ambayo wanaifuga. Kwa hiyo, mimi nadhani na nashauri kwamba, kwenye haya maeneo ambayo ni mapori tengefu pamoja na *WMAs* ikiwemo na ile *WMA* ya Makao na Maswa *Game Reserve* wafugaji waruhusiwe kuingiza mifugo mule ndani kuchunga ile mifugo yao ili mradi tu wasivunje sheria na taratibu za mapori hayo pamoja na hayo maeneo tengefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika taarifa hii kuna maeneo ambayo nadhani Kamati yawezekana labda kwa sababu ya muda haikuweza kuyafanyia kazi ikiwa ni pamoja na wale watu ambao walifika mbele ya Kamati na kuweza kutoa michango yao. Mimi ni mmojawapo wa watu ambao waliitwa na Kamati na nikatoa mchango wangu na naamini ulikuwa ni mchango wenye manufaa na wenye afya. Kulikuwa na maeneo ambayo yalikuwa ni ya muhimu sana kama kule Meatu, eneo la Sakasaka ambapo kuna Diwani aliyeambiwa apige simu kwa kutumia kiatu chake ili kuweza kuwaambia watu wengine hali halisi ya Operesheni Tokomeza inavyoendelea kule, ilikuwa ni hali ambayo siyo nzuri sana na alipigwa sana na akaumia sana lakini sikuiona katika taarifa hii kwamba imeingizwa. Mheshimiwa Diwani wa Sakasaka alipata kichapo cha kutosha kabisa na alitoa maelezo ambayo ni mazuri sana kwa Kamati lakini

haikuweza kuingizwa humu. Katika Mikoa iliyotembelewa, Mkoa wa Simiyu pamoja na Wilaya ya Meatu yote haimo. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii ulipitiwa basi ujaribu kuchukua na yale mambo muhimu ambayo hukuweza kuya-*capture* yaweze kuingia kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini wasio wafugaji wanachukia sana mifugo? Hivi kwa nini watu ambao hawana ng'ombe wanachukia sana ng'ombe? Cha kushangaza, leo hii kwa hawa wachukia ng'ombe hawa ukienda kwenye friji zao zimejaa nyama ya ng'ombe. Hawa wanaochukia ng'ombe ukienda kwenye Dhifa mbalimbali za Kitaifa, nyama ya ng'ombe iko pale. Leo hii wafugaji wamekuwa ni kama vile ni watu ambao wamelaaniwa katika nchi ambayo ni ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri tusiwafanye wafugaji waweze kuichukia nchi yao ya Tanzania. Tumekwenda kutembelea Ethiopia tumekuta kuna wafugaji wanaishi vizuri sana pamoja na wakulima na Serikali imewatengenezea miundombinu ya kutosha kuweza kufanya migogoro ile isiweze kuwepo. Wafugaji wa Tanzania imekuwa kama vile ni watu ambao wameshalaaniwa kabisa, unakuta hakuna hata msaada tunaowapatia wa kutosha. Leo hii hata Wabunge wengine wanapochangia humu ndani wanalaani mifugo, wanasema kwa nini mifugo iende sehemu nyingine, hii mifugo jamani ni neema siyo laana. Tunapokuwa na mifugo katika nchi kwanza *is a symbol of wealth* kwamba Watanzania tuna mifugo ya kutosha na tutumie mifugo hii, tutafute hata uwezekano wa kupata viwanda vya kuweza kusindika nyama ya mifugo hii ambayo watu wanaona kwamba ni laana. Taifa litaondoka kutoka hapa tulipo litaweza kwenda mbele zaidi ya hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo haya kama vile ya wawekezaji pamoja na wananchi. Naomba nitoe mfano ambao ni mfano halisi. Ukichukua Wilaya ya Meatu kuna mwekezaji mmoja anaitwa *Mwiba Holdings* ambaye ndiye

anayemiliki ile *WMA* inaitwa *WMA* ya Makao. Wananchi wamefikia mahali wakasema sasa *WMA* hii hawaitaki tena. Kwanza ni *WMA* ambayo imeanzishwa kinyemela, haikufuata hata utaratibu lakini la pili wananchi hawa wanauwawa kila siku.

Tangu nimeanza Ubunge kuna zaidi ya wananchi kumi ambao wameuwawa na Askari wa Wanyamapori ambao wanaitwa ni *Game Reserve* wa Kampuni ya Mwiba lakini hakuna ambacho Serikali inaweza kuwasaidia watu hawa waweze kupata haki yao.

Mheshimiwa Spika, kuna mwananchi mmoja ameuwawa juzi kwenye kijiji cha Lukare. Mwananchi huyu baada ya kuuwawa na taarifa ya *postmortem* iliyopatikana pale hospitali inaonyesha kwamba huyu mwananchi ameuwawa wakati alikuwa anawakimbia Maaskari wa *game* wasiweze kumdhuru. Kwa hiyo, alikuwa anakimbia na hii ni taarifa ya *postmortem* lakini badala ya yule muuwaji kuweza kukamatwa na kushughulikia inavyotakiwa kisheria kwa kusikitisha sana *OC-CID* wa Meatu alikwenda akabadilisha kabisa yale mazingira ya jinsi yule mtu aliyouawa ikaonekana kwamba eti alikuwa anakwenda kumshambulia Askari aliyekuwa na silaha.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake badala ya mtu huyu kuwa na *charge* inayostahili akapewa *lesser charge,* akaonekana kwamba eti ameuwa bila kukusudia wakati alifanya kwa makusudi. Nimekaa na Mwenyekiti wa Kijiji, nimekaa na Mtendaji wa Kijiji cha Lukare ambapo huyu marehemu ndiye alikuwa anatoka, ikaonekana kweli mtu huyu aliuwawa kwa makusudi na hawa watu mpaka sasa hivi wako nje na wamefunguliwa *lesser charge* badala ya *charges* ya *murder* inayostahili mtu aweze kuipata. Hii ni kwa sababu tu Serikali yetu na hasa Maaskari wetu hawa ambao wanapenda kufanya kazi kwa mashinikizo au kwa kutumiwa na viongozi wa juu ndiyo wanafanya haya mambo yaweze kuonekana kwamba hayaendi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati iliyotuletea taarifa hii ambayo ni taarifa muhimu lakini basi tuweze kuingiza hiki kipengele ambacho ni muhimu sana, maeneo yote ambayo ni ya mapori tengefu pamoja na *WMA's* mifugo iruhusiwe kuingia mle ndani waweze kuchungia kama ilivyo kwenye Ngorongoro *Conservation* ili basi angalau na wao waweze kufaidi matunda ya kuwa na maeneo makubwa ya kuweza kuchungia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho. Kumekuwa na taarifa za upotoshaji kwenye Wizara kwa mfano katika Mkoa wa Shinyanga kwamba kuna maeneo ya kutosha kwa ajili ya kuchungia mifugo zaidi ya hekari 11,000 na kwamba hizi hekari 11,000 kati hizo hekari 8000 ziko Meatu. Hizi hekari 8,000 haziko Meatu na hekari 11,000 kwa Mkoa wa Simiyu hazipo. Sasa angalau basi Mheshimiwa Kamani muwe mna-*crosss check* pamoja na watendaji wenu ili kujua kama kuna taarifa wanazowapatia za uongo ili muweze kujua jinsi ya kuweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kunipatia nafasi hiii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dokta Prudenciana anafuatiwa na Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi.

**MHE. DKT. PRUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kupata nafasi hii kuchangia katika haya mambo mazuri ambayo Kamati imeweza kuyafanyia uchunguzi wa kina na hatimaye kubaini na kuja na mikakati ambayo inaweza kuisaidia Serikali kupanga mipango yake katika kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwashukuru wananchi wa Mkoa wa Katavi ambao Kamati iliwapitia. Walipopitiwa na Kamati hii kwanza walikuwa wanaogopa kutoa maoni wakanipigia simu, nikawaambia naomba

msiogope endeleeni kushirikiana na Kamati ili muweze kuangalia nini ambacho kinaweza kuendelea na walifanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda tu nianze kwanza kwa kuongelea pale tunapolaumu na kusema Serikali, Serikali, kana kwamba sisi Wabunge ama wananchi si sehemu ya Serikali. Nataka niseme, Serikali ni wananchi pamoja na watawala wake ambao ni wananchi wa Tanzania. Sasa tusifike hapa tukawaaminisha wananchi na tukawapotosha na Mheshimiwa Spika umewaasa wanafunzi waliokuja kwenye mafunzo hapa kwamba Wabunge wengi ni wasomi humu, nafikiri na dhana ya msomi ni kutumia elimu yako uliyoipata kuwaelimisha wananchi wako ili waweze kuondokana na hii migogoro na si kuja hapa Mbunge kulalamika. Fanya mikutano na wananchi, waelimishe wapate kuelewa, tunaongea nao wakulima na wafugaji. Sasa tumeanza kujenga dhana kwamba hawa ni wakulima na hawa ni wafugaji, kutengana, hapana wote ni Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Kuna Azimio la Mto Wisa ambalo liliainisha mambo mengi sana. Naomba Serikali ifuatilie haya mambo yaliyotolewa kwenye lile kusudio la Azimio la Mto Wisa. Tatizo ni nini? Tatizo linaonekana watu hatufuati sheria, hatuwajibiki, hatufanyi kazi zetu kwa namna ambavyo tumeajiriwa nazo. Kama ni Mwenyekiti wa Kijiji hatekelezi wajibu wake, kama ni Mbunge hatekelezi wajibu wake wa kuelimisha wananchi. Unaenda kufanya mikutano ya kuhamasisha wananchi wasifanye kazi, waelimishe wananchi namna ya kuingiza mifugo kutoka Kanda ya Ziwa Shinyanga, Mwanza kwenda Katavi waingize mifugo kwa utaratibu upi kwa kufuata sheria. Ndiyo tunachotakiwa kufanya! Tunaposema Serikali ikafundishe, ikamfundishe nani na sisi ni wasomi humu ndani? Wananchi sisi ndiyo wawakilishi wao, wametupa dhamana hii tukaongee nao, tuwaelimishe pamoja na nguvu ya Serikali inatakiwa, ndiyo lakini nasi tuna wajibu wa kuwaelimisha wananchi watii sheria, wajue sheria ili waondokane na hii migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala la ulipaji wa fidia. Ulipaji wa fidia umekuwa wa kusuasua, wananchi wanasikitika. Wananchi wangu wa Majimoto, wa Usevya, wa Kabage waliochomewa nyumba zao kwa ajili tu wameingia sehemu ya mipaka. Je, nauliza, wananchi hawa wanajua mipaka? Watu wa *TANAPA* kama watendaji, watu wa Wizara ya Maliasili ndiyo naongelea suala la uwajibikaji, je, wamefanya kazi zao? Wameweka mipaka inayoeleweka? Kama wote tutawajibika nchi hii itakwenda vizuri. Kwa hiyo, naomba wale watendaji wote ambao hawakuwajibika kwa namna moja ama nyingine, naongelea hususani Mkoa wangu wa Katavi kuanzia Idara ya Maliasili wawajibishwe kwa misingi ya sheria na Katiba ya nchi hii kwa sababu hawakutenda wajibu wao inavyotakiwa. *(Makofi)*

Narudi kwenye suala la utunzaji wa mazingira, yote ni yaleyale lazima sisi kama Wabunge tutoe elimu kwa wananchi wetu ni namna gani ya kuheshimu vyanzo vya maji, namna gani ya kuangalia hao watu wetu hawaingiliani kwenye matatizo. Tukianza kusema huyu mfugaji, huyu mkulima sasa tunaenda wapi? Mimi nimeolewa na mkulima, yule ameoa mfugaji sasa tunatengana tunaenda wapi? Lazima turudi tuwe na njia moja, tutumie *common sense* katika kuangalia mambo siyo lazima kwenda darasani.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa viongozi. Naongelea viongozi hasa wa Serikali za Mitaa, Wajumbe, tunawapa elimu gani? Tunaongelea masuala ya rushwa, ni kweli rushwa ipo. Hawa wananchi mimi nakuja na ng'ombe zangu nimeswaga kutoka Shinyanga nimeingizia kupitia Sikonge kule wametembea kwa miguu polepole ukiona gari limeandikwa *STK* naingia msituni, naangalia gari ikishapita na mimi natoa ng'ombe wangu nawapeleka. Hawa Watendaji Wenyeviti wa Vijiji wana elimu kiasi gani ya kuweza kusema tunafuata utaratibu wa sheria? Tukifuata sheria kila kitu kitanyooka na kitakwenda vizuri, hatutakuwa na migongano na Polisi kama wanasiasa, hatutakuwa na migongano ya mkulima na mfugaji. Tutakapokuwa na dhana ya kuheshimiana ndipo utakapoweza kutii sheria. Kwa hiyo, vitu vingine vinatoka ndani yako na si vya kujivalisha.

Mheshimiwa Spika, naomba nirejee masuala ya hifadhi hasa maeneo ya *TANAPA*, kaka yangu Arfi ameongelea vijiji vya Inyonga kule. Kule kuna maeneo tengefu ambayo yametengwa kupitia Halmashauri. Ni eneo la Mheshimiwa Waziri Mkuu siyo eneo la Mheshimiwa Arfi, Mheshimiwa Arfi anatoka katikati pale, anapambana pale na vijana wanaenda wanamtukana wanampiga, hivyo hivyo siku zinaenda.

Kule kuna maeneo tumetenga ambayo kuna wafugaji wanaotoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga wanakuja pale. La msingi hapa kwa sababu kuna engezeko la watu, kutokana na huduma bora za afya ambazo zimetengenezwa vizuri kupitia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tukapunguza idadi ya vifo, ndiyo maana watu wanaendelea kuongezeka na umri wa kuishi umeongezeka kutoka 47 *up to 67,* ni Serikali kupitia Wizara ya Maliasili iangalie mipaka yake upya. Kwa sababu tumeshauwa tembo wa kutosha, nyati hakuna, shuka bonde la Lyamba lya Mfipa pale, ulikuwa ukishuka hivi unakutana na makundi ya nyati, unasimama unayaangalia. Maana utalii siyo lazima ukakate kibali, hata ukisafiri kwa gari ukaangalia miti ni utalii, hakuna, wamepungua. Sasa waangalie namna ambavyo ile ardhi wakarejea mipaka yao upya kuondoa migogoro kati ya watu wa Maliasili na Wanavijiji hasa vijiji vyangu vya Usevya, Manga, Starike wameathirika sana kutokana na hii mipaka yao.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wajenge mazingira rafiki na wananchi wanaokaa kwenye hivyo vijiji husika. Nimejaribu kuongea sana na Mkurugenzi Kijazi, nimejaribu kuongea na watu wengi, kwamba jengeni mazingira rafiki muone namna gani, zamani watu walikuwa wanatunza wanyama bila tatizo, kwa nini leo? Tulikuwa hatuna tatizo kabisa sisi na wanyama! Mimi nimekulia nyama ya pori, nyama ya ng'ombe sili mpaka kesho, siijui ladha yake. Kwa nini leo? Sasa lazima tuangalie ni namna gani Serikali yetu kupitia Wizara ya Maliasili inarekebisha hii mipaka na ijenge mazingira rafiki. Ni sawasawa na lile la kuondoa vitalu, vitalu viondoke, watu wanaojifanya wanaweka vitalu ndiyo majangili wenyewe, wanakaribisha majangili watoke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wa Maliasili hawaainishi mipaka, wameenda kwenye Jimbo la Ndugu yangu Kakoso, kijiji cha Mnyamasi, Kaseganya, Kabogole, Kabage na Luhafo wamewachomea nyumba wananchi.

Naomba mamlaka husika kwa sababu nchi hii inaendeshwa kwa sheria na taratibu na kanuni wachukuliwe hatua za kinidhamu. Siyo kuhamishwa wala kufukuzwa, sheria zipo na Mahakama ndiyo inayotoa haki. Sasa tutumie utaratibu unaotakiwa kuendesha nchi na siyo kukaa hapa Serikali, Serikali, Serikali ni sisi wote, je, wewe umewajibika vipi kwa nafasi yako? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilimuita Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Buyogera.

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka tu niwaombe Wabunge waelewe kabisa kwamba mada iliyoletwa hapa imeletwa na Kamati ya Bunge na lengo lake ni kujaribu kutafuta ufumbuzi wa kuiondosha kabisa hii migogoro ya wakulima na wafugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini navyoangalia wengi wanavyoelekea kunakuwa na ubaguzi na chuki baina ya wafugaji. Kinachonishangaza, wabaguzi hawa wanaochukia ng'ombe, wamevaa viatu vya ngozi ya ng'ombe, wamevaa mikanda ya ngozi ya ng'ombe, wana mabegi ya ngozi ya ng'ombe lakini wana chuki dhidi ya ng'ombe, ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka niombe, tuyachukue mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yetu ambayo imetumia fedha nyingi kwa ajili ya kujaribu kutafuta ufumbuzi ili mfugaji na mkulima waishi vizuri. Kinachoonekana kuna watu wanadhani hawa wanaotembea na ng'ombe wao ni kama watu ambao ni vichaa. Lazima mjue kwamba, hao wametoka kwenye maeneo mbalimbali kwa sababu maeneo yao ama yamebadilishwa matumizi yakawa ni matumizi labda ya Jeshi, ama yakawa ya machimbo, hawa watu ni lazima watafute maeneo mengine ili waweze kukidhi maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini utashangaa, watu wanasema, waondolewe kwetu! Hivi hawa wanaokuja ni wa kutoka Msumbiji? Au hawa mnaowaona wametoka Shinyanga au Monduli, mnadhani siyo Watanzania mpaka mnafikia hata hatua ya kusema kwangu waondolewe? Wakati unapozungumza hivyo, unasahau kabisa kwamba unakiuka utaratibu unaotuzuia kubaguana sisi kwanza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kabisa tuangalie ni jambo gani ambalo linatakiwa sasa tulichangie. Mimi nilivyokuwa nafikiri, hata hawa wanaojiita wasomi, ambao wanaanza kubagua wenzao wanasema ninyi wote hapa ni Serikali, sasa tungekuwa Serikali tungekuja kuwa Wabunge wa nini? Kwa nini tusingekaa kama Serikali! Kuna shida gani ya kushindwa kuelewa kwamba kuna Bunge, Serikali na kuna Mahakama. Mtu anayesema hayo ana *PhD* lakini anashindwa kuelewa anachozungumza ni kitu gani. Unapowalaumu Wabunge wanaoilaumu Serikali, unataka washindwe kutimiza wajibu wao wa kuirekebisha hiyo Serikali ili itende haki kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tuangalie mapendekezo haya yaliyotolewa ni mazuri sana. Kwanza, kwa Serikali kama itaweza kuyasikiliza na kuyatekeleza haya, migogoro ya wafugaji itaisha. Wafugaji wameanza kuonekana ni kama watu ambao wamelaaniwa wakati kumbe kazi wanayoifanya, kwanza hawa wafugaji, navyojua mimi ni

wawekezaji. Hawa ndiyo waliokuwa wanatakiwa wawekewe mazingira mazuri ili waweze kuineemesha nchi hii. Sasa hivi ng'ombe wanapoonwa, unajua kazi ya kufuga huwezi kuvaa suti, utalazimika uvae mavazi yale yanayolingana na mazingira unapowatunzia hao wanyama. Kwa wengine wanadhani kwamba hawa watu ni watu hovyohovyo, kwa sababu wanamwangalia alivyoshindwa kuvaa suti, kumbe hawa watu suti wangeweza kuzivaa sana kwa sababu mali waliyonayo inazidi gharama ya suti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ni watu wanaojitegemea, hawa watu wanatakiwa watengenezewe miundombinu, wapimiwe maeneo yao, wakishapimiwa waambiwe eneo hili sasa tunahitaji wafugaji muweke mifugo yenu na soko la mifugo ndiyo litakalo-*control* hata wingi wa ng'ombe. Sasa ninyi mnahangaika na kusema mambo ya hovyo, eti wanafuga ng'ombe nyingi sana, kwa nini mtu mmoja anafuga ng'ombe 4,000. Mnashindwa kujua mahitaji ya nyama katika nchi hii ni makubwa kuliko hata mnavyodhani. Watu kama watakomea kufuga ng'ombe 10, hivi Dar es Salaam tu kwanza ng'ombe kwa siku moja wanachinjwa zaidi ya 1000, lakini ninyi mnajikita kuzungumzia suala la ng'ombe wanne, watapatikana wapi wa kutosha maeneo hayo? Juzi tu, Wamasai wamegoma kuuza ng'ombe, Morogoro nzima imetikisika na wanalia, nyama, nyama, nyama hamna. Sasa leo, mnashindwa kuelewa kwamba tunahitaji ng'ombe wawe wengi, Serikali itengeneze namna ya kuboresha mazingira ya kuishi hawa ng'ombe, tujenge masoko, tujenge viwanda ili ng'ombe hawa waweze kupunguzwa na vitu tutakavyovitengeneza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yetu ya Bunge kama yatafanyiwa kazi kama yalivyopendekezwa, nchi yetu itakuwa ni nchi ya kwanza kwa utajiri kuliko nchi nyingine zozote. Hata hivyo, kwa sababu maeneo haya yanazungumziwa ni ya wafugaji, nimeanza kuwasikia Wabunge wengine wanasema, kwanza wafugaji wenyewe wanaweza kujijengea mabwawa. Jamani, hivi kama wenye magari Serikali inaweka mkono wake, leo hawa watu ambao wana mifugo mnataka kila

kitu wakitengeneze wenyewe! Ndiyo maana utaona, tunapojenga barabara tunashindwa kuelewa vilevile kwamba kuna wafugaji. Tutengeneze maeneo ambayo mifugo yao itakuwa inapita kwa urahisi na wao wajione kwamba wanahusika na wanazalisha na ni wazalishaji wakubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba tuyachukue haa mapendekezo na Serikali iyasikie. Kama Serikali hii kweli inajiita Serikali sikivu, mapendekezo yaliyowekwa na Kamati yetu ni mapendekezo ambayo yanaweza yakaifanya Tanzania kuwa nchi tajiri kuliko nchi nyingine zozote kwa sababu hawa ni wawekezaji wanaojitegemea. Tuondoe ile dhana ya kudharau wafugaji hawa, tuwaone ni watu ambao wanatulisha. Wewe unaona umevaa vizuri unapendeza, unapendeza kwa kazi iliyofanywa na mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa na kuwachukia sana wanaochukia ng'ombe wakati ng'ombe ndiyo kila kitu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SYLVESTER M. KASULUMBAYI:** Mheshimiwa Spika, naomba tuyatekeleze mapendekezo haya yaliyowekwa na Kamati yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, alichosema Mheshimiwa Kasulumbayi, ndicho nilichoomba mimi jana. Maana ninyi mkiwa chanzo cha kuwagawa wananchi wa Tanzania katika mapande mapande, siyo sahihi! Tusiwabague watu wowote, sisi ni Wabunge wa wananchi wote. Kwa hiyo, ubaguzi wa namna yoyote ile tuuondoe na mkiendelea namna hii nafunga mjadala kwa sababu inaonekana taarifa hii inajitosheleza, hayo sasa mnatafuta maneno tu.

Kwa hiyo, naomba sana tusiwabague Watanzania kwa sababu sisi ni Bunge la Tanzania, siyo la mtu mmoja dhidi ya mwingine. *(Makofi)*

Tunachosema kuna matatizo kati ya wafugaji na wakulima, tufanye nini, ndiyo sababu ya ile ripoti yetu. Tusiendelee na mtindo huu, hawa wote ni watanzania, ukosefu wa amani ndani ya nchi yetu hapa hautamgusa mkulima au mfugaji peke yake, sisi ni Bunge la Tanzania, kwa hiyo, tujadili hoja iliyoko, tuiimarishe, tuiboreshe kusudi iwe nzuri zaidi.

Nilimwita Mheshimiwa Betty Machangu na Mheshimiwa Buyogera.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na kuitupia lawama Serikali. Ng'ombe wanatolewa Shinyanga, wanatembea kwa mguu, wanakwenda mpaka Lindi na Mtwara, wanaharibu mazingira, wanaharibu vyanzo vya maji na makabila mengine watakata miti yote wanayokutana nayo. Nawaheshimu sana Wamasai, wanakaa Ngorongoro kule, wanaweka mifugo kule hawakati hata tawi moja lakini kuna wafugaji wengine, mimi nimekaa Usukumani, nimeshuhudia kwa macho yangu, wakifika mahali watakata miti yote. Kwa hiyo, haya yote yanatokea kwa sababu Serikali haijaweka matumizi bora ya ardhi. Laiti Serikali ingekuwa imeweka matumizi bora ya ardhi, ikapanga hapa ni kwa Ngosha, hapa ni kwa Shija, hapa ni kwa Masanja, haya yasingetokea!

Mheshimiwa Spika, upangaji huo, uendane na uanzishaji wa viwanda vya nyama. Huyu mfugaji anatembea na ng'ombe, anaweza kuwa na ng'ombe elfu kumi, anatembea nao, kuchwa kutwa anatembea, anakonda yeye, ng'ombe anakonda. Halafu hawa wafugaji, tunasema wako *liquid*, kwamba akifika Manyoni, kuna mnada, ana shida ya fedha, anapeleka mnadani, anapata laki mbili, laki

tatu, laki nne, amefika sijui Mvomero, kuna mnada anauza, matokeo yake kule kokote atakakokwenda kama kuna ugomvi, ana uwezo wa kupigana kwa kutoa rushwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nisiwabague wakulima na wafugaji, lakini nachokisema cha kweli ni kwamba haya yanatokea kwa sababu hakuna matumizi bora ya ardhi. Naomba basi Serikali ilione hili, wamesema kuna muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, basi muda wa kati, kweli tutenge fedha tufanye hii *good land use plan,* kwamba kuwe na maeneo ya wakulima na maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, huyu mfugaji atakayepewa eneo na yeye ana ng'ombe wengi sana, basi kama ng'ombe wale watakuwa hawatoshi hilo eneo, apeleke ng'ombe wake kiwandani, apate fedha, afanye biashara nyingine, a-*diversify* yaani apanue wigo wa biashara yake. Siyo tu ang'ang'anie kwamba biashara yake ni ng'ombe. Kwanza, ng'ombe hawa wakipata matatizo, kama wakipatwa na ndorobo au nini, wanaweza kufa wengi. Kwa hiyo, pia Serikali iwaelekeze au iwafundishe namna ya kufanya biahara vizuri zaidi. Siyo ng'ombe tu, wanaweza wakafanya mambo mengi. Kule Mwanza wanaweza wakajenga majengo mazuri, *real estate,* waka-*engage* kwenye *business* nyingine wakapata fedha. Kwa hiyo, badala ya kutembea kutoka Mwanza mpaka Mtwara kupeleka ng'ombe, akafanya biashara nyingine, akawa na ng'ombe kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani wakati umefika Serikali iweke *maximum* namba ya ng'ombe ambayo mtu anatakiwa awe nao kwa sababu ng'ombe ni wengi. Sasa hivi tuko milioni 45 wananchi wa Tanzania lakini ng'ombe wako zaidi ya milioni 18 navyoongea sasa hivi. Tanzania ni nchi ya tatu kwa mifugo mingi lakini mifugo tunawafanya nini? Wanaweza wakafanya biashara nzuri. Kiwanda kikiwekwa Shinyanga, Tabora, Mwanza, watu wanauza nyama. Kiwanda kingine kikiwekwa Dodoma, Singida, Arusha watu wanauza nyama, wanapata fedha na wanahamasika lakini kwa sababu hakuna viwanda, ndiyo mtu inabidi aendelee kutembea na mifugo yake.

Mheshimiwa Spika, nilisikia wakati fulani Waziri anamwambia Mbunge, basi tafuteni wawekezaji wa viwanda vya nyama, hapana! Tuna *TIC*, hiyo ndiyo kazi yake! *TIC* itafute wawekezaji wanaofaa ambao watasaidia nchi hii. Wawekezaji wa kweli na lazima wawafundishe wafugaji hawa kwamba kitalu chako ni hiki, ng'ombe hawa walishwe namna hii, wapewe virutubisho gani ili waweze kufanya biashara nzuri.

*TIC* nakumbuka kuna wakati walikuwa wanasema wanaweka *land bank* yaani akiba ya ardhi, basi hii *land bank* wawekezaji hawa wawekwe kule kwenye maeneo ambako kunafaa kuwekwa viwanda vya nyama, viwanda viwekwe. Tunawalaumu wafugaji bure kumbe ni Serikali haiweki mpango mzuri. Naomba tafadhali, Serikali iweke mpango mzuri, wafugaji hawa wafuge lakini pia wauze mifugo yao yaani wafuge *commercially*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine nilitaka kusema, wafugaji hawa wanakwenda kwenye Hifadhi za Taifa. Naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, tunahitaji fedha, hatuhitaji tu maziwa na nyama, tunahitaji zaidi ya hapo. Waheshimiwa Wabunge na hifadhi zetu ni muhimu kweli kwa ajili ya kutupatia pato la Taifa. Bila kuwa na hizi hifadhi kutakuwa hakuna utalii, kutakuwa hamna fedha. Wizara ya Maliasili na Utalii, ndugu zangu ndiyo Wizara muhimu inayotupa pato kubwa. Kwa hiyo, tukisema sijui hifadhi tuziondoe, tuzigawe, siyo sawa!

**MBUNGE FULANI:** Kabisa!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba tuwe *realistic* kwamba tunahitaji hata hizi hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya hawa wafugaji kwa sababu nimesema wao wana nguvu zaidi ya kifedha, wakiingia kwenye hifadhi wanakuta Askari wa Wanyamapori, wanapigana nao wanawaua. Hii haikubaliki! Wanawaua kwa sababu gani? Basi ongeeni, bwana umetukuta, kama kuna faini sawa lakini mnawaua kwa nini? Mkurugenzi wa

*TANAPA* anaweka Askari wafugaji wanawaua, kwa nini? Kwa sababu tu wanataka mifugo ile! Narudi kulekule, laiti Serikali ingekuwa imepanga hapa ni kwa Ngosha, hapa ni kwa Shija, hakuna mtu angeingia kwenye hifadhi. Kwa hiyo, Waheshimiwa, naomba Serikali iweke mipango mizuri.

Mheshimiwa Spika, niongee kuhusu misitu. Sasa hivi biashara iliyoko huko mtaani ni biashara ya mkaa. Ukitoka Dar es Salaam unakwenda Arusha, mikaa ni mingi, mingi, hakuna biashara nyingine. Tena eneo hilo ni eneo ambalo linafaa sana kwa kilimo lakini watu hawalimi tena badala yake wanafanya biashara ya mkaa yaani unajiuliza, hivi kuna Afisa Maliasili kweli hapa, unajiuliza, Wizara iko wapi? Hata ukitembea kutoka Dar es Salaam unakuja Dodoma, mikaa ni mingi, mingi. Watu wameacha kulima, wanafanya biashara ya mkaa na mwisho wa siku mabadiliko ya tabia nchi yatatumaliza, nchi itakuwa jangwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tafadhali pamoja na hiyo mipango mingine lakini pia na Wizara ya Maliasili na Utalii iliangalie hili, mikaa imekuwa ni mingi mno mno. Mikaa ni mingi mno na naogopa kama mabadiliko ya tabia nchi yataendelea maana yake ni kwamba sehemu kubwa ya nchi yetu itakuwa ni jangwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Agripina Buyogera, atafuatiwa na Mheshimiwa Mfutakamba.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushuku sana kwa kunipa nafasi nami nichangie katika mapendekezo haya.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nikushukuru na kukupongeza kwa umahiri wako na kwa kweli unaisaidia sana nchi yetu katika kutafuta haki ya Watanzania. Uamuzi wako wa kunda Kamati Teule ni kutokana na malalamiko mengi ya Wabunge kwa niaba ya wananchi, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba niipongeze Kamati. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa kweli ni kiongozi ambaye wengi tunamfahamu na ni mtu mwenye misimamo kwa maslahi ya Watanzania wote. Taarifa hii kwa kweli ni taarifa iliyoboreshwa kwa viwango na Serikali mnajua kabisa mpaka Spika kuamua kuunda Kamati Teule kulikuwa na changamoto nyingi na hapa Bungeni palikuwa hapashikiki. Katika hili naiomba Serikali ikakae izingatie mapendekezo haya ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo yaliyotembelewa na katika maeneo yaliyotokea changamoto nyingi ambapo ni pamoja na mauaji ni pamoja na Jimbo la Kasulu Vijijini. Naomba Mwenyekiti wa Kamati hii na jana niliongea naye ili kuweka kumbukumbu sahihi, Kasulu aiweke kwenye orodha. Nimeangalia kwenye ukurasa wa taarifa hii, kuanzia ukurasa wa 67 - 69 ya Wilaya zilizotembelewa Kasulu haimo, naomba uiweke.

Mheshimiwa Spika, nchi hii wote tunaelewa kwamba wakati wa Baba wa Taifa tumezaliwa tunajua kwamba nchi hii inaongozwa na wakulima, wafugaji na wafanyakazi lakini leo kutokana na uzembe wa watawala wetu, wamefika mahali wametufikisha kwenye hatua ya kuanza mapigano ndani ya nchi ya maziwa hii ya Tanzania. Nchi yetu ni nchi ya asali na maziwa lakini leo wakulima na wafugaji wanapigana!

Mheshimiwa Spika, ukija kule Kasulu, wakulima na wafugaji wanapigana, miaka yote tangu nimezaliwa mpaka nakuwa mtu mzima, sijawahi kuona vita ya ukabila Kasulu! Vita ya ukabila sasa hivi imeingia ya Wasukuma na Waha maana Waha asili yao ni wakulima, siyo wafugaji lakini nyama kama alivyosema Mbunge mwenzangu tunaihitaji. Leo hatuwezi kuendelea kwa kutegemea kilimo tu, wafugaji tunawahitaji, lakini tatizo ni viongozi ambao wanakiuka sheria na taratibu walizojiwekea.

Mheshimiwa Spika, tumeweka ardhi za vijiji kusimamiwa na Serikali ya Kijiji, lakini unashangaa wafugaji wanakuja wanapokelewa na Mkuu wa Wilaya, wanaelekezwa njia ya kupita kwenda msituni.

Mkuu wa Wilaya ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Wafugaji wakishamwona Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya anampigia simu *OCD* kwamba, hakikisha unawasiliana na viongozi, maaskari walioko kwenye vituo kwenye vijiji husika watambue hao wafugaji, ni agizo la *DC!* Sasa unakuta wakulima na wafugaji, wanagombana bila kujua wamwone nani. Ukienda kumuuliza Diwani hajui, ukiniuliza mimi Mbunge kwa niaba ya Wananchi sijui, ukienda kwa Mwenyekiti wa kijiji hajui. Mwisho wa yote, Mtendaji anapigiwa simu na *DC* kwamba angalia hakikisha hao wafugaji wanapita salama.

Mheshimiwa Spika, hili ndilo limetufikisha hapa. Kwa hiyo, tunapoyazungumza haya na uzuri Kamati imefafanua vizuri, ninaomba muyaangalie kwa makini. Hatuna sababu ya kuendelea kupambana na wakulima na wafugaji. Kule kwangu watu wameuawa, wakulima na wafugaji. Wafugaji wameuawa kule Rungwe Mpya na maeneo mengi. Wafugaji wameuawa Nyarugusu. Wakulima wameuawa kule Kitanga, akiwemo na Mwenyekiti wetu wa Serikali ya Kijiji kupitia Chama cha Mapinduzi, aliuawa kutokana na migogoro hii. Wakulima wameuawa Mvugwe na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika mikoa ambayo bado tuna ardhi ya kutosha ni pamoja na Mkoa wa Kigoma ikiwemo Kasulu. Ukiona leo wakulima na wafugaji wanapambana ni kwa sababu ya kukosa Viongozi wenye utashi wa kufanya kazi. Kama ardhi tunayo, hatuna sababu. Mkuu wa Wilaya kama umeona hawa wafugaji wameingia, fuata taratibu, mshirikishe hata Mbunge ajue, mshirikishe Diwani na Mwenyekiti wa Kijiji. Wafugaji tunawahitaji, matokeo yake kule Kasulu wafugaji wanaishi kama siyo raia. Kundi kubwa hili hatufahamiani nao, wanafahamiana na Viongozi wachache, matokeo yake wanaishi msituni. Kesho wanakuwa ni watu wa kufuatwa na kutoa tu rushwa,

kujipendekeza kwa wale wachache kusema bila kuwapa hawa pesa hatuwezi kuishi hapa, siyo kweli. Lazima Serikali ihakikishe inawasiliana na Viongozi hawa, mchezo huu wa kuwagawa Watanzania ukome, kwa sababu wanajenga chuki. *(Makofi)*

Tunajua Kasulu asili yetu ni wakulima. Sasa leo kama wafugaji wanakuja, badala ya Viongozi kusema tukae pamoja tuwaunganishe hawa watu, tukubaliane kijiji kile cha Kitanga wapi na ardhi ipi ipimwe tuwaweke wafugaji, wakulima mashamba yao waendelee kulima hapa, ili mkulima akanunue maziwa kwa mfugaji na mfugaji akanunue chakula kwa mkulima, nchi yetu inaendelea. Leo hakuna sababu ya kukaa mkulima na mfugaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kukupongeza, Kamati hii imefanya kazi nzuri na ndiyo maana nimesema Kasulu iingizwe kwenye rekodi ili mapendekezo haya yaliyotolewa kwenye hii Kamati yaweze kufanya kazi na Kasulu. Kwa sababu hili ni Bunge, leo sisi tupo kesho hatupo, haya tunayoyazungumza leo hayatafutika, yataendelea kuwa kumbukumbu ili yaweze kuendelea kufanyiwa kazi kwa Kiongozi yeyote atakayekuja.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninawaomba sana Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, akiwemo Mkuu wa Wilaya Kasulu, Polisi wangu chini ya *OCD*, waendelee kukaa vizuri. Leo mnaangalia, wanaowatuma ni wanasiasa, lakini kesho mkanda ukigeuka, wanaokosa kazi na kwenda kuteseka na watoto ni ninyi watendaji wa chini. Kwa hiyo, lazima mfike mahali muanze kushtukia dili hili.

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, ninaomba uwasiliane na watu wako wa Uhamiaji, sasa hivi wameanza kunyanyasa Watanzania hasa baada ya kumaliza Uchaguzi wa Serikali za Vijiji. Amekamatwa Mwenyekiti wangu wa Serikali ya Kijiji pale Makele, anashutumiwa kuwa ni Mrundi. Haiwezekani, tumemaliza uchaguzi juzi, kuna taratibu mtu kama siyo raia anawekewa pingamizi. Anachaguliwaje na

kijiji chote mtu amezaliwa hapo, anaishi hapo, leo amekuwa Mwenyekiti anaitwa Mrundi! Naomba Mheshimiwa Chikawe, hili uliangalie na mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi, tusianze misako isiyokuwa na faida kwa malengo ya kudhoofisha Upinzani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Engineer Mfutakamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Abeidy.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa fursa hii. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati Teule pamoja na Kamati nzima, kwa Taarifa muhimu waliyotuletea, ambayo nina hakika itatatua matatizo ya migogoro ya ardhi baina ya wafugaji, wakulima na taasisi nyingine kama wanyamapori, maliasili na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kwa kina Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi. Hapa tuna changamoto kubwa sana, maeneo mengi bado utaratibu haujawekwa mahususi wa kuweza kutenga maeneo haya ya wafugaji, haya ya wakulima na haya kwa ajili ya hifadhi. Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali itenge fedha za kutosha ili maeneo haya yapimwe kwenye nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, juzi nimetoka kwenye Sherehe ya Miaka Thelathini na Nane ya Chama Tawala CCM na nimepata malalamiko; wananchi, kwa mfano, eneo la Mienze, waliomba kupitia mkoa wapate kilometa tano kwa ajili ya wafugaji waendelee kutumia sehemu ambayo kwa kweli kwa sasa ni hifadhi. Sasa ningeomba sana Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Mifugo, waje Mienze wakutane na mimi ili tuweze kupata utatuzi wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nimefanya ziara ya kwenda China nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Kilolo. Kule tulikuwa tunakwenda kutafuta baadhi ya mambo mengine, *delegation* ile ilikuwa

Maafisa kutoka Wizara ya Kilimo na Maafisa kutoka Uvuvi Zanzibar. Tukaenda kule, tulipata wawekezaji ambao wako tayari kuja kuanzisha kiwanda cha kuchinja mifugo hasa ng'ombe na kusindika nyama kwa mahitaji ya ndani na ya nje. Ningeomba maelezo kutoka Wizara ya Mifugo, jitihada zile zilifikia wapi, kwa sababu tuliporejea Tanzania tulikuwa na hawa wawekezaji lakini pia walikuja kwa masuala ya uwekezaji kwenye eneo la kilimo cha chai.

Mheshimiwa Spika, kama matumizi bora ya ardhi hayawezi kupewa umuhimu ambao unastahiki na naomba ni-*quote* kwenye taarifa hii moja ambayo inasema; upo uhusiano wa moja kwa moja kati ya maudhui ya Sera, Sheria ya Ardhi na Mkakati wa Utekelezaji wa Sheria hizo. Hivyo; Sera, Sheria na Mikakati ya Utekelezaji, vikipata usimamizi madhubuti na wenye tija, vinaweza kuepusha migogoro kati ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengi wa ardhi.

Mimi pale Igalula nina wawekezaji wamekuja Kata ya Igalula, wamepata eneo wanataka kunenepesha mifugo. Hili linawezekana kabisa, lakini tumepata ridhaa ya wale wanakijiji husika, Halmashauri imefuata taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ardhi (Na. 4) ya Mwaka 99, kwa ajili ya Serikali za Mitaa na (Na. 5) kwa ajili ya Vijiji, iko wazi na iko bayana. Unapotaka kumleta mwekezaji, lazima uhusishe wananchi walioko katika eneo lile. Mnafanya mikutano ya hadhara, kama wanataka kuhaulisha ile ardhi, kama ni zaidi ya eka 500, Mheshimiwa Rais lazima atoe ridhaa. Kuna baadhi ya maeneo, haya mambo yamekuwa yakifanywa kijanja kijanja. Mimi nimeona masuala haya Lindi na maeneo mengine, hatufuati utaratibu ambao sheria inaelekeza. Tuwe makini sana, tunaweza kutatua migogoro sana kama sheria hizi zitasimamiwa kikamilifu na wale wananchi waweze kulipwa fidia kufuatana na thamani na gharama ya maeneo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, mimi nina makundi ya tembo 15 kwenye Jimbo langu la Igalula. Tembo hawa wamekuwa

wanaishi vizuri kwa kiwango fulani na wananchi. Mgogoro umezidi kwa hawa tembo kuingilia sehemu za kilimo ambako wakulima wamelima ndizi na matikiti maji, tembo ni chakula chao kizuri, wanapita pale. Sasa zipo shuruba za wanyamapori. Kwa hiyo, sheria tukizitumia vizuri, za kuainisha hili ni eneo la mifugo, hili ni eneo la kilimo, hili ni eneo la hifadhi ya wanyamapori, tatizo hilo halitokuwepo. Wananchi wetu wapewe elimu ya kutosha ili mgongano huu usijitokeze.

Wananchi wangu wawili; Kashinje na mwingine, bahati mbaya walikanyagwa na tembo, kwa sababu wao wamejenga kwenye maeneo yale. Utaratibu wa tembo mwaka mmoja na mwaka mwingine anapopita kufuata maji au malisho, atapita eneo lile lile, hata kama kuna nyumba au umejenga miundombinu ya aina nyingine, ataivuruga ili aende akapate maji. Tukiweka uelewa mzuri, kule Mtandika na Ruaha Mbuyuni, *concern* walitusaidia wakaweka mpango bora wa matumizi bora ya ardhi kule Kilolo, tatizo hili liliondoka. Ningeomba Serikali, vijiji vyote iainishe kufuatana na Sheria na Miongozo na Taratibu hizi, naamini kabisa matatizo haya yataondoka. Uhitaji wa kutumika fedha ni muhimu sana, lakini ninaamini matatizo haya yatapungua.

Mheshimiwa Spika, matatizo yapo hata maeneo ya Nsololo, hifadhi ambayo inapakana na Sikonge, wafugaji kweli wanapeleka mifugo yao kwenye mashamba ya Wananchi. Mimi nahitaji kuwe na uwiano na mahusiano mazuri baina ya wakulima na wafugaji, kwa sababu wote wanachangia uchumi wa Pato hili la Taifa. Changamoto kubwa iko upande wa Serikali, tutenge maeneo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, Oktoba, 2010, pale Ilolwansimba, alitoa maelekezo kwamba, kuweko na eneo la kupanda malisho ya mifugo. Sasa sijui ile Sera imetekelezwa kwa kiwango gani, kwa sababu Kongwa wana maeneo ambayo wanafuga nyasi kwa ajili ya mifugo, lakini utaratibu huu bado sijauona maeneo ya Igalula na kwingineko. Sera na Mkakati huo utekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa sisi tuna mifugo ya kutosha tutawazidi Botswana. Botswana wao wana Sera na utaratibu unaosimamiwa kikamilifu, wafugaji wana maeneo ya visima ambapo mifugo inakunywa pale. Sisi idadi yetu ya ng'ombe ni kubwa na huo ni utajiri, mimi nauunga mkono kabisa, lakini lazima tufuge kwa tija. Ukimwambia mfugaji akauze mifugo, kwanza, mpe soko bora, halafu pia mpe utaratibu wa kunenepesha hii mifugo.

Kule Arusha tuna *center* ya *artificial insemination*. Ile *center* itatusaidia kuboresha mifugo. Wananchi wakiona wananenepesha ng'ombe mpaka anawapa lita za maziwa 36 kwa siku watahamasika. Kwa kutumia utaalam, tuwape elimu hii, tutakuwa na mifugo michache, yenye tija na itakayotupatia Pato kubwa la Taifa. Sekta ya Ufugaji ni muhimu kama ilivyo kwa Utalii na kama ilivyo Kilimo; kwa hiyo, tuwasaidie wafugaji, hawa ni watu wanaochangia Pato la Taifa, wawe pamoja na sisi. Tuangalie tunatenga maeneo haya kufuatana na Sheria na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi wa Mwaka 2013 - 2033. Hii miaka 20 iwe ya kujipanga.

Ndugu zangu upande mwingine msiwe na wasiwasi, Mipango hii ni madhubuti na utekelezaji wake unahitaji fedha, kwa hiyo, zitengwe fedha zinazotosha ili tuwe na matumizi bora ya ardhi katika maeneo yote kwenye Majimbo yetu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naona muda umepita, Mheshimiwa Moza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu kuhusiana na mgogoro wa ardhi.

Kwanza kabisa, nikupongeze wewe kwa juhudi zako na hekima ulizotumia kuweza kuteua Kamati hii Teule, ikiongozwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka, pamoja na Wajumbe wake wote. Nawapongeza sana, kazi waliyoifanya ni kubwa na wametumia busara kubwa sana kuweza kuangalia migogoro yote katika maeneo yote ya nchi yetu ya Tanzania. Jambo ambalo lilikuwa linachukua sura mbaya na ya kutia aibu kabisa nchi yenye amani, ambayo ni kimbilio kubwa la Wananchi wa kutoka nchi jirani. Watu wengi kutoka nje wanakimbilia Tanzania kwa kuwa ni nchi ya amani. Leo hii tunashuhudia nchi yetu ya Tanzania ilitaka kuanza kugeuka kuwa ya umwagaji wa damu.

Tumeona maeneo mengi ya migogoro ya ardhi, huko Morogoro wakulima na wafugaji, tumeona huko Mwanza maeneo ya Geita na tumeona maeneo mbalimbali ambayo Kamati imepita na mengine ambayo hawakupitia. Kwa mfano, wawekezaji wengine walioko huko Mbeya, ambao waliweza kuwapiga watu na kuwaathiri viungo vyao na mpaka leo hii hawajawezeshwa kwa njia yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la migogoro. Migogoro hii tukiiangalia imeanzishwa na Viongozi wa maeneo husika. Kama hivyo ndivyo na imejulikana hivyo, naomba suala hili lichukuliwe kwa haraka na mapema mno. Viongozi wote waliohusika kwenye masuala kama hayo, sheria iwaangalie kwa sababu wamechangia kuwapoteza wananchi, wananchi wenyewe kwa wenyewe wamegongana na wakulima na wafugaji wamepigana, ambao wote ni ndugu.

Tumeshuhudia maeneo ya Kiteto pale, nimefika eneo lile, imekuwa kama uwanja wa mauaji. Mambo yaliyokuwa yakijitokeza Serikali ilikuwa ikifumbia macho mpaka nilipolizungumzia sana hapa Bungeni. Kwa kweli nimeishukuru Serikali kwa kuchukua hatua, wameweza kudhibiti kwa kiwango fulani, lakini bado mauaji yanatokea mpaka majuzi, tumeona hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inatenga baadhi ya maeneo kwa ajili ya Jeshi. Nimekuwa nikiomba au kupendekeza basi angalau kungejengwa Kambi ya Jeshi pale eneo la Kiteto ili kuzuia mgongano mkubwa ambao unaweza kujitokeza. Kwa sababu kama wale Viongozi waliokuwamo wako pale, na ndiyo wenye migogoro hiyo, wanaipokea na wanaianzisha na wanailinda, hawajachukuliwa hatua zozote, angalau likijengwa Jeshi hilo litaweza kudhibiti kiwango fulani cha kutokea mauaji ya wananchi ambao wanapotea bila hatia yoyote, wanauwana wenyewe kwa wenyewe bila ya hatia; huu ni mgongano.

Chanzo kikubwa ni mgogoro wa Pori la Akiba la *WMA*. Pori lile limeanzishwa pale halikushirikisha wananchi. Maeneo mengi yanatengwa, lakini wananchi hawashirikishwi. Hii ni moja ya migogoro. Pili, hakuna mipaka ya Wilaya kwenda Wilaya, mipaka ya Mkoa kwa Mkoa, imekuwa ni ya muda mrefu. Angalau na Wananchi sasa waanze kutambua maeneo yao husika, kila mtu asivuke kwenda kwenye eneo la mwenzake. Hii imeleta migogoro mikubwa sana.

Nimeshuhudia hata kule Wilaya ya Kondoa, eneo la Mkongonero, tatizo ni hili hili la mipaka, *beacon* zinazowekwa ni ndogo mno, mkulima akija pale hata akilima anazifukia. Baadaye inaonekana hakuna *beacon*, inasababisha kutokutambua maeneo ya mipaka kwa wale ambao wanakaa maeneo yale.

Askari wa Wanyamapori nao wamekuwa wachochezi wakubwa wa migogoro hii. Nimeona mpaka wapewe pesa, wanapewa pesa wanaruhusu Wananchi wenye pesa wanaenda kulima maeneo yale. Asiyekuwa na pesa haruhusiwi kulima pale; unafikiri inatokea nini? Lazima mgogoro utatokea kwa sababu kila mtu anahitaji mahitaji yake ya huduma ya jamii.

Mbaya zaidi katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kondoa pale tumeshuhudia, tayari TAMISEMI imepeleka huduma kwenye Kijiji cha Kisondoko, pale lakini eneo lile

wanaambiwa liko katikati ya Hifadhi. Watu wana miaka 54 wako katika eneo lile, leo wanaambiwa wako katika eneo la Hifadhi! Tuangalie vitu vingine tuvisuluhishe, viweze kukaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mkuu wangu wa Mkoa, dada yangu Chiku Galawa, kaja juzi tu ndani ya miezi miwili amefika Kondoa. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi aliyeteuliwa juzi, dada yangu Kairuki na Mheshimiwa Mgimwa, walifanya vizuri kwenda Wilaya ya Kondoa, kuongea na Wananchi wa Kondoa na kuona matatizo yao na kero zao wameziona ingawa katika eneo lingine la Itaswi hawajafika. *(Makofi)*

Ninashukuru katika Taarifa hii, ukurasa wa 43, migogoro ya ardhi na Serikali; namba 9, wamebainisha kutambua mgogoro ulioko Atta, Itaswi pale wa Mkurugenzi na Wananchi kulima eneo la malisho. Ulikuwa mgogoro mzito sana huo, ambao uko mpaka hivi sasa.

Hii yote inaonyesha kwamba, Viongozi wa Wilaya zetu wanashiriki pia kwenye migogoro. Sasa suala hili Serikali hebu ituangalie tusipate aibu sisi kama Wabunge, kupiga kelele hapa Bungeni kila siku jamani huko kwetu kumetokea hili na lile. Hivi sasa tufike mwisho, Serikali ninaipongeza sana, ninajua hii ni Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, inaweza kufanya mambo mazuri na yenye hekima njema sana kwa kuwa na Idara nyingi zenye utitiri mwingi wa usalama, lakini bado uvunjifu wa amani unazidi kuendelea, imekuwa utawala mkubwa zaidi kuelekeza kwenye mabomu na kwenye maandamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu Swagaswaga. Wilaya ya Kondoa, pamoja na Kamati yetu kufika, lakini eneo la Swagaswaga halijaonyeshwa; pia limeanza kufukuta mfukuto huo huo wa mgogoro wa ardhi. Ninaomba jamani katika hili tuliangalie katika nchi yetu yote hii ya Tanzania, tupitie upya. Idara hii ya Ardhi sasa iwezeshwe ili iweze kuhakiki mipaka yake na Maliasili, iangalie askari wake. Askari wamekuwa waporaji, wamepora mali za watu

nyingi, wamechoma vibanda vya watu, bila ya wao kujua hatima zao na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, migogoro kama hii inasababisha wingu kubwa la njaa ambalo linaweza likaikumba jamii. Kwa hiyo, elekezo kubwa litakuwa ndani ya Serikali. Jamii inakosa huduma za jamii, watoto hawasomi mpaka sasa hivi, yote hii inatokana na migongano kama hiyo.

Mheshimiwa Spika, nije kwa wawekezaji. Kuna maeneo ya uwekezaji. Wawekezaji tunawakimbilia na ni wazuri, lakini wanawanyanyasa wananchi wetu. Maeneo mengi yaliyo na wawekezaji tumeona yana matatizo. Mimi nikigusa sehemu moja tu ya pale Atta Kondoa, mwekezaji amekaribishwa pale na wanakijiji na wakasaini bila wao wenyewe kuelewa kinachoendelea, lakini wameweka mwekezaji yuko pale kisheria kabisa.

Mwekezaji yule sasa ananyunyiza dawa mpaka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tumeshajua tatizo, utafiti umefanyika, takwimu zimepatikana, ni nusu ya kupata majawabu sahihi. Endapo takwimu hizi zitatumika kwa nia njema, kutakuwa kuna utashi wa kisiasa, kutakuwa na dhamira ya kisiasa na kutakuwa na nia njema ya kuweza

kutumia hili tatizo lililoko mbele yetu kwa maslahi mapana ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninajiuliza tangu jana tunalijadili hili nchi yetu ina itikadi gani? Tukijiuliza kwa mapana nchi yetu ina itikadi gani, itikadi ya kuuwana kati ya wakulima na wafugaji ni itikadi ya ujima. Kwa sababu mwanadamu huyu ambaye ameumbwa na Mwenyezi Mungu, ardhi tunayo kubwa zaidi ekari 900,000, lakini Watanzania wanauwana wenyewe kwa wenyewewe kwa sababu ya ardhi. Tunawaona wafugaji kwenye maeneo ya wakulima ni watu wasiofaa, wakati ni Watanzania, ni matajiri wa nchi hii kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Ukifikiria wakati wa Mkoloni kabla hata ya uhuru, kulikuwa kuna eneo linaloitwa *Maasai Land*. *Maasai Land* unajua hili ni eneo la Wafugaji tu. Kuna *Sukuma Land*. Ukikuta *Sukuma Land* unajua hapa kuna wafugaji na wakulima. Maeneo yalitengwa vizuri tu wakati wa ukoloni; sasa hapa katikati kumetokea nini?

Enzi ya ujima wanasema *Stone Age*, mwanadamu hkujua thamani ya rasilimali zilizomzunguka, hakujua thamani ya utu wa mwanadamu wala thamani ya uhai wa binadamu, ndiyo maana walikuwa wanafanya mambo ya ajabu ajabu. Nipongeze kwa dhahiri kabisa kutoka sakafu ya moyo wangu, kazi kubwa waliyoifanya Kamati hii na kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Zimeshafanyika tena Kamati nyingine za akina Profesa Issa Shivji na wakaja na takwimu. Tunajiuliza je, wasimamizi wa takwimu hizi na Taarifa hizi wako wapi?

Je, Serikali imeandaa namna gani Wataalam ikasema tunaangalia Dunia ya leo ikoje? *Let us think globally but act locally*. Hapa kwetu nyumbani, kasi ya mabadiliko Duniani leo hii ikoje?

Mheshimiwa Spika, tuandae Wataalam, tuseme Wataalam hawa wanapelekwa Duniani huko kuona kuko

namna gani. Waje na utaalam ambao wamejifungia tu, wanaona kasi ya mabadiliko Duniani na sisi tukimbizane na kasi hiyo. Hapa kwetu tunaanza kulialia wengine wanafikiria Washington halafu sisi ndiyo tunatenda, watakuwa wanatuvuruga vuruga Dunia hii na hili linakuwa ni tatizo la Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme kabisa wafugaji tulionao ni utajiri mkubwa, tunatakiwa turinge, tuwe na jeuri kubwa kwamba hawa ni matajiri, lakini utaratibu uko wapi? *(Makofi)*

Maendeleo yoyote ya mwanadamu yanatokana na mfumo wa elimu inayojali utu. Tumeandaa vipi Sera yetu ya Elimu hata ya sasa hivi ya Mwaka 2014 ilianza tangu mwaka 2006, imeshapitwa na wakati. Kabla hamjaizindua imeshapitwa na wakati! Inaandaliwa namna gani Sera ya Elimu ya kuandaa Watanzania kuiona miaka 50, miaka 100 ijayo?

Mheshimiwa Spika, ninasema hivi kutokana na itikadi yetu tu. Angalia nchi zetu, nitatoa mfano Netherland, Wadachi hao; Wadachi wana eneo dogo la ardhi, ekari 36,000, ni ndogo kuliko Mkoa wa Kagera, lakini wanaishi pale wako zaidi ya Wadachi milioni 16. Eneo moja la Mtanzania leo hii wanaweza wakaishi Wadachi zaidi ya 20.

Wanawezaje kuwa na eneo la ardhi ekari 36,000, watu zaidi ya milioni 16 na wakawa na eneo la kufuga, eneo la kulima na *natural areas* zaidi ya asilimia 62? Nimefanya utafiti huo Netherlands kwa ekari 36,000 tu na wana ng'ombe wanazalisha maziwa, Tanzania tunanunua maziwa kutoka Netherlands, hivi tuna akili timamu kweli au ni utaahira, yaani ni shida kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekosa kufikiri. Tusipojitambua tukajua tuko wapi, tukawa na utulivu wa ndani, tukaiangalia Tanzania miaka 20 mpaka 55 ijayo, tutaendelea kulumbana tu hapa. Wenzetu walipotoka kwenye Ujima wakaenda kwenye Ukabaila, miaka ya 1648 mpaka 1689, wakatoka

kwenye Ukabaila wakaenda kwenye Ubepari, wakaja na Kanuni ya Kidemokrasia, hakuna kulipa kodi kama hakuna uwakilishi. *No taxation without representation*. Walikuwa wanafikiri kwa mapana.

Mwalimu Nyerere na mengine mengi tu, sawa alikuwa na Itikadi ya Ujamaa. Itikadi yake ya Ujamaa ikawa lengo ni kujitegemea. Leo hii tatizo la ardhi Tanzania, leo hii tatizo la wakulima na wafugaji Tanzania, maeneo ya Hifadhi ya Watanzania, itikadi yetu ni nini, lengo letu ni nini ili tuweze kuondokana na matatizo haya?

Mheshimiwa Spika, nishauri tu, takwimu hizi zilizopatikana, zichambuliwe kwa ufanisi. Zikichambuliwa utapata ubora wa takwimu ukoje na ukubwa wa tatizo ukoje. Sasa ukishaligawa lile tatizo unalipatia tiba na unaangalia hatua za kuchukua huko mbele ya safari. La sivyo, tutakuwa tunazungumza tu, hakuna usimamizi ulio bora. Namna gani tunapanga, namna gani tuna-*organize*, namna gani tunaratibu, namna gani tunaelekeza na namna gani tunasimamia matatizo haya?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwa mapana hayo na tukaona duniani kukoje halafu wawekezaji, unajua mtu anaweza kuwa na ekari 50,000 hata 100,000 ukaona huyu ni adui. Mwekezaji huyu mwenye ekari 100,000 akiweza kuwekeza vizuri na akatoa ajira zipatazo 1,000 mpaka 2,000, huyu utamlalamikia nini; kwa sababu huyu ni mwekezaji ameshaondoa tatizo la ajira?

Wewe ambaye una ekari na tatizo letu la kimfumo Kiteto, Kilosa ni sisi Viongozi. Mawaziri wangapi, Wabunge wangapi na Viongozi wengine wastaafu wangapi wenye ardhi kubwa kwenye maeneo haya? Sasa *DC*, atasuluhishaje migogoro ambayo bosi wake ndiye mwenye kuleta mgogoro pale? *(Makofi)*

*DC*, huyu atasuluhishaje migogoro ya Wakulima na Wafugaji wanaopigana Morogoro Mjini kana kwamba pana

ardhi pale Morogoro Mjini kwa sababu ya matatizo ya Kilosa? *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuna tatizo la kimfumo la kimaadili. Sasa bila kujitambua kwamba hili ni tatizo kubwa, tuone hapa tulipofika namna gani tunahitaji nini, labda tunahitaji itikadi ya utu, lengo lake ikiwa ni Ustawi wa Jamii. Jamii ya namna gani? Jamii yetu sisi Watanzania kwa pamoja, ili kila Mtanzania awe na haki ya kuishi. Huyu mkulima apewe haki yake, Tanzania ni yake. Huyu mfugaji apewe haki yake na turinge kwamba tunao wafugaji wana utajiri mkubwa. Sasa ni kazi yetu sisi kuratibu vizuri na hili linahitaji Wataalam.

Sisi tukishalizungumza na wale wenye kufanya maamuzi, tukubali kufanya maamuzi kwa kutumia takwimu za kitaalamu. Tusitumie tu basi umeibuka huko una *knowledge* ya jambo hilo unaona basi unaweza kufanya upendavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia njema, sisi tuna kilometa za mraba zaidi ya 900,000, tukizitumia vizuri, maeneo ya hifadhi yatakuwepo, kilimo kitaendelea vizuri na tutauza nje na wafugaji watafanya kazi yao vizuri sana na watazalisha vizuri sana. Wawekezaji nao vilevile watakuja bila matatizo. Leo hii Wamarekani wanatafuta wawekezaji kutoka China, sasa uwekezaji huu unatumikaje kwa nia kubwa?

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Prof. Msolla!

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii, niweze kutoa mchango wangu katika Taarifa hii ya Kamati. Vilevile nakushukuru sana wewe mwenyewe kwa kuunda Kamati hii Teule, ambayo imepata fursa ya kuangalia maeneo mbalimbali, yanayohusiana na migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji, hifadhi na watumiaji wengine wa ardhi.

Katika mazungumzo yaliyoanza toka jana katika michango mbalimbali, baadhi ya wachangiaji wamesema huku Kamati haikufika, hapa Kamati haikufika. Mifano imetolewa Tanga, leo imetolewa Mara. Nipende kueleza tu kwamba, Kamati ilichukua *sample*. Tunaamini kwamba, *sampe* iliyochukuliwa ina-*reflect* matatizo ya sehemu mbalimbali hapa nchini na kwamba, Taarifa hii, imani yetu ni kwamba, Serikali itaifanyia kazi, si kule tu ambako Kamati ilifika, sasa ifanyie kazi kwa eneo kubwa zaidi.

La pili, nami napenda kukiri kwamba, migogoro ya ardhi, imekuwepo kwa muda mrefu, kwa zaidi ya miaka 50. Kwa hizi siku za karibuni, migogoro hii imezidi kuongezeka na sababu mbalimbali zimetolewa kwenye Taarifa hii. Ningelipenda kusema kwamba, sababu kubwa ya msingi ya kuwepo kwa migogoro hii ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali ni kuwepo kwa ardhi ambayo haina mwenyewe. Hili ndiyo tatizo kubwa.

Ningelipenda kumnukuu Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ambaye aliwahi kusema na alisema kwa Kizungu: *"Land without title deeds, is in itself a cause of disputes and conflicts."* Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo hali halisi tuliyonayo hivi sasa. Jana baadhi ya wachangiaji wameeleza, tunavyo vijiji zaidi ya 12,000 hapa nchini, lakini vile ambavyo vimepimwa mipaka yake ni vijiji chini ya 1,000. Kwa hiyo, zaidi ya vijiji 11,000 havijapimwa; hili ni tatizo. Hiyo tunazungumzia mipaka tu, lakini katika vijiji hivyo 1,000 ambavyo vimepimwa mipaka, vile ambavyo vimekuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi ni vichache sana. Kwa hiyo, hili nalo limekuwa ni tatizo kubwa na limesababisha migogoro mingi ambayo tumekuwa tukiizungumzia.

Mheshimiwa Spika, tufanye nini kwa sasa maana kila mmoja amezungumza hapa nini kinachotakiwa kufanywa? Mimi ninafikiri kwanza hatufahamu tulichonacho. Tunatakiwa kuchukua *stock* ya nini tulichonacho. Tuna ardhi kiasi gani,

inayofaa kwa shughuli gani. Tunazungumza hapa kwa ujumla kwamba, tuna eneo la mraba *square kilometre* zaidi ya 900,000. Kwa muda mrefu tumezungumza kwamba, tuna eneo linalofaa kwa kilimo zaidi ya hekta milioni 44, zinazofaa kwa umwagiliaji zaidi ya hekta milioni 29.2, lakini hizi ni takwimu za siku nyingi zimepitwa na wakati.

Wakati idadi ya watu imeongezeka na idadi ya mifugo imeongezeka. Kuna Mbunge mmoja hapa amesema kwamba, Tanzania ni nchi ya pili kwa idadi ya mifugo kwa maana ya ng'ombe; hii siyo kweli. Tanzania sasa ni ya tatu. Ya kwanza ni Ethiopia, Sudani ni ya pili bado na Tanzania ni ya tatu. Kwa hiyo, hata eneo ambalo linafaa kwa kilimo hatulifahamu. Aidha, idadi ya mifugo tuliyonayo, sensa iliyofanywa mara ya mwisho ni zaidi ya miaka kumi. Hata mifugo tuliyonayo tunakisia. Tunahitaji kufanya sensa ili tujue nini tulichonacho, hapo ndiyo tunaweza kuweka Mipango. Hatuwezi kuwa na Mipango bila kufahamu nini tulichonacho. Hili ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, upimaji wa ardhi, wengi wamezungumza kwamba kuna gharama kubwa na kweli ni gharama, lakini angalau tungeanza hata kwa awamu, tungeweza kupunguza hili tatizo kwa sehemu kubwa. Jana mchangiaji mmoja, Mheshimiwa John Chiligati, alitoa pendekezo la kuanzisha Mfuko wa Urasimishaji na baadaye akapendekeza Tume. Ninaiomba Wizara ya Ardhi, ilitazame jambo hili kama linawezekana ili utaratibu huo uweze kuanza. Kwanza, tuanze na bajeti, ili pole pole tuendelee kupima mipaka ya vijiji na matumizi bora ya ardhi ili hatimaye tuweze kupunguza hii migogoro.

Mheshimiwa Spika, tukipima maeneo haya, ni dhahiri mtu akipewa eneo kama ni kulima atalima kufuatana na eneo alilonalo, kama ni kufuga atafuga kufuatana na eneo alilonalo. Kwa hiyo, tutaingia kwenye *intensive agriculture* na *intensive livestock keeping*. Kadiri watu wanavyoongezeka, ardhi hii itazidi kuwa tatizo; kwa hiyo, ni muhimu mambo haya yakaanza sasa kuliko kungojea mpaka siku za baadaye.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza sana juu ya wafugaji kuwa na mifugo mingi. Mimi niseme tu kwamba mifugo mingi ni fursa! Ni fursa kubwa kwa sisi Watanzania. Tuna ng'ombe karibu milioni 23. Mifugo hii kama ingetumika vizuri, ingetupa utajiri mkubwa sana. Mifugo hii kwa wale ambao hawafahamu, kama tungekuwa tunaagiza mazao ya mifugo kutoka nje, kuanzia nyama, maziwa, jibini na kila kitu, Tanzania ingekuwa inatumia fedha nyingi sana za kigeni. Lakini kwa kuwa tunazalisha sisi wenyewe, mahitaji yetu ya nyama tunajitosheleza. Maziwa nayo tungeweza kujitosheleza. Kwa hiyo, kuna *import substitution* kubwa ya matrilioni ya Shilingi.

Kwa hiyo, nafikiri kwamba changamoto yetu ni namna tunavyoitumia mifugo yetu vizuri ili iweze kuwa na tija zaidi na tuweze kunufaika zaidi.

Wafugaji tunasema wanahamahama na sababu zao za kuhama zinajulikana. Lakini ndugu zangu, sio wafugaji tu wanaohama, hata wakulima wanahama. Mfano, dhahiri kabisa Mkoani Iringa sehemu ya Ismani, miaka ya 1950 na 1960 zilijulikana sana kwa uzalishaji wa mahindi, walilima kilimo cha *shifting agriculture,* baadaye ardhi ikapoteza rutuba, wakulima wote walihama wakaingia kwanza Mpwapwa…

**SPIKA:** Nakuongezea dakika tano zaidi!

**MHE. PROF. PETER MAHAMUDU MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Wakahama wakaingia Mpwapwa na baada ya kutoka Mpwawa wameingia Kongwa na kote wanakohama ni kwamba ardhi inakuwa imeharibika. Kwa hiyo, *shifting agriculture* imekuwepo. Kwa hiyo, siyo wafugaji tu wanaohama na wakulima vilevile wanahama. Tatizo sasa hivi lililokwenda kuingia Kiteto ni vilevile baada ya Kongwa kuanza kuwa haizalishi vizuri, wakulima wakaona nao waanze kusogea sehemu nyingine. Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kuingia kwenye *intensive agriculture* ili kusudi tutumie eneo dogo ambalo litazalisha kwa tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tuna tatizo la viwanda, hatuvuni mifugo yetu kadri inavyotakiwa. *Recommended take off* ya mifugo ni asilimia 10 kwamba kwa kila mwaka angalau tuvune asilimia 10 ya mifugo yetu. Lakini huko hatujafikia kwa sababu hatuna masoko ya uhakika na hatuna viwanda vya kusindika. Tulikuwa na *Tanganyika Packers* ambayo zamani ilifanya kazi nzuri sana hata kusindika nyama za kopo, lakini kiwanda kile kilikufa, aliyepewa akageuza kwa matumizi mengine. Serikali imejitahidi sasa hivi kujaribu kujenga kiwanda cha kusindika nyama pale Ruvu. Nafikiri jiwe la msingi liliwekwa mwaka 2010 na Mheshimiwa Rais wetu, lakini mpaka leo hii majengo yale yamebakia kama magofu.

Mheshimiwa Spika, wenzetu kama Botswana kama ambavyo wengine wametoa mfano, kuna *Botswana Meat Commission*, kile kiwanda *literally* ni cha Serikali na kuna utaratibu watu wanauza wanapeleka mifugo yao, wanachinja na kila kitu, hakuna zao linalotupwa lakini sisi hapa viwanda vya ngozi vyote viliuzwa na hatuna mahali pa kusindika ngozi, hakuna mahali pa kusindika nyama. Kiwanda kilichokuwa kinajengwa Shinyanga, mpaka leo hakijafika popote! Kule Mbeya nako kulianzishwa kiwanda, lakini hatujafanya kitu.

Mimi naisihi Serikali kwamba kwa jambo kama hili na kwa zao kama hili kwamba sisi ni wa tatu Afrika kwa wingi wa mifugo na hatuna viwanda, hii kwa kweli haitupeleki mahali popote, bali inachangia tatizo la migogoro ya ardhi ambayo inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, hatuna miundombinu ya mifugo; hatuna majosho ya kutosha, hakuna malambo ya maji, hatuna malisho ya kuaminika. Zamani katika Wizara ya Kilimo na Mifugo kulikuwa na Idara iliyokuwa ya *Range Management*. Idara hii kazi yake ilikuwa ni kuchimba mabwawa, kutengeneza majosho na kuhakikisha kwamba mbegu za majani zinapatikana na kutawanywa.

Mheshimiwa Spika, nina hakika tukirudi katika mkondo huu na hasa kama bajeti inakuwa ya kujitosheleza; Wizara

ya Mifugo inapewa bajeti ndogo na hata ile ndogo ambayo inaahidiwa haipatikani mwisho wa mwaka. Kwa hiyo, kuna haja ya kuzingatia jambo la bajeti ili kusudi haya malengo ambayo yamewekwa yaweze kupatikana.

Kubwa zaidi kuliko yote, kadri watu wanavyozidi kuongezeka tuna haja ya kugeuza aina ya kilimo chetu na ufugaji wetu kuwa wa kisasa zaidi na cha kibiashara kwa sababu bila kufanya hivyo mifugo itazidi kuongezeka, tutakuwa na mifugo mingi ambayo haina tija. Maeneo yetu nayo yatazidi kuharibika.

Mheshimiwa Spika, wengi hapa wamesema kwamba watu wanaongezeka na mifugo inaongezeka. Wakasema ardhi inabakia pale pale! Siyo kweli, hata ardhi imepungua. Tuna sehemu ya ardhi kwa sababu ya ongezeko la kina cha maji ya bahari imezama, lakini *productive land* au ardhi ambayo inafaa kwa uzalishaji nayo imepungua kwa sehemu kubwa. Nimetoa mifano ya maeneo machache ambapo hayo yamejitokeza na watu wakalazimika kuhama kwa sababu uzalishaji wake siyo mzuri.

Mheshimiwa Spika, tunayo Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi chini ya Wizara ya Ardhi. Tume hii imebakia kule juu tu, haina matawi! Miguu yake haifiki chini. *National Land Use Planning Commission* inatakiwa ipewe nguvu zaidi, ipewe vitendea kazi na tupate wataalamu ambao ni bora zaidi. Lakini zaidi ya hapo, ni lazima Tume hii iwe na Ofisi katika Mikoa, isaidiane na Mabaraza ya ardhi ili kusudi matatizo yote ya ardhi yaweze kutatuliwa kwa pamoja wakishirikiana na Mabaraza ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda kuwashukuru sana wote waliochangia. Nilichokuwa nategemea zaidi ni kwamba katika taarifa hii tungejadili zaidi mapendekezo, maana yake sasa kila mmoja wetu amekuwa kama analalamika. Lakini mapendekezo yaliyowekwa hapa naona kama ni Wajumbe wawili tu walioyazungumza kwa sababu hayo ndiyo tunataka Serikali iya-*adopt* tuone kama kuna kuboresha ama namna gani, lakini haya hatujayafanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo. Pia nakushukuru wewe binafsi kwa kuunda Tume au Kamati Teule ya Bunge iliyofanya kazi kubwa, kwa uzalendo na kwa manufaa ya Taifa letu. Niwapongeze Wajumbe wote wa Kamati pamoja na wasaidizi wao kwa umakini mkubwa walioutumia wakati wa kufanya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kutoa mapendekezo machache ili kuboresha ushauri wao na kurekebisha baadhi ya maeneo katika taarifa hii.

Kwanza, tuhimize Sheria za Matumizi Bora ya Ardhi zilizopo zitumike na watendaji wanaotakiwa kutekeleza hizo sheria wafanye hivyo bila kusita. Tuwe na mfumo wa kuangalia ni wapi au katika ngazi gani hizo sheria zinakiukwa na hatua stahiki ichukuliwe. Moja, katika vigezo vya kupanua uwezo wa kazi wa kiongozi iwe usimamizi wa sheria na utawala bora *(performance of leadership based on rule of law and good governance)*.

Pili Sheria ya Kulinda Ardhi za Watumiaji Mbalimbali zitungwe mapema ili kupunguza migogoro baina ya watumiaji wa ardhi mbalimbali. Mfano Sheria za Ardhi za Kilimo, Ardhi ya Mifugo, Ardhi ya Hifadhi ya Vyanzo vya Maji na Ardhi za Hifadhi Nyingine.

Tatu, tuwe na sheria itakayodhibiti uuzawaji wa ardhi au kuhamisha miliki kiholela, tuwe na *register* maalum ya watumiaji ardhi au mmiliki ili wanaoendelea kudai ardhi na kuuza wadhibitiwe, mfano ni nchini India, huwezi kumiliki ardhi ya kilimo kama huna historia ya kuwa mkulima na upo kwenye *register* ya wakulima wenye ardhi. Hii inafanya wakulima wasiuze ardhi kiholela, matumizi ya ardhi za kilimo yanabaki

kuwa ya kilimo na huwezi kubadilisha matumizi yake. Pia matajiri wenye uwezo mkubwa kifedha hawawezi kununua ardhi hizo na kufanya wasio na ardhi kuwa wengi.

Nne, katika kitabu cha Taarifa za Kamati Teule naomba kufanya marekebisho, kwanza katika ukurasa wa 51 na 21 wanaposema wawekezaji waliouziwa mashamba ya *RIVACU* Wilaya ya Babati, hakuna mashamba ya *RIVACU* yaliyouzwa, ni *RIVACU* wenyewe wanakodisha.

Pia ukurasa wa 54-55, siyo shamba la *Kiru Six,* ni mashamba katika bonde la Kiru.

Tano, naomba nipendekeze katika eneo la mgogoro wa ardhi baina ya wanavijiji wa vijiji vya Ayamango, Gedermar, Gidejabong na Hifadhi ya Tarangire, wanavijiji hao walipewa na kuwekwa sheria kipindi cha *operation vijiji*. Baada ya miaka 30 wananchi hao hao wanaambiwa ni wavamizi katika eneo hilo. Wananchi hao walikwenda Mahakamani, baadaye walishauriwa na Serikali kuondoa kesi Mahakamani na wapate usuluhisho nje ya Mahakama, wananchi hao waliahidiwa eneo mbadala na fidia ya maendelezo kwenye ardhi hiyo. Fidia iliyolipwa ni ndogo sana na ilicheleweshwa sana, pia hadi leo hakuna eneo mbadala.

Nashauri wananchi wapewe eneo hilo kwa ajili ya ufugaji tu na siyo shughuli nyingine, pawe na mpango maalum na pia wapatiwe eneo mbadala kwa kilimo kwenye shamba la *Galapo Estate* na shamba la *RIVACU Dareda,* eneo hilo ni zaidi ya hekta 8,000. Eneo la kilimo kwa ekari tano kila kaya ni ekari 1400, hii itakuwa suluhisho la mgogoro wa eneo hilo. Pia wananchi wa eneo hilo walipwe fidia ya fedha taslimu kama hakuna eneo mbadala.

Mheshimiwa Spika, katika Bonde la Kiru tunashukuru Kamati Teule iliweza kupita na Serikali imeanza kuifanyia kazi. Tulishauri shamba la *Kiru Valley Estates Unit* Na. 19 na 20 nalo lichukuliwe na Serikali kwa kumfidia huyo mwekezaji na pia shamba la *Kiru Plantation* na *Hamir Estate* ambapo Serikali ilianzisha vijiji kisheria ndani ya eneo la *lease*.

Mheshimiwa Spika, tunashauri hizo hati *(lease)* wenyekuzimiliki warudishe Serikalini na kupewa hati mpya inayoonyesha eneo ambalo analitumia kwa sasa. Wapewe fidia kwa eneo wanalorudisha kwa wananchi kama Kamati ilivyopendekeza.

Pia wananchi wachache waliopo katika mashamba ya *Mombo Estate, Hair Estate, Mara Estate* na zingine wapewe maeneo kwenye shamba la *RIVACU Dareda.* Muhimu pia kuchukua hatua kwa wananchi waliokuwa na maeneo kijijini na pia kuvamia hayo mashamba wachukuliwe hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, tunaomba suala la eneo la Mwada - shamba halali la wananchi lililochukuliwa kutoka Kijiji cha Mwada na *RIVACU* lirudishwe kwa wenyewe.

Pia eneo la Vilima Vitatu, mahali Serikali ya kijiji ilitoa eneo kwa wawekezaji na kuweka eneo la hifadhi *(buffer zone)* na kutaka kulazimisha wafugaji kuondolewa katika eneo hilo la Mdorie kumpisha mwekezaji maboma yamechomwa moto, watu na mifugo wameteswa, naomba hatua stahiki zichukuliwe. Eneo hilo ni la wafugaji tangu mwaka 1967 kuna miundombinu leo ni mwaka 2008 walitoa eneo kwa *WMA.*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali kuchukua hatua stahiki kurudisha maeneo ya wafugaji na hizo kanuni za *WMA,* wafugaji na wakulima walidanganywa na viongozi kuanzisha hizo *WMA* na leo zimekuwa kero.

Eneo la Kakoi, viongozi walikamatwa na kushitakiwa kisa mwekezaji wa kitalu cha uwindaji kabadilisha matumizi kuwa utalii wa picha. Leo hii wananchi kwenye eneo lao la *WMA* hawapati huduma ya malisho, dawa za asili, majani ya kuezekea nyumba, miti ya ujenzi, kuni na wanateswa. Tunashauri maeneo haya ya uwindaji wa kitalii na picha yafutwe, ni hatari kwa hifadhi ya Tarangire, sababu sasa tuna *private park* iliyopakana na Tarangire, mapato ya Tarangire yatashuka.

Mwisho, naomba shamba la *RIVACU* na Dareda lirudishwe kwa wananchi. Vijiji vya Arri, Dohom, Endasagu, Singu pamoja na wale wachache kutoka Kiru, Ayamango, Gedamar na Gidefabong. Haiwezekani kisa sheria haitumiki na viongozi wa Wilaya na Mkoa kisa ndiyo wanalima hapo.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwapongeza Wajumbe wa Kamati Teule, kwa hakika wamefanya kazi kubwa sana kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo yaliathirika ni pamoja na Jimbo langu la Kasulu Vijijini kwenye Hifadhi ya Makere Kusini, Pori la Malagarasi. Ninaomba nipate majibu mliyopata Kasulu kwa kuwa ninajua mlifika huko.

Mheshimiwa Spika, Kasulu katika Kijiji cha Kitanga aliuawa Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji wakati wa Operesheni Tokomeza, wakulima wa Kijiji cha Mvugwe watatu waliuawa katika mapigano ya wakulima na wafugaji. Hivyo basi kwa hayo machache ni wazi kwamba tunahitaji majibu na Kasulu isomeke katika taarifa hii. Ahsante.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Kamati Teule ya Bunge iliyochunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa maeneo yenye mashamba mengi ya mkonge ambayo hayaendelezwi kwa miaka mingi na kwa hali hiyo kutoa mwanya mkubwa kwa wananchi kuingia katika mashamba hayo kwa zaidi ya miaka 40 iliiyopita na kulima na kupanda mazao ya muda mfupi na mazao ya kudumu na kujenga vijiji na hata kufikia hatua ya kuandikisha vijiji katika Magazeti Maalum ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji wa mashamba hayo kupitia Bodi ya Mkonge, *PSRC* na *CHC* umefanyika bila kuzingatia Sheria za Ardhi ambapo vipo vifungu vinavyotoa

haki kwa watumiaji wa sehemu ya ardhi iliyotelekezwa kwa zaidi ya miaka 15 na kuishi na kutumia eneo hilo la ardhi kwa zaidi ya miaka 40. Wilaya ya Muheza imefuata taratibu za kisheria kuomba kufutwa kwa hati miliki za mashamba zaidi ya saba.

Tunamshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete kwa kuonyesha dhamira ya kukubali kufuta hati za mashamba hayo na hivyo Wilaya ya Muheza kuanza kutekeleza utaratibu wa upimaji na ugawaji wa ardhi hiyo shamba moja baada ya lingine. Tumeanza na shamba la Mkonge la Kibaranga.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, yapo mashamba mawili ya Kumburu na Muheza Mkumbi yalibinafsishwa na kuuzwa kwa wawekezaji bila kuzingatia utaratibu na haki za wananchi walioishi kwa miaka mingi ndani ya mashamba hayo. Matokeo yake sasa mauaji yametokea katika shamba la Kumburu kati ya wananchi, wafanyakazi wa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, naambatanisha pamoja na mchango huu barua yangu Kumb. Na. MB/JMZ/WAM/701/2/5 ya tarehe 03/02/2015 kwenda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi yenye vielelezo 01/02/03/04 kuonyesha hali halisi ya mashamba katika Mkoa wa Tanga, Wilaya za Muheza, Korogwe, Lushoto na Pangani (wakati huo Wilaya ya Muheza ilikuwa pamoja na Wilaya mpya ya Mkinga).

Mheshimiwa Spika, nashauri ripoti hizo na vielelezo vyake viwe sehemu ya ripoti ya Kamati Teule kusaidia kuainisha chanzo na kuongezeka kwa migogoro ya ardhi kati ya wananchi/wakulima na wawekezaji Wilaya ya Muheza na Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, Kamati haikupata fursa ya kutembelea Mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi ambako athari za uhamiaji na mifugo ni jambo jipya, halikuwepo kwa miaka mingi tangu uhuru wa

nchi yetu. Hata hivyo, mapendekezo ya Kamati kwa kiasi kikubwa yanatoa ufumbuzi wa changamoto zilizopo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri/ mapendekezo ya kuboresha mapendekezo ya Taarifa ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 58 wa Taarifa, mapendekezo ya muda mrefu, pendekezo la muda mrefu namba 2. Pendekezo hili lisiwe chini ya mapendekezo ya muda mrefu kwa tafsiri iliyotolewa ukurasa wa 57, aya 3.8.3. Hii ni kwa sababu utekelezaji wa pendekezo hili unatakiwa kuanza mara moja kwa maana ya bajeti ijayo na pia utekelezaji huo uwe wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, vilevile pendekezo lisiishie 'kuheshimu bajeti…' bali tuanze na kutenga fedha za kutosha kwa kadri iwezekanavyo na kuheshimu bajeti hiyo katika hatua ya utekelezaji wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 49, aya ya 19, dosari katika utaratibu wa kupima na kusajili vijiji. Pendekezo la Kamati ni zuri na liko sawa isipokuwa nashauri uboreshaji kama ifuatavyo: "Kwa kuwa wananchi wanaotaka kuunda kijiji kipya wanatoka katika vijiji vilivyopo (vijiji mama) basi uanzishaji wa vijiji vipya pamoja na vigezo vingine vilivyotajwa uhusishe pia "ridhaa" ya vijiji mama watokako wananchi hao".

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 38 na 39. Kudhibiti uswagaji wa mifugo, aya ya pili na kutenga njia za kupitisha mifugo aya ya 3. Napendekeza pendekezo katika Taarifa ya Kamati, namba 2(c) lifanyiwe ulinganifu na pendekezo lililopo katika aya ya tatu. Inawezekana kabisa kuondoa 2(c) na kuliboresha pendekezo katika aya ya tatu kwa kuwa maneno yaliyomo yanawiana.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 47, aya ya 15, kuyafuta maeneo ya Hifadhi yaliyopoteza sifa. Mifano ijumuishe

maneno ya Muhuwesi, Huria na kadhalika katika Jimbo la Tunduru Kaskazini.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia suala hili la migogoro baina ya wakulima, wafugaji na wawekezaji. Suala hili limeitia doa chafu Serikali ya CCM, haieleweki ni kwa nini hasa mambo haya yanaendelea kana kwamba nchi hii haina utawala. Mambo ya ajabu yanafanyika chini ya Rais wa nchi ambaye ndiye mmiliki wa ardhi yote. Rais ana mamlaka ya mwisho kutwaa ardhi kwa ajili ya faida ya wananchi lakini amekaa kimya bila kutumia mamlaka aliyopewa na Watanzania kuwalinda na kulinda ardhi yao.

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ni wawekezaji wa kitabaka ambao wengi wao wanaletwa na viongozi hawahawa wanaopaswa kutulinda; kazi zao kupindisha sheria na kiburi chao tu cha madaraka kuwaonea wananchi wanyonge aliowaacha Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Cha kusikitisha kupita kiasi ni kwamba, watendaji wabovu hawa ingawa wanajulikana ni akina nani, kwani wanaishi katika utajiri wa damu lakini hawachukuliwi hatua yoyote kwa kusababisha hali ya hatari katika jamii, inatisha!

Mheshimiwa Spika, nchi hii haijifunzi hata kidogo kwa yaliyotokea Zimbabwe hadi kufikia hali iliyokuwepo. Cha kuchangaza zaidi viongozi wa nchi hii wako tayari kuwaalika makaburu walewale wakatili kuchukua ardhi ya Tanzania tena sehemu zilizo na rutuba na muhimu, hili jambo haliingii akilini hata kidogo watu wenye akili timamu kualika vita ya ardhi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ni yetu wote, inatuhusu sisi sote, kwa hiyo, haikubaliki hata kidogo, wananchi wamechoka sana kiasi cha kwamba wako tayari kwa lolote. Kinachohitajika sasa ili mradi tumetambua matatizo yenyewe kuwa kwa sehemu kubwa inatokana na uongozi wa juu na watendaji ambao hawajasimamiwa vema au wamekataa kutii kutokana na tamaa zao za utajiri na kujinuifaisha

wenyewe. Hivi sasa ni wakati muafaka wa kuchukua hatua madhubuti kuwashughulikia wote kwa kuwatangaza ni akina nani, tuwafilisi. Pia, Rais azinduke kwenye usingizi mzito achukue hatua mbalimbali bila kuchelewa ili angalau ajirudishie heshima kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, ahsante.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono taarifa ya Kamati asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba katika kuhakikisha Sekta ya Mifugo, Taasisi ya Miundombinu ya Mifugo iwe *Agency* na siyo Bodi.

Pili, Urasimishaji ardhi kwa waliopata hatimiliki *(Title Deed)* wapewe mikopo kama Mfuko wa Pembejeo unavyoelekeza kwenye kipengele cha kwanza cha dhamana za mikopo.

Mheshimiwa Spika, Lutende Kata iliyopo Jimbo la Igalula wamerasimisha ardhi yao lakini mikopo hawajapata (Mfano Mzee Hamisi Sukwa) – MKURABITA.

Mwisho, naomba elimu ya kutosha kunenepesha mifugo itolewe sehemu nyingi na hasa Igalula, kwani ilikuwa na tija. Ahsante.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, naipa pongezi Kamati Teule kwa kazi kubwa ya uchunguzi waliyoifanya. Nakubaliana na ushauri walioutoa, lakini ninayo maoni yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa kwa wakulima na wafugaji kutengewa maeneo kila Wilaya ili Mkoa na Kijiji na mipaka iwekwe vyema.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili wanapopanga kuongeza *National reserve* kwa wanyama, basi mashauriano

yafanyike ili Viongozi wa Vijiji waweze kujua athari zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji na kuishauri Serikali ili kuepusha ugomvi. Pia wananchi waelimishwe umuhimu wa kuhifadhi ardhi yao, utunzaji wa mazingira na kutoiuza kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, wakulima na wafugaji ni lazima waelimishwe namna ya kuvumiliana na kila mmoja kujua kazi yake na maeneo yao. Mipango ya uhakika ya matumizi bora ya ardhi ipangwe na isimamiwe. Wageni wasipewe nafasi ya kumiliki ardhi.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati Teule kwa kazi nzuri na ushauri wao kwa Serikali. Napenda kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba viwanja vipimwe na bajeti ya Wizara ya Aridhi na Maendeleo ya Makazi bajeti iongezeke; pili, elimu kwa Watendaji juu ya Sheria ya Utoaji wa Ardhi hasa Watendaji wa Vijiji itolewe; tatu, Wizara ya Uwekezaji bado inatoa ardhi bila ridhaa ya wananchi na maamuzi yataleta vita, hivi karibuni; nne, kuna urasimu wa Wizara ya Ardhi kutoa hati. Sijui tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, mwisho, nchi lazima ichukue maamuzi magumu kutatua migogoro hiyo kwani imegeuka kuwa siasa kuweza kushinda uchaguzi.

**MHE. NAMLOCK E. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru wote kwa kazi kubwa na nzito mliyoifanya. Naomba niishauri Serikali iangalie namna ya kutoa elimu juu ya haki ya wanawake na watoto katika migogoro hii, kwani waathirika wengi katika migogoro hii ni akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya kikatili yanayofanywa na watu dhidi ya wanawake na watoto. Kuna ukiukwaji wa haki za binadamu na hufanywa na Watendaji na Viongozi husika. Muhimu tunaomba suala la utawala bora na sheria izingatiwe. Sheria zipo, ila hazitumiki kwa sababu ya ubinafsi.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Umiliki wa Ardhi iangaliwe upya. Umiliki wa eka 50 kwa mtu mmoja inalenga zaidi wakulima, kwa upande wa wafugaji ipo *silent*. Marekebisho yafanyike ili wafugaji pia wajue sheria inawasaidiaje. Elimu kwa jamii ienezwe kuhusu haki za wakulima na wafugaji, hasa wafugaji waelimishwe kuhusu umuhimu wa kumiliki ardhi, ubaya wa kugawa ardhi kiholela, ubaya wa kuhamahama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Viongozi hasa wa kisiasa wajifunze au wachukue jukumu la kuwa wapatanishi baina ya wakulima na wafugaji badala ya kuwa upande mmoja na kusababisha uchochezi. Viongozi wote tuwe wapatanishi na siyo wachochezi, tujue wapiga kura wetu ni wakulima na wafugaji na sio jamii moja.

Mheshimiwa Spika, kilimo ni cha msimu wakati ufugaji ni shughuli ya kila siku. Wananchi waelimishwe nini maana ya matumizi bora ya ardhi na kuepuka migongano. Kwa kuwa mfumo wa umilikishaji wa ardhi uko mikononi mwa Serikali za Vijiji, Serikali itenge bajeti kuwapa elimu ya kufanya shughuli hizi kitaalamu kuliko hali ya sasa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashauri wafugaji wahimizwe kulima ili kupunguza idadi ya mifugo yenye tija.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono taarifa ya Kamati na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, ardhi inaharibiwa zaidi na wafugaji, watawala mnazidi kuangalia. Miaka ijayo tutawaachia nini watoto wetu? Ardhi ndiyo mali mama, kama kuna Serikali au mamlaka yoyote iliyopo katika madaraka ya kutawala ikashindwa kusimamia ardhi, itakuwa inafanya makosa makubwa!

Mheshimiwa Spika, ardhi inachezewa na wawekezaji toka nje na wanaitumia kukopea fedha tu, hakuna kinachoendelezwa kwenye ardhi yetu. Matumizi bora ya ardhi ni lazima yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji sehemu nyingi ikiwemo Nkansi Kusini, inasababishwa na wafugaji ambao kwanza ni wahamiaji wa maeneo, lakini pia hawaheshimu kazi ya kilimo ya wenyeji wao jambo ambalo linaleta ugomvi mkubwa baina yao.

Mheshimiwa Spika, mauaji yanayotokea ni kwa sababu hakuna usimamizi wa sheria sawasawa na rushwa zilizokithiri na kwa upande wa rushwa wafugaji wamekuwa wakipewa haki kila kesi. Tunachojifunza ni rushwa. Mahakimu wanakula rushwa, watu wanauawa, tutafute ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, suluhisho ni kwamba, tupime ardhi, tumilikishe watumiaji wake, wafugaji wawe na ardhi yao, waelimishwe kupunguza mifugo ili ilingane na ardhi waliyopewa na waelimishwe namna ya kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo ya wahifadhi kuwapiga wananchi bila sababu. Kwenye Mbuga ya Lwaufi Kijiji cha Ng'undwe siku chache kabla ya uchaguzi walivamia kijiji na kuwachalaza viboko baadhi ya wananchi. Utaratibu wa wapi? Utawala wa sheria uko wapi? Viongozi hawakemei tabia mbaya hii, kwanini?

Mheshimiwa Spika, nashauri kama kuna mtu kakosea akamatwe, apelekwe Mahakamani, sheria ichukue mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, naomba vijiji vya Kasapa King'ombe, Kilambo, Namambi, wanasumbuliwa eti wako ndani ya pori la akiba wakati vijiji vimekuwepo hata kabla pori kubainishwa. Naomba mipaka ipimwe ili kusuluhisha kadhia hii.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, suala la ardhi na mifugo limekuwa likisababisha sana migogoro nchini kitu ambacho kinaweza kusababisha machafuko, Serikali ipitie upya sheria zake ili ziboreshwe.

Mheshimiwa Spika, mfano suala la Wawekezaji kupewa maeneo makubwa yanayowazidi uwezo na badala yake wanarudi kuwakodishia wananchi, huo ni ubepari. Serikali iangalie namna ya ugawaji maeneo kwa wananchi na Wawekezaji ili mwananchi asinyonyeke vile vile kwani wananchi wengi wanakosa maeneo ya kulima huku maeneo mengi yakiachwa kuwa mapori bila kufanyiwa shughuli. Serikali irekebishe mfumo wa ugawaji ardhi na kutoa elimu kwa wananchi kujua mipaka ya wananchi na wawekezaji ili kuondoa migogoro.

Mheshimiwa Spika, watendaji wa Kata na Wenyeviti wa Vijiji wamekuwa ni tatizo katika migogoro ya ardhi, kwani na wao wamekuwa wakigawa ardhi kwa wananchi kwa kunyang'anya mashamba ya wananchi na kuwapa wananchi fulani kwa kupewa rushwa na kusababisha migogoro mikubwa ikiwemo kuchomeana nyumba, kuuana na mlundikano wa kesi za kunyang'anyana mashamba.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingetoa elimu sana kwa hawa Watendaji wa Kata, Wenyeviti wa Vijiji ambao wamekuwa wakipewa rushwa na watafuta maeneo ili waelewe maana ya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kuahidi kutenga maeneo kati ya wakulima na wafugaji lakini kumekuwa na uzembe katika utendaji na kuwaacha wakulima na wafugaji kujiongoza wenyewe. Wakulima wamekuwa wakilumbana kwa kuingiliana maeneo.

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali kwa nini isitenge maeneo rasmi ya kutenganisha maeneo ya wafugaji na maeneo ya wakulima ili kuondoa migongano.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kupanga mipango mizuri itakayotekeleza kazi ya kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji, ziba ufa kabla hujajenga ukuta. Bajeti ijayo Serikali itenge fedha za kutosha kushughulikia hili suala la kutenga maeneo ya wafugaji na wakulima ili tusishuhudie damu za wananchi zikimwagika. Yaliyotokea huko Vjiji vya

Kabage, Mnyamasi na huko Katavi, hatutaki yatokee tena na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuipongeza Kamati Teule ambayo imefanya kazi nzuri ya kutatua ugomvi wa ardhi kati ya wakulima na wafugaji kwani wote ni raia wa Tanzania, wanayo haki sawa.

Vile vile Kamati imetoa mapendekezo ambayo yatamaliza migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ugomvi wa wakulima na wafugaji. Ni ukweli usiofichika kuwa kuna ugomvi mkubwa juu ya ardhi. Napenda kuungana na Kamati kwa mapendekezo yote yaliyotolewa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iendelee kusimamia sheria ili kuondoa migogoro hii. Kuna maeneo wafugaji wanataka kuwa juu ya sheria kwani wanahamia maeneo bila utaratibu, wanajenga hata kwenye vyanzo vya maji, wanakata miti ovyo, wanachukua maeneo ya mashamba ya wakulima bila idhini.

Mheshimiwa Spika, yote haya wanafanya kwa sababu ya nguvu ya fedha ambazo wanazo. Mfano, Kata ya Chinangali Kijiji cha Mahaka, Wilaya ya Manyoni Watendaji wanapokea fedha na kunyanyasa wakulima hata kukiuka sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, naiomba Serikali kutoa semina kwa viongozi na Watendaji wa Vijiji na Kata kila unapomalizika muda wa uchaguzi ili viongozi wapate elimu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo la wakulima wakubwa kuwanyanyasa wakulima wadogo kwa nguvu ya fedha. Hii haikubaliki, Serikali isimamie sheria ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, wafugaji kupunguza mifugo; inafika mahali ardhi ya wafugaji inakuwa ndogo kwa sababu ya ongezeko kubwa la mifugo. Naungana na Kamati kuwa wafugaji wapate elimu ya kuuza mifugo ili iwanufaishe na pia kuondoa tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukiliwa na Serikali. Kumekuwa na tatizo kati ya baadhi ya wananchi na Serikali yao pale Serikali inapochukua ardhi inayomilikiwa na wananchi kwa miradi ya Serikali; hali hii inaleta migogoro. Ni vyema kuwepo maelewano na fidia kutolewa au kulipwa mapema kwa wahusika.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la watu kwenye Wilaya zenye Misitu ya Hifadhi. Wilaya ya Manyoni ina asilimia 52 ya Misitu ya Hifadhi na asilimia 48 ni makazi na mashamba ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu imeongezeka, naomba Serikali kupitia Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Ardhi waje Manyoni kuona hali halisi kwa lengo la kutafuta ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuunga mkono taarifa ya Kamati na naiomba Serikali itekeleze mapendekezo ya Kamati.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi katika nchi yetu imeendelea kuongezeka siku hadi siku. Hivi karibuni tumeona migogoro mipya iliyozuka ambayo imehusisha wafugaji na wakulima, wakiuana na mifugo ikiuawa jambo ambalo limekuwa tishio la amani kutoweka ndani ya jamii.

Mheshimiwa Spika, operesheni tokomeza ilileta maafa makubwa jambo ambalo katika maeneo mengi ambayo operesheni hiyo iliendeshwa bado kuna msuguano na chuki kubwa ambayo Serikali inatakiwa ifanye taratibu za haraka ili kuleta utulivu katika maeneo hayo. Aidha, wote waliofanya

mauaji kwa raia wasio na hatia wachukuliwe hatua za kisheria ili liwe somo kwa wengine na jambo hilo lisijirudie.

Mheshimiwa Spika, wapo wawekezaji uchwara ambao wamepewa ardhi kubwa kwa kigezoo cha uwekezaji, badala yake wametumia hiyo ardhi kuikodisha kwa wenyeji kwa bei kubwa ya sh. 250,000/= kwa msimu wa kilimo. Mfano mzuri ni eneo la Karangai, katika mashamba ya *Karangai Sugar Estate,* mashamba yaliyopo katika Wilaya ya Meru, Mkoani Arusha.

Mheshimiwa Spika, hakuna jambo linalowakera wananchi kama kukodishiwa ardhi yao ambayo babu zao waliimiliki. Wawekezaji kwa muda mrefu Wilayani Meru wamekodisha ardhi ya *Karangai Sugar Estate* kwa wenyeji wa eneo hilo. Mgogoro ulidumu kwa muda mrefu, lakini Serikali imeshindwa kuchukua hatua ya kuwamilikisha wananchi ardhi ile.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa migogoro hiyo inayoendelea kuwagandamiza wananchi na kuwakosesha amani katika ardhi au nchi yao, Serikali iwafutie umiliki wawekezaji wote nchini ambao wamepewa ardhi kwa misingi ya kuiendeleza, kuwekezaji lakini badala yake wamejigeuza madalali kwa kuikodisha ardhi vipande vipande kwa wenyeji wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba kuwasilisha.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati Teule kwa uchambuzi uliofanyika juu ya hali halisi kuhusiana na suala zima la migogoro ya ardhi iliyopo katika Taifa letu.

Kwanza, naunga mkono uchambuzi uliofanyika juu ya Sera ya Taifa ya Mifugo na namna ya utekelezaji wake, hasa katika ukurasa namba 15 wa ripoti, pale ambapo wameonesha kasoro zilizopo katika utekelezaji wa sera, kwa mfano kutokutengwa kwa maeneo mahususi kwa ajili ya

shughuli za ufugaji; vile vile na shughuli nyingine za kiuchumi. Hii ni sababu kubwa na ya msingi inayosababisha migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi nchini kuna migogoro mingi baina ya wananchi na wawekezaji. Mara nyingi wananchi wanakuwa wanaishi katika maeneo yao bila kuwa na umiliki wa maeneo hayo. Kunapotokea shughuli za madini zimevumbuliwa na wananchi mahali, mara Serikali hujitokeza na kuwafukuza wananchi waishio maeneo hayo, na wakati mwingine eneo hupewa mwekezaji. Wananchi wanaofukuzwa kwenye maeneo mara nyingi wanafanya vurugu na kunatokea migogoro mikubwa. Hivyo ni vyema Serikali itekeleze sera na sheria zilizopo ili kupunguza migogoro hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge maeneo mahsusi kwa ajili ya matumizi mbalimbali, kwa mfano wakulima, wafugaji na wachimbaji wa madini watengewe maeneo maalum, hii itapunguza migongano na migogoro inayoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuyafuta maeneo ya hifadhi yaliyopoteza sifa; Mimi naunga mkono hoja hii ya Kamati Teule. Maeneo mengi yamepoteza sifa kuwa hifadhi. Unakuta kwamba wananchi wananyanyaswa kila mwaka, wanachomewa nyumba, wanafukuzwa kinyama. Kwa mfano, katika Jimbo la Busanda kuna Kijiji cha Saragulwa kina wakazi/kaya zaidi ya mia nne, wana shule mbili na huduma nyingine. Kila mwaka Serikali inawafukuza na kuwaambia wahame wapishe hifadhi, wakati huo ni Kijiji kinachotambulika. Kwa hiyo, ili kuondoa migogoro hii ni vema Serikali ikafanya utafiti na kubaini maeneo haya kwa Tanzania nzima na hatimaye ione umuhimu wa kuyafuta maeneo haya kuwa hifadhi.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu la muhimu na la msingi ambalo Serikali inatakiwa kuliangalia na kulipa kipaumbele ni ukosefu wa miundombinu ya mifugo. Hii inasababisha wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda

eneo lingine, hivyo ninaunga mkono pendekezo la Kamati katika ukurasa wa 55 kuwa Serikali ianzishe miundombinu muhimu ya mifugo kama vile malambo na majosho katika maeneo yote yaliyotengwa rasmi kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja ya Kamati Teule.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuipongeza Kamati kwa nzuri waliyoifanya na kutuletea taarifa iliyosheheni uchambuzi wa kina na mapendekezo mazuri. Nakubaliana na mapendekeo mengi yaliyotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo lililo dhahiri linalojitokeza katika taarifa ya Kamati na kusisitizwa na baadhi ya wachangiaji huru ni kuwa sheria, taratibu na kanuni zipo lakini kwa kiasi kikubwa zinakiukwa wala hazisimamiwi.

Jambo lingine lililo dhahiri ambalo limezungumzwa ma Wabunge wengi kwa muda mrefu ni ufisadi uliokithirii katika masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Wabunge wanapendekeza yafuatayo:-

(a) Ardhi yote katika nchi hii ipimwe, kwa kuanza na maeneo yenye migogoro baina ya (i) wakulima na wafugaji, (ii) wananchi na hifadhi na (iii) wananchi na wawekezaji.

(b) Serikali itafute fedha ya kutosha kwa ajili ya shughuli ya upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukubaliana na rai kwamba watendaji wote ambao wameshiriki katika kukiuka sheria, taratibu na kanuni wawajibishwe kwa mujibu wa taratibu zilizopo za utumishi na kisha washitakiwe kwa mujibu wa sheria.

Suala la ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni katika sekta ya ardhi limezungumzwa sana na Wabunge kwa muda mrefu lakini hakuna hatua za maana zilizochukuliwa. Ukiukwaji huu unatokea nchini kote, na katika Wilaya ya Bukombe unatisha.

Mifano ni mingi, lakini nitatoa mfano mmoja wa eneo la Mlima wa Mganza na Ushirombo mjini ambalo limemlikishwa kwa watu binafsi (Bwana Juvenari na Bwana Nyerere).

La kushangaza, watu hawa wameshapata hata hatimiliki zisizokuwa na mihutasari ya Kamati za Ardhi Halmashauri ya Wilaya Bukombe na Kijiji cha Igulwa.

Maswali kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

(a) Je, eneo la Kijiji (mlima) linawezaje kumilikiwa na mtu binafsi bila idhini ya Kijiji (kupitia muhtasari wa mkutano halali wa Kijiji) na Kamati ya Ardhi ya Halmashauri?

(b) Hizo hatimiliki ambazo watu hao wamezipata kinyume na taratibu ni halali?

(c) Je, Wizara itachukua hatua gani (i) dhidi ya watendaji waliohusika na (ii) kuhusu umiliki wa eneo hilo?

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, naomba nami niungane na wenzangu kuchangia suala lililopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Spika kwa kuunda Tume hii iliyoongozwa na Mwenyekiti na Kamati yake yote kwa kazi nzuri na nzito waliyoifanya kushughulikia mgogoro wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia wananchi wakiuana wenyewe kwa wenyewe wakigombea maeneo ya ardhi katika nchi yetu na Serikali imekaa kimya bila

kulitatua tatizo hili mapema. Tatizo hili limechukua sura mbaya ndani ya nchi yenye amani kama Tanzania yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia migogoro hii inasababishwa na Viongozi wenye dhamana ya eneo husika; kwa mfano, wakulima na wafugaji inatokana na kutoheshimu mali za wengine. Mfugaji anapeleka mifugo yake na kuchunga kwenye shamba la mkulima bila idhini yake. Viongozi wanalima kwenye maeneo ya malisho na kutengeneza migogoro ya kudumu na chuki. Serikali iwaangalie Viongozi kama hao.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Mkungunero ni wa muda mrefu, sasa umeshafikia hatua ya mauaji ya askari wawili, watu kupotea, kupoteza mali zao na kufungwa kiholela tu. Hali hii imefikia mpaka Januari, 2015 askari alizuiliwa kufika huko. Tatizo hili lingetatuliwa mapema hali isingekuwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, eneo hilo linasemwa ni *game reserve* baada ya kupanda hadhi, lakini watu walikuwepo humo muda wote huo. Askari na Viongozi wao wanalima hapo, wananchi hao wanakatazwa, wakitoa pesa wanalima na waliokosa pesa wanazuiliwa kukanyaga huko. Hilo linatosha Viongozi kuanzisha migogoro kwenye maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, ardhi haiongezeki, wananchi wanaongezeka na kuzaana na wanahitaji ardhi. Tukiwa tunatenga kila eneo liwe la akiba wananchi waende wapi?

Naomba Serikali iangalie suala hili kwa undani zaidi ili kuondoa migogoro ya wakulima na wafugaji na askari wa wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, nashauri eneo la Itaswi la malisho alilolima Mkurugenzi na wenzake, wachukuliwe hatua na Serikali iwakataze kuendelea na tabia hiyo, siyo nzuri na inaanzisha migogoro. Vilevile rushwa imezidi katika Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya kijiji na kata, wilaya na mkoa ipimwe mapema sana ili kuepuka migogoro. Mauaji yataisha iwapo utekelezaji utafanyika mapema.

Mheshimiwa Spika, kuna mgogoro wa swagaswaga, hamjafika, ni tatizo linalojitokeza kati ya askari wa *game reserve* na wananchi. Naomba hilo liangaliwe mapema.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono Taarifa hii pamoja na Mapendekezo yake. Maelezo yangu kwa uzoefu wa Jimbo langu la Nkasi Kusini kumekithiri matatizo yafuatayo:-

Vijiji vingi havijapimwa. Vijiji vya Namansi, Ng'undwe, King'ombe, Mlambo, Kasapa, China (Itekesha) na Kitongoji cha Nkata, wanaelezwa kuwa wako kwenye Hifadhi ya Lwanfi *(Lwanfi Game Reserve),* wakati vijiji hivyo vilikuwepo kabla ya pori lenyewe kubainishwa. Lazima mipaka irekebishwe katika vijiji hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuna mashamba yasiyoendelezwa katika Wilaya ya Nkasi kama vile vitalu vya kuchungia ng'ombe walivyopewa watu ambao wala si wananchi wa Wilaya kwa utaratibu ambao wananchi hawakuelimishwa vya kutosha ili washiriki kwenye ushindani. Shamba lililoko Kijiji cha China haliendelezwi; hivyo, lichukuliwe na Serikali kwa matumizi ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, Maafisa Wanyamapori wanawapiga Wananchi wakati mwingine majumbani mwao bila utaratibu na hakuna mtu anayekemea jambo hili hasa Serikali. Ninaomba ardhi igawanywe na watu wamilikishwe kwa matumizi yao.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Kamati Teule ya Bunge (2013), kwa kazi nzuri waliyoifanya. Taarifa iliyotayarishwa imekuja wakati mwafaka. Kamati Teule hii iliteuliwa mwaka 2013, lakini Taarifa yake imeletwa Bungeni na kujadiliwa Februari, 2015. Mategemeo yangu ni kuwa, utekelezaji wa maoni na

mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii, pamoja na michango yote iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, utachukua muda mfupi, ili tuanze kuona mabadiliko ya haraka kutokana na matatizo mengi ya migogoro ya ardhi ya Wananchi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ya Bunge hii iliyoteuliwa, wamejitahidi kufika maeneo mbalimbali. Yako maeneo mengine ambayo Kamati hii haikupata nafasi ya kufika na maeneo hayo yana matatizo na migogoro mingi. Kwa mfano, katika Jimbo la Mpwapwa – Dodoma, upo mgogoro wa ardhi kati ya Wananchi wa Kijiji cha Kibodyani na eneo la Chuo cha Utafiti wa Mifugo, *Livestock Training Institute (LITI)* Mpwapwa. Mgogoro huu umedumu kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mifugo, (mwenye dhamana ya Chuo cha Mifugo hiki) analijua tatizo la mgogoro huu. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayohusika na Ardhi, Maji, Maliasili na Mazingira, analijua tatizo hili. Kwa kuwa Kamati Teule haikupata nafasi ya kutembelea eneo hili la Kibodyani, utatuzi wa mgogoro huu utakuwaje?

Mheshimiwa Spika, mgogoro huu zaidi unahitaji uamuzi wa busara tu. Kijiji cha Kibodyani kipo Kisheria, kimeandikishwa kisheria, mpaka na eneo la Chuo imeingiliana. Mahusiano ya Kijiji hiki na Chuo cha Utafiti zamani yalikuwa mazuri, lakini hivi sasa siyo mazuri. Amani inazidi kutoweka, kesi iko Mahakamani hivi sasa, baada ya kutokea mapigano baina ya Wananchi na Chuo cha Utafiti.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mgogoro huu umekuwa ukiathiri Wananchi wa Kijiji cha Kibodyani kiuchumi na kuwafanya wakose mahali pa kufanya shughuli zao za kilimo na kutokuwa na imani na Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza mgogoro huu upatiwe ufumbuzi wa haraka kwa kuchukua hatua stahiki dhidi ya wananchi wa Kijiji hiki na Chuo cha Utafiti wa Mifugo.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Mifugo atoe maelezo kuhusu mgogoro huu unaoendelea baina ya Kijiji cha Kibodyani na Chuo cha Utafiti wa Mifugo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri Mkuu!

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nami nianze kwanza kwa kuishukuru sana Kamati Teule ambayo imefanya kazi nzuri sana, kwa maoni yangu. *(Makofi)*

Kamati ilichonisaidia mimi ni kubainisha hasa maeneo ya msingi ambayo ni ya kisera ambayo wameshauri Serikali ijaribu sasa kukaa na kutazama namna gani tunaweza tukajaribu kumaliza mgogoro huu wa muda mrefu. Sasa maadamu ni ya kisera, kwa hiyo, sasa itabidi kuambatanisha mikakati mbalimbali na katika baadhi ya maeneo pengine, hata kuwa na ratiba mahususi ya yale maeneo ambayo tunafikiri tutayapa kipaumbele.

Wameeleza vizuri sana sababu za migogoro ya ardhi na wamebainisha pale maeneo saba ambayo ndiyo wamejaribu kuyaangalia. Ukitazama katika kile eneo, wamejaribu vilevile kuonyesha nini kinaweza kufanyika kisera lakini zaidi kiutekelezaji.

Katika maeneo yale saba, eneo lililo kubwa kwetu ni hili la migogoro kati ya wafugaji na wakulima; ndiyo hasa limepewa nafasi kubwa nami nakubaliana nao kabisa kwamba ni sawa kabisa mtazamo huo, kwa sababu ni jambo ambalo sasa lipo karibu kila mahali.

Mheshimiwa Spika, rai yangu ya jumla kwanza kwa Watanzania, ni lazima kama Watanzania tukubali kwamba mkulima na mfugaji bado ni Mtanzania. Tusije tukaingia katika mtego wa kuanza kubaguana kwa sababu mmoja ni mkulima na mwingine ni mfugaji, tutakuwa tunaingia katika eneo la hatari sana kwa umoja wa Taifa letu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naamini katika zoezi hili ambalo tutalifanya hili jambo, itabidi kuliwekea msisitizo sana. Mkulima na mfugaji

ni Watanzania, kama alivyo mkulima ndivyo alivyo na mfugaji, anaweza akaishi mahali popote ilimradi tu havunji sheria. Kwa hiyo, nadhani huo ni msingi muhimu sana kwa makundi yote mawili ambayo lazima yazingatiwe. *(Makofi)*

Sasa kuna mambo mengine tutajaribu kuyatazama ya kuheshimiana na hapa tulipofika hasa baada ya mgogoro wa Kiteto upande wa Manyara na sasa Morogoro kwa maeneo mengi ambayo yapo pale; ukienda Mabwegere, ukitazama mgogoro wa Kambara na vijiji vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, kuna haja sasa ya kutumia mbinu nyingine vilevile za kujaribu kusaidia makundi yote haya mawili yaweze kutambua kwamba vitendo wanavyovifanya miongoni mwao, siyo halali, lakini vilevile ni vitendo ambavyo ni vya hatari hata kwa makundi yao wao wenyewe, hasa inapotoka na kuwa ni kisasi kwa sababu tu ni mfugaji, kwa hiyo hutakiwi. Au ni kisasi kwa sababu ni mkulima, basi hutakiwi, hapana! Hili nadhani tutafanya kila linalowezekana tuweze kutumia kila mbinu kuhakikisha kwamba linapewa uzito mkubwa, kutoa elimu lakini lakini vilevile kujaribu kutoa hamasa ya Watanzania kubadilika polepole na kufika mahali ambapo tunatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi nimesimama sehemu kubwa kabisa kukubaliana na mengi ambayo yamependekezwa na Kamati au Tume hii Maalum ya Bunge letu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali na kwa upande wangu tumeshaanza kulitazama tayari.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kuahidi ni kwamba, kimtazamo, sisi tumeona kwamba tutaunda timu *Multisectoral* mchanganyiko kidogo ya Wataalamu ili wapitie mapendekezo haya moja baada ya nyingine, tuyapange katika utaratibu wa yale ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. *(Makofi)*

Timu hii ikishafanya uchambuzi huo wa kiutekelezaji, tumetaka timu ya Makatibu Wakuu wachache na yenyewe itakuwa ni *Multisectoral,* wapitie hayo maelezo

yatakayokuwa yameandaliwa na hii timu ya Wataalamu katika kujibu au kuweka mambo ambayo tunafikiri yanaweza yakatuondoa katika migogoro hii kwa kila eneo katika maeneo yote saba ili tuweze kuwa na uhakika kwamba tutakapokuja kutoa *report* hapa, itakuwa ni ile ambayo imetoa sura inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, tumeona vilevile sasa kwamba itabidi Makatibu Wakuu wote wakae chini watazame haya yote ambayo yamependekezwa yatakayokuwa yamepitiwa na makundi yale ya chini, chini ya utendaji wao, na wao tumeomba baada ya kulitazama chini ya Katibu Mkuu Kiongozi walete kwenye Baraza la Mawaziri tuya-*adopt* sasa kama mawazo ambayo tunataka twende nayo kama Serikali katika kutatua mambo yote ambayo yametajwa katika maeneo yale saba.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo tuliyoyafanya na wachache wetu hapa Dodoma, tumeona vilevile itabidi kutazama maeneo mengine mengi ya ziada kwa sababu suala hapa ni mifugo mingi, lakini nadhani kuna haja vilevile kwanza ya kuweka mikakati ya namna ya kuvuna mifugo hiyo. Tufanye nini ili ng'ombe huyo ambaye yuko katika mikono ya watu aweze kumsaidia kubadili maisha yake kwa utaratibu mzuri wa uvunaji lakini wakati ule ule kumwezesha kuwa na maisha bora kwa sababu ng'ombe kusema kweli ni fedha ambayo iko tayari. Ukimweka vizuri, ukimuuza pesa ipo tayari. Kwa hiyo, inaweza ikabadili sana maisha na ikaondoa umasikini kwa Watanzania wengi ambao wapo katika kundi hili la wafugaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumejaribu kuangalia eneo moja ambalo nilisema nalo vilevile tuliangalie, ni huu mgogoro sasa kati ya hifadhi na wafugaji. Hili nalo linagusa maeneo mengi na hifadhi hizi zipo za sura nyingi. Zipo hifadhi ambazo ni la *Local Government,* Halmashauri zetu, zipo hifadhi ambazo zinasimamiwa na Serikali Kuu, zipo hifadhi nyingine ambazo zipo kwenye makundi ya vitalu ambayo yawekwa tayari kwa ajili ya wawindaji. Hili ni eneo ambalo linatakiwa vilevile tuliangalie sana.

Sasa mategemeo yangu ni kwamba kwa mapendekezo ambayo tumeyaona, tutaona sasa ni namna gani nzuri ya kuweza kusimamia eneo hili. Kubwa, ni lazima tuone ni namna gani mifugo hii iwe na maeneo ya kutosha kwa ajili ya malisho ili na yenyewe iweze kuwa na tija na mchango mkubwa katika uchumi wa Taifa letu. Nadhani tukiliweka vizuri hili, nina hakika kabisa tunaweza tukafanya kazi ikawa nyepesi.

Mheshimiwa Spika, mwisho nataka niseme moja ya jambo ambalo linajitokeza mara nyingi katika baadhi ya maeneo, ni tatizo lakini siyo kubwa, nadhani linatokana na sisi wenyewe watendaji. Kwa hiyo, mara nyingi katika migogoro inayojitokeza hii, baadhi ya Watendaji wa Serikali wanaigeuza inakuwa ni sehemu ya kujipatia chochote, ama kujipatia fedha. Kwa hiyo, kwa namna fulani wanachochea upande mmoja ili yeye aweze kunufaika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimesema TAMISEMI na Wizara ya Mifugo ni lazima jambo hili walitazame kwa ukaribu sana. Hawa Watendaji ambao wana-*take advantage,* wanakuwa wakati mwingine ndio wanaofanya uchochezi mkubwa katika baadhi ya maeneo ili wao wenyewe waone kwamba katika kubembeleza kundi moja, basi ni lazima umchangie, umtafutie vihela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili halikubaliki na lazima wote hawa ambao watabainika kwamba wanafanya vitendo vya namna ile, kama ni wale wa Serikali za Mitaa ni lazima TAMISEMI wachukue hatua haraka sana kuhakikisha kwamba jambo hili linakoma na wale wote wanachukuliwa hatua ambazo ni stahiki. Kuna taarifa juu ya maeneo fulanifulani ambazo zimeletwa na wafugaji ambazo zinaashiria kwamba jambo hili linaonekana katika baadhi ya maeneo limetumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi nimesimama tu kukubaliana na mapendekezo mengi yaliyomo humu na ndiyo maana nimeona niseme namna tulivyoanza kujaribu kujipanga ili kuhakikisha kwamba jambo hili sasa linakuwa ni

la Serikali kwa ujumla wake, lakini vilevile tuahidi tu kwamba tukishajipanga vizuri, tukatengeneza mkakati mzuri, na pengine ratiba ya utekelezaji katika baadhi ya maeneo, basi katika kipindi muafaka tutakachoona kinafaa, tutaleta hiyo taarifa na kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge namna tulivyokaa kama Serikali na matarajio yetu ni nini.

Mheshimiwa Spika, tutakuwa na *budgetary implications* katika baadhi ya maeneo hasa katika upimaji wa maeneo, lakini hakuna namna. Tulichojaribu kuzungumza ni kwamba Wizara ya Ardhi haiko kwenye *Big Results Now* kwa maana ya Mpango wa Matokeo ya Haraka, hapana, lakini ni wajibu wa Wizara, na bahati nzuri Waziri yupo, katika vipaumbele vyake katika Wizara kwenye bajeti ijayo, moja ya jambo ambalo lazima alipe nafasi kubwa ni upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali. Nami nitaomba sana Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono katika jambo hili kwa sababu hili naamini ndiyo litatupa ufumbuzi wa tatizo hili kwa kiasi kikubwa, baada ya pale itakuwa ni suala tu la anayevunja sheria na taratibu, basi hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na namshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Ole-Sendeka na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Imani yangu ni kwamba, huu ni mwanzo mzuri na ninafikiri tutatoka hapa tulipo katika mazingira ambayo ni mazuri zaidi kuliko ilivyokuwa siku za nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa mtoa hoja! Nakupa nusu saa kama unahitaji.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA - MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa jinsi ambavyo umeliongoza zoezi hili la kujadili hoja hii ya Kamati Teule uliyoiunda, lakini nakushukuru pia kwa uamuzi wako wa tangu

mwanzo kuamua kuiteua Kamati hii Teule ili iweze kufanya kazi hii. Nakushukuru pia kwa kutuwezesha wewe pamoja na Katibu wa Bunge kufanya kazi hii kwa ufanisi mkubwa na mara zote umekuwa ukitutia moyo na kutushauri ili tuweze kufanya kazi hii kwa maslahi makubwa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kwa uamuzi wake wa kusimama kwa niaba ya Serikali na kupokea taarifa ya Kamati Teule na kuweza kuliahidi Bunge hili na Watanzania kwa ujumla kwamba amekubaliana na mapendekezo ya Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo sisi tuliyapendekeza na yale yote ambayo yataridhiwa na Bunge, na kwamba Serikali imetoa kauli kwamba itayafanyia kazi mapendekezo haya kwa haraka zaidi kwa maana ya kuunda Kamati hiyo ya *multisectoral* na hatimaye mapendekezo haya yaweze kuingia kwenye Baraza la Mawaziri kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Waziri Mkuu nakushukuru sana na ni imani yangu kwamba, haya yote ambayo yatapitishwa na Bunge hili kama mapendekezo, Serikali yetu itayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kushukuru mtu mmoja mmoja lakini niwashukuru Wabunge wote kwa kazi kubwa waliyoifanya kuanzia kuishauri Kamati yetu lakini kwa maoni pia mengi ambayo wameyatoa hapa. Wabunge waliochangia kwa kusema, wako 38 na waliochangia kwa kuandika wako 17. Nawapongeza na kuwashukuru sana Wabunge wenzangu kwa kuimarisha ripoti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitambue mchango wa dada yangu, Mheshimiwa Halima Mdee, alizungumza hapa akasema alitoa mchango.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nataka niseme, tulipata michango mingi ya Mawaziri na tulipata pia mchango wa Waziri Kivuli. Kwa hiyo, natambua na kuthamini mchango wa kila mmoja, siyo rahisi kuyataja.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inatambuliwa duniani kama kisiwa cha amani, lakini katika siku za karibuni tumekuwa na mambo ambayo kidogo yanaanza kuharibu heshima ya nchi yetu machoni mwa nchi jirani na nchi nyingine duniani. Ningependa tu niazime maneno machache sana ya Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia, nikianza na kuazima maneno aliyoyasema Mheshimiwa Riziki Lulida ambaye naye aliyaazima kutoka kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, maneno ambayo Baba wa Taifa aliyazungumza mwaka 1958. Mwalimu alisema:

"Katika nchi kama yetu ambamo Waafrika ni masikini na wageni ni matajiri, kuna uwezekano mkubwa kwamba, Mwafrika akiruhusiwa kuiuza ardhi yake katika miaka 80 au 100 ijayo, ardhi yote ya Tanganyika itamilikiwa na matajiri wageni na wenyeji watakuwa watwana. Lakini hata kama wageni wasipokuwa matajiri, litaibuka tabaka la Watanganyika matajiri wajanja tukiruhusu ardhi iuzwe kama kanzu katika muda mchache kutakuwa na kundi dogo la Waafrika wakiwa na ardhi na walio wengi watakuwa watwana."

Maneno haya aliyasema Mwalimu mwaka 1958 kabla ya uhuru wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona niseme hili kwa sababu kuna dhana inayoonekana kwamba Tanzania bado kuna ardhi kubwa ambayo wawekezaji wanaweza kuja bila ukomo na inaweza kutolewa bila ukomo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambieni migogoro kati ya wafugaji na wakulima nchini ni ishara tosha kwamba ardhi yetu sasa ni ndogo na nina hakika mtakapofanya tathmini mtagundua kwamba hatuna ardhi kama ambavyo tunatangaza huko duniani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakubaliana na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge walioshauri kwamba kuna haja ya kupimwa kwa ardhi ya nchi yetu ili kuweza kujua tuna ardhi kiasi gani. Tulichokubaliana tu ni kwamba hatuwezi

kusimamisha shughuli zote za Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tukisubiri mpaka ardhi yote ipimwe, ila ni lazima tugawe ardhi kiasi kidogo kidogo tukitambua kwamba bado hatujajua ukubwa wa ardhi tuliyonayo na kwa sababu Watanzania mmoja mmoja na katika ngazi ya vijiji na maeneo mbalimbali wanahitaji ardhi kwa ajili ya maendeleo yao. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutenge fedha, tupime ardhi, tuweke mipango, tutenge maeneo ya vijiji, kila kijiji kipewe cheti chake, kijue mipango yake na kiweke matumizi bora ya ardhi. Tukifanya hivyo, tutapunguza migogoro ya ardhi nchini na nina hakika tutatenga maeneo ya wafugaji vizuri, tutatenga maeneo ya wakulima na kila mmoja atapaswa kumheshimu mwenzake na mazao yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge hili ni moja kati ya mihimili mitatu ya nchi yetu. Naogopa, katika siku za karibuni tumekuwa na mijadala ambayo wakati mwingine inaingilia uhuru na mamlaka ya mihimili mingine ambayo ina hadhi sawasawa na sisi.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niwape mfano wa jambo moja. Kuna kauli ambazo zimekuwa zikitoka hapa zikitaka kuonyesha kwamba Mahakama zetu nchini zinatoa maamuzi yake kwa rushwa tu. Nataka niwaelezeni, kwa mfano wa vijiji mlivyovitaja na maamuzi ya Mahakama ambayo Kamati yangu Teule imerejea, ni maamuzi ambayo hayatiliwi mashaka yaliyotolewa siyo tu na Mahakama ya kawaida, bali yametolewa na Mahakama ya juu ya nchi yetu, yaani Mahakama ya Rufaa.

Mfano wake ambao ningependa sana niseme, ni maamuzi yaliyotolewa yanayohusiana na ardhi ya Kijiji cha Mabwegere. Maamuzi yaliyotolewa na Mahakama ya Rufani, yaliyotolewa na Jaji Kimaro wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kalegeya wa Mahakama ya Rufani, kwa pamoja na Jaji Mbarouk wa Mahakama ya Rufani ya nchi yetu. Hakuna namna ambapo muhimili huu unaouongoza unaweza kutilia mashaka maamuzi yaliyotolewa na Majaji watatu wa

Mahakama ya Rufani ya nchi yetu na kuyabeza kwa namna yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, maamuzi haya ni halali, yanapaswa kuheshimiwa na Mbunge mmoja mmoja na pia Bunge zima. Tufike mahali pa kunyanyua heshima na hadhi ya Mahakama zetu. Tunatengeneza mgogoro ambao dunia nzima itatushangaa. Ni kweli wakati mwingine katika Mahakama zetu kumekuwa na rushwa rushwa zinazopokelewa katika Mahakama fulani, lakini siamini kama tumefika mahali kwa Mtanzania wa kawaida, mkulima wa kawaida au mfugaji wa kawaida, kuweza kuwa na rushwa inayoweza kufikirika kumbadilisha Jaji yeyote wa Mahakama ya Rufani ya nchi yetu. Maamuzi haya yanastahili kuheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna maamuzi ya Mahakama ya Rufani katika suala la Emmborley Murtangos kule Kiteto ambayo yaliamuliwa na Majaji watatu ambapo iliamua juu ya haki ya wafugaji na wakulima. Nasema wafugaji na wakulima kwa pamoja wa Wilaya ya Kiteto wa vijiji vinavyounda Emmborley Murtangos, maana ni vizuri kwanza ieleweke, mgogoro ulioko katika eneo la Emmborley Murtangos siyo mgogoro kati ya wakulima na wafugaji wa Kiteto, hapana!

Mheshimiwa Spika, wakulima na wafugaji wa Wilaya ya Kiteto katika eneo hilo, lao ni moja dhidi ya watu waliotoka nje ya Wilaya ya Kiteto waliongia katika eneo la Emmborley Murtangos. Ni vizuri jambo hili mkaliona na lina hukumu ya Mahakama ya Rufani. Watanzania wote tunapaswa kuiheshimu, vinginevyo basi mngeiomba Mahakama ya Rufani ipitie upya uamuzi wake.

Mheshimiwa Spika, katika eneo Vilima Vitatu, kuna maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya nchi yetu. Kubwa sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Serikali kuwa madhubuti katika kusimamia maamuzi haya na hasa utekelezaji wake. Lakini kwa namna ya pekee nakushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa uamuzi wako mwenyewe kwenda Kiteto na

kushughulikia hali ile na baadaye hali hivi sasa ni tofauti na ilivyokuwa huko nyuma. Sasa uendelee tu kuongeza ukali kidogo ili watu wasirejee tena kuanzisha vurumai katika maeneo hayo na amani katika eneo lile iendelee kuwa vizuri sana. Sasa hivi migogoro inayotokea na maafa yaliyotokea karibuni siyo pale Emmborley Murtangos, bali ni nje ya eneo lile.

Mheshimiwa Spika, ni kwa maana hiyo, nalazimika kurejea na kunukuu tena na kuyaazima maneno ya mchango wa maandishi yaliyotolewa na mmoja wa Wabunge wa Viti Maalum katika Bunge hili yanayosema hivi:-

*"Viongozi hasa wa kisiasa wajifunze na wachukue jukumu la kuwa wapatanishi baina ya wakulima na wafugaji badala ya kuwa upande mmoja na kusababisha uchochezi. Tuwe wapatanishi na siyo wachochezi." (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasikiliza mjadala hapa ndani, wakati mwingine tunakuwa wakali kweli, tunasahau kwamba sisi ni Viongozi wa wakulima na wafugaji. Mbaya kuliko yote ni pale ambapo mnasahau kwamba dunia nzima inatutazama.

Mheshimiwa Spika, sasa ukiongea kwa ukali dhidi ya hawa, ukasema kundi hili liondoke, kundi hili litoke, bonde hili libaki kwa ajili ya kilimo peke yake, lakini mifugo isikanyage katika eneo hilo, sasa unataka kufikisha ujumbe gani kwa Watanzania?

Kwamba huyu mkulima akilima kilimo chake cha kufyeka miti yote; maana wakati mwingine tuambiane ukweli, kilimo chake cha kufyeka ardhi yote na kulima na kung'oa miti na kupanda mazao anayoyapanda, hapo ardhi haijaguswa, bado ni nzima. Ila ng'ombe akija, akipita chini ya mti, akala nyasi zinazoota kwa msimu kila mvua inaponyesha, huyo kaharibu, atoke.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, pengine dhambi kubwa tunayoifanya ni kutokuambiana ukweli.

Mgogoro kati ya wafugaji na wakulima nchini, nataka niwaambieni kilichojificha nyuma ni dhambi ya Watanzania sasa kuanza kubaguana kwa misingi ya ukabila. Sasa kwa sababu huwezi kutamka kwamba hawa Wasukuma warudi kwao, hawa Wamasai warudi kwao, hawa Wakwere waende zao, huwezi kutamka hayo, sasa inabidi usingizie ni mgogoro wa kilimo na ufugaji.

Sisi tuliopata nafasi, mliotutuma kwenda huko, kuna dhambi kubwa sana na mambo mengi hatuwezi kuyasema hapa. Kuna maeneo mengine sitaki kusema ambapo Kiongozi mwenye hadhi kama ya kwangu na wewe, anasimama kushuhudia nyumba ya mmoja wa wafugaji ikichomwa. Ni mkulima lakini ni mfugaji pia wa jamii ya Kisukuma, nyumba yake ilichomwa na mazao zaidi ya magunia 200, lakini na mama anamwagiwa mafuta ya taa kwa nia ya kuchomwa, wasamaria wema wanamwokoa. Tumefika hapo! Hatutaki kusema!

Mheshimiwa Spika, ili kuweka umoja wa Kitaifa, ndiyo maana tumeacha kusema haya.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wamechangia, lakini nataka niungane na Mheshimiwa Profesa Msolla, kwamba tuna mapendekezo ambayo tumeyatoa hapa.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yatatusaidia zaidi kuweza kuishauri Serikali ili yapitishwe na Bunge hili Tukufu ili hatimaye Bunge hili liweze ku-*adopt* maazimio haya na baadaye liweze kufuatilia kila kila pendekezo lililotolewa ili kuhakikisha kwamba dhambi hii inayoendelea hivi sasa ya kubaguana na dhambi ya kuuana kati ya wakulima na wafugaji, inakoma kutoka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu ametuweka mahali pazuri sana, amesema Wakulima hawa na Wafugaji ni Watanzania, kwa maana hiyo, kila mmoja ana haki ya kwenda mahali popote ilimradi havunji sheria. Kila mmoja ana haki ya kwenda popote ilimradi havunji sheria.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo lingine la migogoro kati ya hifadhi zetu na maeneo yanayozunguka hifadhi. Ni kweli kwa hivi sasa bado nchi yetu na wataalam wetu wa hifadhi hawajajiridhisha kuona kama kuna uwezekano wa mifugo kuingia katika hifadhi bila kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni wazo langu binafsi, kuna haja ya Serikali sasa na wataalam wa uhifadhi kuangalia namna ambapo katika baadhi ya mapori tengefu unaweza kuruhusu kulisha mifugo kwa msimu na baadaye kuiondoa. Lakini ni muhimu tupate uzoefu wa nchi jirani za wenzetu na pia kutoka maeneo ya Ngorongoro ambapo mifugo na wanyama wanaishi pamoja. *(Makofi)*

Mhesimiwa Spika, napenda pia katika hilo la maeneo yenye migogoro niungane na Mheshimiwa dada yangu Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Moza Abeid, katika suala lile la *Mkungunero Game Reserve* na katika eneo lile la Tarangire.

Mheshimiwa Spika, eneo la Mkungunero lina mgogoro kwa upande wa Kondoa, lina mgogoro kwa upande wa Kiteto, lina mgogoro kwa upande unaotazama Wilaya ya Simanjiro na hili linahitaji kupatiwa ufumbuzi.

Mfano wake mwingine pia ni migogoro iliyoko katika Mkoa wa Kagera ambako kwa kweli niwaelezeni, kuna baadhi ya mifugo inaingia kutoka Uganda, Rwanda na Burundi, lakini inaingia katika mashamba ambayo yalitolewa kwa baadhi ya Watanzania kama *ranches* ambapo badala ya wao kufuga mifugo, wanakodisha maeneo hayo kwa wageni kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mapori yetu ya Kimisi ambayo yako huko huko Mkoa wa Kagera ambapo huko nyuma yalikuwa yanatumika kwa ufugaji. Hivi sasa yanahifadhiwa na wakati mwingine tumeweka pale kwa ajili ya masuala ya kawaida ya usalama. Nataka kusema kwamba uhifadhi ni muhimu sana lakini kuna haja ya

kuangalia pia kilio cha wananchi na wafugaji wa Kagera katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba huko Kagera kuna Watanzania wa asili ya Kitusi ambao wanaishi pale na ambao wana haki kama Watanzania wengine. Wengine walipewa vyeti vya uraia na wakaendelea kuwa na watoto wao katika maeneo hayo, wanafanana na wale wanaotoka Rwanda, wanafanana na wengine wanaotoka Uganda, wanafanana na wengine wanaotoka Burundi, lakini ni vizuri wakati wa kufanya *operations* hizi tukajua kwamba sio kila Mtusi aliyeko pale ni Mnyarwanda. Sio kila Mtusi aliyeko pale anatoka Burundi.

Kuna wengine wenye asili ya Kitusi wako Kagera kama ambavyo sisi Wamasai tulioko Simanjiro, kuna Wamasai wengine walioko Kaijado huko Kenya wako pia wenzangu hawa Wachaga wengine wako huko na wengine wako mpakani kule lakini sina hakika labda kama wameenda kama wako wengi, nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Mbatia anaonyesha onyesha hapo nikasema labda pengine kuna watu wenye asili ya kichaga walioko Tanzania na wengine walioko Kenya. Sasa sijui huko Kenya wanaitwa nani?

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaangalia tu ili tusije tukaanza kuwazoa watu na kuwafukuza bila kuwa na uhakika, ili tusije tukawafukuza Watanzania wenzetu, lakini pia wale wenye vibali vya kuishi nchini tukaweza kuwatambua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nitaomba tu unisaidie kuniongoza maana kuna maazimio yale ambayo ninayo hapa kama itabidi yasomwe baadaye au itabidi nipate maelekezo yako juu ya hatua zinazostahili katika hatua hii.

Kikubwa zaidi ambacho napenda kusema Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu siyo rahisi kujibu hoja ya kila Mbunge mmoja mmoja, baada ya kauli ya Waziri Mkuu

kwamba mapendekezo yetu yote yatakayokuwa yametolewa hapa yatafanyiwa kazi na Serikali, ni imani yangu kwamba maeneo ya kufugia yatatengwa, maeneo ya kilimo yatatengwa, fedha kwa ajili ya sekta hizi mbili zitatengwa ili kuhakikisha kwamba tunamaliza mgogoro huu *once and for all*.

Mheshimiwa Spika, kubwa kuliko yote lengo la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni ustawi wa Watanzania na kwamba ustawi wa Watanzania hauwezi kuja kama tumefarakana, kama tunachoma mazao ya wakulima au tunalisha mifugo kwenye mashamba ya wakulima au tunapiga mifugo risasi au tunawafukuza wafugaji wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli namwomba Waziri Mkuu, yaliyokuwa yakiendelea Kilosa, Mvomero na Morogoro Vijijini ambapo Viongozi wa Halmashauri wanasema hamisha mifugo nje ya mipaka ya Wilaya yangu, ni vizuri sasa tukafika mahali mfugaji yeyote aliyeko mahali popote aliko katika nchi hii ahakikishe kwamba anapewa hifadhi na eneo la kuishi na mifugo yake.

Mheshimiwa Spika, mkulima yeyote mahali popote alipo katika nchi hii atengewe eneo la kilimo bila kuulizana wewe ni kabila gani au dini gani? Tukibaguana kwa misingi hiyo, nchi hii haitakalika na Tanzania itakuwa imesambaratika.

Mheshimiwa Spika, nimemaliza hoja yangu, nasubiri maelekezo yako kama…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA - MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Ahsante sana. Hii hoja ni ya Kamati Teule, kwa hiyo, haihitaji hayo mengine yote. Ahsante Mheshimiwa umemaliza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ni lazima muwapigie makofi mkitaka. Maana naona mnapiga kama mna wasiwasi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, makusudi ya kuundwa kwa hii Kamati Teule ilikuwa ni kule kuzagaa kwa hofu, taabu, malalamiko na ukosefu wa amani kwa Watanzania wa aina mbalimbali.

Kwa hiyo, sisi kama Bunge tulitaka tujihusishe na mazingira hayo na tujue ni nini tunataka kuiambia Serikali. Kama walivyosema wenyewe hawa, hawakwenda kila Kijiji au Wilaya, isingewezekana, lakini wameyapata yale mambo ya muhimu kabisa ambayo ni sababu moja au nyingine ya kusababisha matatizo haya na mapendekezo yao yafanyiwe kazi. Nasema hivyo kwa sababu nimekuta kuna watu wameleta marekebisho. Hii taarifa ni *very broad in nature*. Ikishakuwa *broad in nature* ukianza kusema unafanya *amendment* unakuwa sijui una-*amend* kitu gani, ni sawasawa kama unataka kudonoa sijui kitu gani.

Kubwa hapa tunataka Serikali ifanye hayo yaliyostahili ili wakulima waishi kwa amani, wafugaji waishi kwa amani na haya makundi mengine yaishi kwa amani. Hilo ndilo kubwa na ndiyo maana Kamati haikujihusisha sana kusema afukuzwe nani au nani, maana migogoro hii haijaanza jana wala nini ni ya muda mrefu.

Sasa mnachokitaka, Serikali ianze kuji-*address;* nayo *is not business as usual*, kwa sababu tukienda *business as usual* katika kipindi hiki, itakuwa tatizo kabisa! *(Makofi)*

Kama walivyosema wengine hapa watu wanaongezeka kuzaliwa, hawajui wakakae wapi mwishoni itakuwa ni shida kubwa.

Kwa hiyo, marekebisho kwa kweli siyapokei, kwa sababu ni sawa sawa mtu unaamua kutibua tu, unataka kuihamisha bahari iende wapi, huwezi. Hili suala Waziri Mkuu ni kubwa sana na linachelea uhai wa nchi hii. Naamini kabisa mliyosema mtayafanyia kazi tena kwa nguvu sana. Kuna mmoja hapa amesema habari ya MKURABITA, MKURABITA ilikuwa ni sehemu ndogo tu ya kufundisha Halmashauri iweze namna ya kupima ardhi yote. Hata hivyo, kwa namna moja au nyingine Halmashauri hazijapima ardhi na tusipofanya hivi hakika tunakokwenda wala sio miaka mingi kuanzia sasa, itakuwa tatizo.

Waheshimiwa Wabunge, mnajua kabisa leo wengine nimewaudhi na wengine mmeandika barua za kuniudhi na mimi, lakini hakuna namna siwezi kuwapa nafasi wote lazima tufike mahali tumalize na huu ndio wakati, lakini mliozungumza mmetuwakilisha tulio wengi. Mmezungumza vizuri sana kwa kweli, angalau kila mtu amejisikia vile anavyoona eneo lake lilivyofanyiwa. Hii siyo tu taarifa hii ya Kamati mtakayofanyia kazi na *Hansard* zetu tutawaletea na *Hansard* zilizozungumzwa na Bunge hapa nazo pia tutawapeni mzifanyie kazi, kwa sababu kuna utajiri mwingi Wabunge wamesema hapa, ambao pengine humu haupo, lakini *Hansard* zetu ni sehemu ya *official documents.*

Kwa hiyo si tu taarifa ya Tume Teule iliyoandikwa na *Hansard* zetu tutakuletea baada ya muda mfupi tu ukimaliza hapa tutakuletea sisi *Hansard* zote. Mtakuta mle utajiri mwingi wa Waheshimiwa Wabunge waliouweka mle ndani uweze kutusaidia kwenda mbele, kubwa tulete amani. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo nawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa Kuchunguza Sababu za Migogoro baina ya Wakulima, Wafugaji, Wawekezaji na Watumiaji Wengine wa Ardhi Nchini Ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Wote wameafiki tunataka Mheshimiwa Waziri Mkuu uweze kulifanyia kazi. Niipongeze Kamati na Wajumbe wake. Ile Kamati ilinipa tatizo sana, unajua Kamati Teule Wajumbe wake *maximum five*, yaani ilinipa shida hata kuongeza, sina madaraka ya kuongeza tulisema watano. Baada ya kuangalia ukubwa nikasema tulifanya kosa, watano tu ndio wazunguke nchi nzima na matatizo makubwa yale.

Kwa hiyo, tunadhani baadaye tutajifunza aina fulani ya Kamati Teule itabidi tuiweke tofauti na zile ambazo ni *investigative* kama ile ya *Audit*. Ile ni ndogo, inakwenda ndani, lakini hii kwa kweli wamefanya kazi kwa shida sana. Wamefanya kwa shida na nawashukuru sana na nawapongeze sana na ripoti yenu ni nzuri. Ahsante sana. *(Makofi*

**KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tumekuwepo hapa kwa takriban siku 12 katika shughuli za Mkutano wa 18 wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye ame tufikisha salama siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, tumekutana hapa tukiwa tumeshuhudia mabadiliko katika Baraza la Mawaziri na Wenyeviti wa baadhi ya Kamati za Kudumu za Bunge. Hivyo, niruhusu nitumie nafasi hii ya awali kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote ambao wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika mabadiliko hayo. Aidha, napenda niwapongeze Wenyeviti watatu pamoja na Makamu mmoja kwa kuchaguliwa kuongoza Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo Kamati ya Bajeti, Kamati ya Nishati na Madini na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Tunawatakia afya njema Mawaziri, Naibu Mawaziri na Wenyeviti wote katika kutekeleza majukumu yao mapya.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipomaliza Mkutano wa 16 na 17 wa Bunge lako Tukufu, kumetokea majanga katika

sehemu mbalimbali ya nchi ikiwemo mafuriko na mapigano ya Wakulima na Wafugaji kule Morogoro, pamoja na ajali za barabarani. Naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wote walioathirika na majanga, maafa na ajali za barabarani. Kwa wale waliopoteza maisha tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi Amina.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya kawaida na yale ya papo papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Jumla ya maswali 122 ya msingi na 313 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Aidha, Maswali 15 ya msingi na 13 ya nyongeza yaliulizwa na kujibiwa kwa utaratibu wa maswali ya papo kwa papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tunahitimisha Mkutano huu tukiwa tumekamilisha kazi kubwa ya kusoma na kujadili taarifa mbalimbali za Kamati za Bunge za Kisekta na zisizo za Kisekta. Kamati za Kisekta ambazo Taarifa zake zimewasilishwa na kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge ni:-

(i) Kamati ya Miundombinu;

(ii) Kamati ya Nishati na Madini;

(iii) Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira;

(iv) Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji;

(v) Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala;

(vi) Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;

(vii) Kamati ya Masuala ya UKIMWI;

(viii) Kamati ya Ulinzi na Usalama;

(ix) Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa;

(x) Kamati ya Huduma za Jamii; na

(xi) Kamati ya Maendeleo ya Jamii.

Aidha, Bunge Lako Tukufu lilipokea na kujadili Taarifa za Kamati zisizo za Kisekta zinazosimamia Fedha za Umma zifuatazo:

(i) Kamati ya Hesabu za Serikali;

(ii) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa; na

(iii) Kamati za Bajeti.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tumepokea na kujadili taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya Wakulima, Wafugaji Wawekezaji na Watumiaji wengine na Ardhi Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, tulipanga na tulitarajia kujadili Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi wa mwaka 2014 (*The Tax Administration Bill. 2014*); Muswada wa Sheria ya Takwimu wa mwaka 2013 (*The Statistics Bill, 2013);* na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali (Na. 2) wa mwaka 2014, *(The Written Laws Miscellaneous Amendments (No. 2) Bill, 2014)* ambao ndio pia ulihusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kiislamu, Sura 375 (*The Islamic Law (Restatement) Act)* unaotambua Mahakama ya Kadhi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Miswada hii haikuweza kuijadili katika Mkutano huu, ili kutoa nafasi kwa Kamati husika zweze kupata nafasi na muda wa kupitia na kutoa ushauri kwa Bunge lako Tukufu na pia kwa upande wa Serikali kupata muda vile vile wa kuzidi kuyatazama maeneo mbalimbali ambayo yamewekewa au yametolewa maelezo katika Kamati mbalimbali kwa ajili ya kuboresha Miswada hiyo. Matumaini yangu ni kwamba Miswada hiyo itapata nafasi katika Bunge lako lijalo la 19.

Pamoja na shughuli zilizopangwa katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata pia fursa ya kupokea na kujadili Hoja ya Mheshimiwa James Mbatia kuhusu kukamatwa na Polisi kwa Mwenyekiti wa Chama cha *CUF* Profesa Ibrahim Lipumba kutokana na maandamano ya Wafuasi wa Chama hicho yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam kiyume cha Sheria. Aidha, Serikali kupitia Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ilipata nafasi ya kutoa kauli ya Serikali kuhusu kutatua changamoto za soko la Sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa. Napenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge, maoni na mapendekezo ya Kamati zote kwa ujumla yatazingatiwa na Serikali kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini kwa ujumla imeendelea kuwa ya kuridhisha katika maeneo mengi kufuatia mavuno mazuri katika msimu wa kilimo wa 2013/2014. Tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini hadi mwezi Septemba, 2014 inaonesha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2013/2014 ulifikia jumla ya Tani Milioni 16.0 zikiwemo Tani Milioni 9.8 za mazao ya nafaka na Tani Milioni 6.2 za mazao yasiyo ya nafaka.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, makadirio ya mahitaji ya chakula Nchini kwa mwaka 2014/2015 zilionesha kuwa tunahitaji Tani Milioni 12.8. Hivyo, kutokana na uzalishaji huu, nchi ina ziada ya Tani Milioni 3.2 za chakula na tumewezesha kujitosheleza kwa chakula kwa asilimia 125. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Wananchi na hasa wakulima wote nchini kwa kuitikia wito wa Serikali wa Mpango wa "Kilimo Kwanza" na kuongeza tija katika uzalishaji, ambao umetuwezesha kupata mavuno mengi na kupata ziada hii ya chakula. Serikali itaendelea kuweka juhudi zaidi katika uzalishaji wa mazao ya Chakula ili kulihakikishia Taifa letu kuondokana na njaa na aibu ya kuomba chakula kutoka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tathmini hii pia imeonesha kuwa, uzalishaji wa nafaka kwa ujumla umeongezeka kutoka Tani Milioni 7.6 msimu wa 2012/2013 hadi Tani Milioni 9.8 msimu wa 2013/2014. Kati ya Tani hizo Milioni 9.8, Tani Milioni 6.7 ni za mahindi, Tani Milioni 1.7 ni za mchele na Tani Milioni 1.4 mtama. Kutokana na mahitaji ya nafaka kwa msimu wa 2014/ 2015 kuwa Tani Milioni 8.1; Taifa lina ziada ya Tani Milioni 1.4 za nafaka. Uzalishaji wa mahindi ambayo ni chakula kikuu umeongezeka kutoka Tani Milioni 5.2 katika msimu wa 2012/ 2013 hadi kufikia Tani Milioni 6.7 katika msimu wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahitaji ya mahindi kwa mwaka 2014/2015 kukadiriwa kuwa Tani Milioni 5.2, Taifa lina ziada ya Tani Milioni 1.5 za Mahindi sawa na Asilimia 29.7. Vile vile, uzalishaji wa mchele umeongezeka kutoka Tani Milioni 1.3 msimu wa 2012/2013 hadi Tani Milioni 1.7 katika msimu wa 2013/2014. Kwa vile makadirio ya mahitaji ya mchele kwa mwaka 2014/2015 ni Tani 900,000, Taifa lina ziada ya Tani 800,000 za mchele, sawa na asilimia 89.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa *(NFRA)* walianza ununuzi wa nafaka katika msimu wa 2014/2015 wakiwa na akiba ya chakula ya Tani 189,493.7. Hadi kufikia tarehe 29 Januari, 2015 Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa ilikuwa imeshanunua jumla ya Tani 298,122.3 za nafaka sawa na asilimia 107.2 ya lengo la ununuzi. Aidha, kiasi cha chakula kilichochukuliwa katika maghala hadi tarehe 29 Januari, 2015 kilikuwa Tani 29,290.5, jumla ya Tani 1,117.5 ziko njiani kutoka vituo vya Vijijini kwenda katika maghala ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa katika Kanda mbalimbali. Hivyo, hadi tarehe 29 Januari, 2015, akiba ya chakula katika maghala ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa ilikuwa Tani 460,175.5 zikiwepo Tani 451,589.1 za mahindi; Tani 3,939.6 za mpunga; na Tani 4,646.8 za mtama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mvua nzuri zilizonyesha katika msimu wa 2013/2014, ongezeko hili la uzalishaji wa chakula, limechangiwa na juhudi za Serikali za kuhimiza Wananchi kuongeza matumizi ya zana kubwa za kilimo (matrekta makubwa) pamoja na kutoa pembejeo za ruzuku

kwa wakulima. Aidha, bei nzuri ya kununulia mahindi ya Shilingi 500 kwa kilo iliyotumiwa na Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa iliwavutia wakulima wengi kupeleka mahindi yao katika vituo vya ununuzi vya Wakala, jambo lililowafanya Wakala kushindwa kununua nafaka za ziada kutoka kwa wakulima na hivyo kusababisha kuwepo kwa malalamiko mengi kutoka kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 11 Novemba, 2014, uwezo wa Wakala wa kuhifadhi nafaka katika maghala yake ulikuwa ni Tani 246,000 tu, hivyo kutokana na akiba kubwa iliyopo sasa ya Tani 460,175.5, imewalazimu Wakala kuhifadhi sehemu ya akiba hiyo katika maghala mengine Vijijini, katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi; na nje ya maghala ya Wakala kwa kufunikwa na maturubai.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mahitaji ya hifadhi Kitaifa kwa kipindi cha muda mfupi ni tani 400,000; kwa kipindi cha muda wa kati ni tani 700,000; na tani 1,000,000 kwa kipindi cha muda mrefu.

Katika jitihada za kukabiliana na changamoto ya upatikanaji wa maghala ya kutosha ya kuhifadhi nafaka katika maghala ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa, Serikali imeandaa mpango maalum unaotarajiwa kugharimu takriban Shilingi Bilioni 212 wa kuongeza uwezo wa Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa wa kuhifadhi nafaka hadi kufikia Tani 400,000 ifikapo mwaka 2015/2016. Chini ya mpango huo, Serikali itajenga maghala au vihenge vya kisasa *(Silos)* katika maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa nafaka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuwepo kwa changamoto ya ujenzi wa *Silos*, nilipokuwa Nchini Poland mwezi Oktoba 2014 nilipata fursa ya kukutana na Viongozi wa Serikali ya Poland pamoja na kutembelea Kampuni ya *Mtynpol* inayohusika na ujenzi wa *Silos*, kuhifadhi na kusindika nafaka kwa kutumia teknolojia za kisasa. Nilitumia fursa hiyo, kumwomba Makamu wa Rais wa Chama cha

Wafanyabiashara cha Poland, Bwana Witold Karczewski ambaye pia ndiye Mwekezaji wa Maghala (*Silos*) na Viwanda vya Usindikaji Nchini Poland kutembelea Tanzania ili kuona uwezekano wa kujenga *Silos* zitakazotumia teknolojia inayoendana na mazingira ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tarehe 4 hadi 5 Oktoba, 2014; Bwana Witold alifika hapa nchini na kwa pamoja tulitembelea maghala ya Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa yaliyopo Kizota – Dodoma. Baada ya ziara hiyo, mwezi Novemba, 2014 Serikali ya Tanzania imewasilisha maombi ya kupata Mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Poland.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa tayari Serikali ya Poland imepokea na kuyapitia maombi yetu; na mwishoni mwa mwezi huu wa Februari, 2015; Wizara ya Fedha inatarajia kukamilisha mazungumzo ya kupata mkopo huo wa masharti nafuu. Ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa mradi huo utaanza mapema mwaka huu baada ya Serikali ya Poland kuridhia maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2003/2004 hadi mwaka 2007/2008, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kama fidia za gharama za usafiri ili pembejeo hizo ziuzwe kwa bei moja nchi nzima. Kutokana na changamoto mbalimbali za kiutendaji, Mfumo huo ulibadilishwa na kuanzisha utaratibu wa kutumia Vocha kati ya mwaka 2008/2009 hadi msimu wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, mpango huo katika kipindi hiki cha miaka kumi umewezesha uzalishaji wa mazao ya chakula kuongezeka kutoka Tani Milioni 7.7 mwaka 2003/2004 hadi kufikia Tani Milioni 16 mwaka 2013/2014. Ongezeko hili limechangia ongezeko la viwango vya utoshelevu wa chakula nchini kutoka asilimia 88 mwaka 2003/2004 hadi kufikia asilimia 125 mwaka 2013/2014. Aidha, uzalishaji wa zao la mahindi umeongezeka kutoka Tani Milioni 3.2 mwaka 2003/2004 hadi Tani Milioni 6.7 mwaka 2013/2014. Uzalishaji wa mchele umeongezeka kutoka Tani 600,000 mwaka 2003/2004 hadi Tani Milioni 1.7 mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la uzalishaji wa mazao hayo pamoja na sababu nyingine limechangiwa na ongezeko la matumizi ya pembejeo zilizotokana na mpango wa ruzuku. Pamoja na mafanikio ya mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kupitia utaratibu wa Vocha, pamekuwepo na changamoto katika ngazi mbalimbali za utekelezaji, ikiwemo ubadhirifu, upotevu wa Vocha na ucheleweshaji wa Vocha, hali iliyosababisha wakulima wengi kushindwa kupata pembejeo kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto zilizopo katika Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo kwa kutumia vocha na katika jitihada za kutekeleza azma ya kuwapelekea wakulima pembejeo kwa ufanisi zaidi, Serikali katika msimu wa 2014/2015 imebuni utaratibu mpya wa majaribio ambao lengo lake ni kuviwezesha vikundi na Vyama vya Ushirika kuchukua mikopo ya pembejeo za kilimo kutoka Taasisi za fedha na vikundi vya wakulima, VICOBA na Vyama vya Ushirika moja kwa moja kutoka katika Makampuni ya Pembejeo.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Kaya 946,000 zinatarajiwa kunufaika na Mpango wa Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo kutoka Taasisi za Fedha na Makampuni ya pembejeo. Hadi sasa *AMCOS* 247 katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Mbeya (Chunya) Katavi, Singida, Iringa na Shinyanga zimepata mikopo ya pembejeo ya jumla ya Shilingi 74,737,708 kupitia Benki za *CRDB*. Benki ya *NMB* imetoa mikopo kwa vikundi sita (6) vinavyojishughulisha na kilimo cha mpunga yenye thamani ya Shilingi Milioni 600. Kupitia Benki za Wananchi, vikundi vya wakulima 147 katika Wilaya za Mbinga, Njombe, Mufindi, Kagera na Tandahimba vyenye wanachama 3,242 vilipata mikopo ya pembejeo yenye thamani ya Shilingi Milioni 844.4.

Kwa vile Halmashauri za Wilaya zitahusika moja kwa moja katika suala la usimamizi wa mpango huu na kwa vile Kamati za pembejeo za Wilaya zitakuwa chini ya usimamizi wa Mkuu wa Wilaya, nawaagiza Viongozi wa Mikoa na Wilaya kusimamia kwa karibu zoezi la kuhamasisha vikundi kuchukua mikopo katika Taasisi za fedha na vyombo vingine

na kuhakikisha kuwa usambazaji wa pembejeo hizi unafanyika ipasavyo ili tuongeze idadi ya wanufaika wa mfumo huu na kuufanya kuleta mafanikio yaliyotarajiwa kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Wakala wa Hifadhi ya Chakula wa Taifa ilikuwa na kazi kubwa ya kununua nafaka kutoka kwa wakulima; vikundi vya wakulima na wafanyabiashara. Kutokana na wakulima kupewa bei nzuri na kutokana na wakulima kwa hiyari yao kuomba mazao yao yanunuliwe na Wakala kwa mkopo kuepuka kuharibika, wakulima walifika kwa wingi katika vituo vya mauzo tofauti na kiasi cha fedha ambacho Wakala walikuwa wametenga kwa ununuzi, hivyo kuliwasababishia wakulima adha kubwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Desemba, 2014 Serikali ilikuwa inadaiwa kiasi cha Shilingi Bilioni 89 za wakulima waliouzia Wakala mahindi. Aidha, hadi kufikia tarehe 29 Januari, 2015, Serikali ilikuwa imelipa wakulima hao kiasi cha Shilingi Bilioni 15 na kubakiza deni la Shilingi Bilioni 74. Katika juhudi za Serikali za kutatua changamoto ya deni hili, Mwezi Februari 2015 Serikali inategemea kulipa kiasi cha Shilingi Bilioni 40 na kubakia na deni la Shilingi Bilioni 34 ambazo tunategemea zitalipwa kutokana na mkopo wa *CRDB* wa Shilingi Bilioni 15 na Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali pia imepanga kuuza kiasi cha Tani 175,000 kutoka katika akiba yake ya chakula kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani *(WFP)* na wafanyabishara. Nichukue fursa hii kuwapa pole wakulima wanaoidai Serikali kwa usumbufu wanaoupata. Hata hivyo, napenda kuwahakikishia kuwa wote watalipwa stahili zao katika kipindi kifupi kijacho.

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto tulizonazo katika kipindi hiki kwenye Sekta ya Elimu ni pamoja na suala la madawati katika Shule za Msingi na Sekondari nchini. Taarifa nilizo nazo ni kuwa, hadi sasa mahitaji yetu kama Nchi ni madawati milioni 3.3 kwa Shule za Msingi, na tayari

tunayo madawati milioni 2.1 sawa na asilimia 63 ya mahitaji. Kwa maana hiyo, tuna upungufu wa madawati milioni 1.2 sawa na Asilimia 37. Kwa upande wa Shule za Sekondari tunayo madawati milioni 1.4 kati ya madawati 1.5 yanayohitajika au asilimia 92 ya mahitaji. Kuna upungufu wa madawati takriban 120,000 sawa na asilimia nane ya mahitaji. Upungufu huo ni kwa idadi ya wanafunzi walioko Shule za Msingi na Sekondari kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, wakati tunazungumzia upungufu huo wa madawati idadi ya wanafunzi wa Shule ya Msingi na Sekondari inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kadiri idadi ya watu inavyoongezeka. Hivyo, kasi yetu ya kuondoa upungufu wa madawati inatakiwa kuwa kubwa kuliko kasi ya ongezeko la wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari kwa mwaka. Ni jukumu letu wote Serikali, Sekta Binafsi pamoja na wananchi kwa ujumla kuondoa upungufu huo hususan katika Shule za Msingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuondoa tatizo hili la madawati. Hatua hizo ni pamoja na kupeleka fedha za ununuzi wa madawati kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye Serikali za Mitaa. Aidha, kiasi cha Shilingi Bilioni 12.3 zilizotokana na fedha za fidia ya Rada zilielekezwa kwenye Halmashauri kwa ajili ya kununulia madawati.

Hadi sasa madawati ya plastiki 30,996 yameshasambazwa nchini. Usambazaji wa madawati 61,468 ya mbao utaanza hivi karibuni. Vile vile, Serikali imekamilisha mikataba ya kusambaza madawati mengine ya plastiki 75,699. Tunatarajia kuwa fedha hizo za Rada zitapunguza uhaba wa madawati kwa asilimia 5.1. Katika mwaka 2014/2015, kiasi cha Shilingi Bilioni 1.1 kimetengwa na Halmashauri kwa ajili ya kununua madawati 152,000.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikiana na Taasisi za Umma, Wahisani, Sekta Binafsi na mwananchi mmoja mmoja katika kupunguza uhaba madawati nchini, Nitumie nafasi hii kuwashukuru, wote ambao wamekuwa

wakichangia Sekta ya Elimu hasa katika tatizo hili la upungufu wa madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa kwenye ziara Mkoani Singida mwaka 2012 alielekeza kila Shule ya Sekondari nchini iwe ina vyumba vitatu vya maabara ifikapo tarehe 30 Novemba, 2014.

Tangu wakati huo hadi sasa Viongozi wa Serikali Mitaa na Tawala za Mikoa wamekuwa wakitekeleza maelekezo hayo. Hali ya ujenzi wa vyumba vya maabara nchini inaonesha kuwa hadi mwezi Desemba, 2014 vyumba 3,607 sawa na Asilimia 34 ya mahitaji ya vyumba 10,653 vya maabara nchini vilikuwa vimejengwa. Aidha, vyumba 6,249 sawa na asilimia 59 ya mahitaji vilikuwa vinaendelea kujengwa na asilimia saba bado vilikuwa havijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa uliofanya vizuri katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais hadi kufikia Desemba 2014 ni Mkoa wa Njombe ambao ulifanikiwa kukamilisha ujenzi wa vyumba vya maabara kwa asilimia 96 ya shule za sekondari zilizopo mkoani humo. Mkoa wa Ruvuma nao ulikamilisha ujenzi kwa asilimia 81, ukiwa ni Mkoa wa pili Kitaifa. Napenda kutumia fursa hii kuipongeza Mikoa hii miwili kwa kutekeleza vizuri maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Imeonesha mfano mzuri katika kutekeleza maelekezo ya Kiongozi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika zoezi hili Mkoa wa Morogoro ulikuwa Mkoa wa tatu ambao ulijitahidi kujenga vyumba vya madarasa kwa kufikia kwa asilimia 53 ya mahitaji. Mikoa 22 iliyobaki haikuweza kufikia asilimia 50 ya lengo kwa kipindi chote cha mwaka 2012 – 2014. Kati ya Mikoa hiyo ambayo haikuweza kufika hata robo ya lengo (asilimia 25) katika kipindi tajwa cha takribani miaka mitatu ni Mikoa sita; nayo ni Mtwara (asilimia 21), Lindi (asilimia 20), Tabora (asilimia 17), Dodoma (asilimia 12), Rukwa (asilimia 11) na Kigoma (asilimia 10). Tunaweza kusema hii ndiyo Mikoa ya mwisho

katika kutekeleza agizo la Rais. Mikoa 16 ambayo sikuitaja hapa iko katika kundi la asilimia kati ya 26 hadi 49. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais katika hotuba yake kwa wananchi ya tarehe 31 Desemba, 2014 aliongeza miezi sita zaidi hadi Juni, 2015 kwa wale ambao hawajakamilisha ujenzi wa maabara hizo ili waweze kukamilisha. Ni matarajio ya Mheshimiwa Rais kuwa muda huo unatosha kwa kila Sekondari iliyopo nchini kuwa na vyumba vitatu vya maabara na aliweka bayana kuwa hakusudii kuongeza tena muda baada ya muda huo kupita yaani Juni, 2014.

Mheshimiwa Spika, hivyo, nawataka Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mameya, Wenyeviti na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya na Miji kuhakikisha maagizo haya yanatekelezwa. Aidha, natoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kutoa msukumo stahiki katika utekelezaji wa maagizo haya kwa maslahi ya Taifa letu.

Kwa upande wa Serikali, Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI haina budi kuhakikisha agizo hili la Mheshimiwa Rais linatekelezwa ndani ya muda uliotolewa. Aidha, katika kufanya hivyo wahakikishe kuwa vyumba vya maabara vinavyojengwa vina ubora stahiki na vinalingana na thamani ya fedha zilizotumika. Ubadhirifu wa aina yoyote usipewe nafasi na watakaobainika kuhusika wachukuliwe hatua za kisheria mapema. Nitapenda Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI waendelee kufuatilia suala hili na kunipa taarifa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuimarisha na kuongeza kiwango cha huduma za upatikanaji wa Nishati ya Umeme Vijijini ili kujenga msingi wa uchumi imara na wa kisasa wa Taifa linalojitegemea. Moja ya hatua zinazochukuliwa ni utekelezaji wa Mpango Kabambe wa usambazaji umeme Vijijini.

Mheshimiwa Spika,Ili kufikia azma hiyo, Wakala wa Nishati Vijijini umeanza kutekeleza Mradi Kabambe wa Awamu ya Pili unaohusisha usambazaji wa umeme Vijijini katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Mradi huu unahusisha ujenzi wa Vituo sita vya kupoozea umeme na njia ya kusambaza umeme kwenye maeneo yenye msongo wa *33kV* yenye urefu wa Kilomita 15,000.

Mheshimiwa Spika, vile vile, utahusisha ujenzi wa njia za kusambaza umeme yenye msongo wa *kilo-Volti* 400 zenye urefu wa kilomita 8,000 na ufungaji wa Vipooza Umeme 3,300. Mradi huu utakapokamilika utakuwa umeunganisha wateja wa awali takriban 250,000 katika Vijiji 1,142. Mradi huu unafuatia baada ya kukamilika kwa zaidi ya asilimia 80 ya Mradi Kabambe wa Awamu ya Kwanza ambapo Wateja 17,688 wameunganishwa kwenye miundombinu ya usambazaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, Mradi Kabambe wa Awamu ya Pili unakadiriwa kugharimu Shilingi Bilioni 881. Hadi sasa takriban Shilingi Bilioni 278 zimelipwa kwa Wakandarasi ikiwa ni malipo ya awali ya asilimia 10 na gharama za kununua vifaa na hati za dhamana zenye jumla ya Shilingi Bilioni 439 kwa Miradi yote 35 zimefunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na juhudi za Serikali za kuongeza kasi ya kuunganisha umeme Vijijini ambazo zimechochewa na kupunguza gharama za kuunganisha umeme kwa wananchi hasa waishio Vijijini idadi ya Watanzania waliounganishiwa umeme imeongezeka kutoka Asilimia 2.5 kwa mwaka 2007 hadi Asilimia 18.4 kwa Mwaka 2010 na kufikia Asilimia 24 kwa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2013 Serikali ilianza kutekeleza Mradi wa ujenzi wa Bomba la Gesi kutoka Mtwara na mitambo ya kuchakata na kusafisha gesi unaendelea vizuri. Mpaka kufikia mwezi Oktoba, 2014 ujenzi wa bomba ulikuwa umefikia asilimia 94 na ule wa mitambo ulikuwa umefikia Asilimia 84. Kwa wastani mradi mzima sasa

umekamilika kwa asilimia 92. Matarajio ni kumalizika kwa ufungaji wa mitambo yote na kuanza majaribio ya awali. Mara majaribio yote ya miundombinu yatakapokamilika, miundombinu hii itakabidhiwa kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* kwa uendeshaji. Zoezi hilo linatarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, ili kujiandaa kunufaika na upatikanaji wa Gesi Asilia, *TPDC* imeanzisha Kampuni yake Tanzu *(GASCO)* ambayo imepewa majukumu yote ya kumiliki miundombinu yote ya usafishaji, usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia hapa nchini pamoja na kukusanya gesi kutoka vyanzo mbalimbali. Ili kufanikisha azma hii ya Serikali, tayari *GASCO* kupitia *TPDC* imeajiri Wafanyakazi wapya wapatao 120 kwa ajili ya mitambo ya kusafisha gesi na wengine 50 kwa ajili ya kuendesha bomba la gesi.

Mheshimiwa Spika, manufaa mengine yatakayopatikana kutokana na upatikanaji wa gesi asilia ni kupata umeme wa uhakika na matumizi viwandani, magari na majumbani. Aidha, nchi itaokoa Dola za Marekani bilioni moja (sawa na Shilingi za Tanzania Trilioni 1.6) kwa mwaka kutokana na mitambo iliyopo nchini kutumia gesi asilia badala ya mafuta. Faida nyingine za mradi mpya ni pamoja na ajira katika mitambo itakayojengwa Madimba na Songo Songo kwani kila mtambo utahitaji wastani wa wafanyakazi 60. Pia, mradi utatoa ajira katika Sekta zote na hususan za Afya, Elimu, Maji, Usafiri pamoja na huduma nyingine za Kijamii zitakazohitajika katika maeneo husika. Natoa wito kwa Wananchi wote kulinda miundombinu ya gesi asilia ambayo inajengwa kwa gharama kubwa. Aidha, nawahimiza Wakandarasi wa Mradi wa Bomba la Gesi kukamilisha ujenzi kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa uliofanyika nchini tarehe14 Desemba 2014 ulihusisha uchaguzi wa Wenyeviti wa Vijiji 12,261, Wenyeviti wa Vitongoji 63,319, Wenyeviti wa Mitaa Mijini 3,884, Wajumbe wa Serikali za Vijiji/Mitaa na Wajumbe wa Viti Maalum. Jumla ya watu 8,137,974 sawa na asilimia 69 ya watu waliojiandikisha kupiga

kura walijitokeza kupiga kura. Vyama vya Siasa 17 sawa na asilimia 81 ya Vyama vyote vyenye usajili wa kudumu vilishiriki kwenye uchaguzi huu.

Taarifa ya matokeo inaonesha kwamba katika nafasi ya Wenyeviti wa Vijiji, CCM kilishinda kwa asilimia 79.4, CHADEMA asilimia 15.1 na *CUF* asilimia 4.6. Vyama vingine kwa ujumla vilipata asilimia 0.9. Matokeo ya Wenyeviti wa Vitongoji yanaonesha kuwa CCM imeshinda kwa asilimia 79.3, CHADEMA asilimia 15.6, *CUF* asilimia 4.3 na vyama vingine vilipata asilimia 0.8. Nafasi za Wenyeviti wa Mitaa CCM kilishinda kwa asilimia 66.5, CHADEMA asilimia 25.4, *CUF* asilimia 6.8 na vyama vingine vilipata kwa asilimia 1.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya Wajumbe wa Serikali za Vijiji/Mitaa ni kuwa CCM ilipata asilimia 79.3, CHADEMA asilimia 15.7, *CUF* asilimia 4.3 na Vyama vingine vilipata asilimia 0.7. Kuhusu matokeo ya Wajumbe wa Viti Maalum ni kuwa CCM walipata asilimia 82.1, CHADEMA asilimia 13.7, *CUF* asilimia 3.5 na Vyama vilivyobaki navyo vilipata asilimia 0.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana wakati wa uchaguzi huo, zipo changamoto zilizojitokeza katika mchakato mzima wa upigaji kura. Hii ni pamoja na kuwepo kwa vurugu siku za uchaguzi, wagombea kufariki au kujitoa, ukosefu wa umakini katika usimamizi na ucheleweshaji wa vifaa vya kupigia kura. Kutokana na kasoro hizo asilimia 1.2 ya maeneo yaliyostahili kupiga kura bado hawajapiga kura. Hata hivyo, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI wamejipanga vizuri kuhakikisha kwamba uchaguzi wa maeneo yaliyobaki na tathmini yake unakamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na baadhi ya Wakurugenzi wa Halmashauri kuonesha udhaifu katika kusimamia uchaguzi huo, Serikali ilichukua hatua ya kutengua uteuzi wa Wakurugenzi sita (6) ambao ni Mkurugenzi wa Mkuranga, Kaliua, Kasulu, Serengeti, Sengerema na Bunda.

Vile vile, wapo Wakurugenzi waliosimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi wa makosa yao wakiwemo Wakurugenzi wa Hanang', Mbulu, Ulanga, Kwimba na Manispaa ya Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, wapo pia, Wakurugenzi waliopewa "ONYO KALI" ambao ni Wakurugenzi wa Rombo, Busega na Muheza. Wakurugenzi waliopewa "ONYO" pekee ni wa Manispaa ya Ilala, Hai na Mvomero. Watumishi wa ngazi za chini pia walichukuliwa hatua na Halmashauri ambazo ni mamlaka zao za nidhamu. Utekelezaji wa hatua hizi utasaidia kupeleka ujumbe kwa wale wote ambao watashindwa kutoa usimamizi thabiti kwenye chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mchakato mzima wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014, naomba uniruhusu nitumie fursa hii kushukuru na kuwapongeza wananchi wote walioshiriki na hivyo kufanikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2014. Nipongeze pia Vyama vyote vya Siasa vilivyojitokeza kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo. Kipekee kabisa niwapongeze Viongozi na Wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa na wa kishindo katika maeneo yote kuanzia nafasi za Vijiji, Vitongoji, Mitaa, Wajumbe wa Serikali za Mitaa/Vijiji na Viti Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 10 Januari, 2015 nilibahatika kuhudhuria katika sherehe ya uwekaji jiwe la msingi katika Shule ya Sekondari ya Kibuteni Mkoa wa Kusini Unguja. Ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Shule ya Sekondari ya Kibuteni ambayo nilikwenda kuiwekea jiwe la msingi pamoja na shule nyingine ya Mkanyageni, Pemba zinajengwa kwa ushirikiano na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* ambapo *BADEA* imetoa mkopo wa Dola za Kimarekani Milioni Sita na Serikali ya Zanzibar imatoa Dola 600,000 ambazo ni asilimia 10 ya gharama zote. Gharama za ujenzi kwa fedha za Kitanzania inatarajiwa kufikia Shilingi Bilioni 3.0.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa shule hiyo ya kisasa ni mwendelezo wa juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya kusukuma maendeleo ya Elimu katika sehemu zote za Zanzibar. Aidha, Shule hii ni miongoni mwa Shule za Sekondari 27 zilizojengwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Saba inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein ambapo Shule 19 zimekamilika na 18 kati ya hizo zimekwishafunguliwa.

Mheshimiwa Spika, chini ya mkopo wa Benki Kuu ya Dunia Shule tatu za Sekondari zimefanyiwa ukarabati mkubwa, kampasi mpya ya Chuo cha Ualimu cha Benjamini William Mkapa huko Pemba imejengwa, madawati na vitabu vya ziada na kiada, vifaa vya maabara na kompyuta vimenunuliwa. Pia, mafunzo ya Ualimu kazini yameendeshwa kwa muda wa miaka mitano. Mradi huo umegharimu Dola Milioni 48 ambapo Dola Milioni 42 zimetolewa na Benki ya Dunia na Dola Milioni sita ni mchango wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, wakati tunaadhimisha miaka 51 ya Mapinduzi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, alieleza mafanikio yaliyopatikana Zanzibar baada ya utekelezaji wa Dira 2020, MKUZA II, Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 na Malengo ya Milenia. Miongoni mwa mafanikio muhimu yaliyopatikana ni kukua kwa uchumi ambapo kuanzia mwaka 2010 hadi 2014 Pato la Taifa limeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 942.3 mwaka 2010 hadi Shilingi Bilioni 1,442.8 mwaka 2013 sawa na asilimia 53.0.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kipindi hicho uchumi wa Zanzibar ulikua kutoka asilimia 6.4 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 7.4 mwaka 2013. Pato la mtu binafsi nalo limeongezeka kwa wastani wa asilimia 38 kutoka Shilingi 778,000 mwaka 2010 na kufikia Shilingi milioni 1.1 mwaka 2013. Kwa mwaka 2014 kasi ya kupanda kwa bei za bidhaa na huduma (Mfumuko wa Bei) ilibaki katika wastani wa tarakimu moja ya Asilimia 5.6, ikilinganishwa na 6.1 kwa mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yanaonekana pia katika ukusanyaji wa mapato ambapo, katika miaka minne 2006/2007 hadi 2009/2010, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikusanya mapato ya Shilingi Bilioni 484, ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 997 zilizokusanywa katika kipindi cha 2010/2011 mpaka 2013/2014. Takwimu hizi zinaonesha ongezeko la asilimia 106.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mazingira ya biashara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi, Zanzibar imeweza kusafirisha bidhaa zenye thamani ya Shilingi Milioni 94,235.8 kwa mwaka 2014 kutoka bidhaa zenye thamani ya Shilingi 87,799.6 kwa mwaka 2013, sawa na ongezeko la asilimia 7.3.

Kwa upande wa Sekta ya Utalii, idadi ya Watalii imeongezeka kutoka Watalii 132,836 mwaka 2010 na kufikia Watalii 274,619 mwaka 2014. Hili ni ongezeko la asilimia 107. Katika elimu idadi ya Shule za maandalizi imeongezeka kutoka Shule 238 mwaka 2010 hadi 279 mwaka 2014, ongezeko hili ni sawa na asilimia 17. Shule za Msingi zimeongezeka kutoka 299 mwaka 2010 hadi 359 mwaka 2014 ongezeko la asilimia 20. Shule za Sekondari zimeongezeka kutoka 194 mwaka 2010 hadi Shule 210 mwaka 2014. Ongezeko hili ni sawa na asilimia nane (8%). Idadi ya Wanafunzi katika Vyuo Vikuu imeongezeka kutoka 3,624 mwaka 2010 hadi 6,038 mwaka 2014. Ongezeko hili nalo ni sawa na asilimia 67.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Afya, idadi ya Wataalam wa Afya imeongezeka kutoka 3,634 mwaka 2010 hadi kufikia 4,618 mwaka 2014. Katika kutoa huduma za maji safi na salama, baadhi ya maeneo yamefikisha asilimia 87.7 ya mahitaji halisi katika Mkoa wa Mjini Magharibi Kaskazini Unguja asilimia 71.7, Kusini Unguja 76.4 Kaskazini Pemba, asilimia 56.4 na Kusini Pemba asilimia 74.1.

Mafanikio yapo pia na yanajionesha katika Sekta zingine zote kama vile Barabara, usafirishaji na uimarishaji wa Miundombinu ya Bandari, Viwanja vya Ndege, Kilimo, Ardhi, Upatikanaji wa Umeme, Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Spika, nimeamua kuyasema mafanikio haya kuonesha hatua iliyofikiwa kutokana na juhudi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kujenga uchumi imara wa watu wake. Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein na wananchi wote wa Zanzibar kwa jinsi wanavyoshirikiana katika kuhakikisha wanapiga hatua ya maendeleo ya kukuza uchumi wa Zanzibar. Pamoja na pongezi hizi ni matumaini yangu kwamba wananchi wa Zanzibar wataendeleza ushirikiano uliopo chini ya uongozi wa Dkt, Ali Mohamed Shein katika kukuza uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hitimisho; kama ilivyo ada, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kutuongoza vizuri na kwa busara kubwa. Niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri ya kuongoza vikao vya Bunge lako Tukufu. Kipekee niwatambue Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o na Mheshimiwa Kidawa Salehe ambao wamekalia kiti kwa mara ya kwanza lakini kwa weledi mkubwa, nasema hongereni sana. *(Makofi)*

Niwashukuru tena Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta na zisizo za Kisekta kwa kuwasilisha taarifa za Kamati zao vizuri. Aidha, nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Teule kwa kazi nzuri aliyoifanya katika uwasilishaji wa taarifa yake pamoja na wajumbe wake wote.

Aidha, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri ya kujadili taarifa hizo na kwa michango mbalimbali wakati wa Mkutano huu. Mapendekezo ya Kamati zote tuliyokubaliana tumeyaweka pamoja ili kupata urahisi wa kuyatekeleza. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge wote wawe na nakala ya mapendekezo hayo kwa ajili ya ufuatiliaji na kuendelea kuibana Serikali kuhakikisha kwamba wanatekeleza kile walichoshauriwa.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kumshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ya kuhakikisha Mkutano huu unakamilisha shughuli zake kama ilivyopangwa. Niwashukuru Wataalam wote wa Serikali na Taasisi zake ikijumuisha Taasisi za Sekta Binafsi, kwa misaada ya Kitaalam na huduma mbalimbali za kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi*

Niwashukuru pia Waandishi wa Habari kwa kazi nzuri walizofanya kuhakikisha kuwa taarifa za majadiliano na maamuzi mbalimbali ya hapa Bungeni zinawafikia wananchi. Niwashukuru Madereva kwa kazi nzuri waliyofanya ya kuwasafirisha kwa usalama Waheshimiwa Wabunge, Viongozi mbalimbali, Wataalam na Wasaidizi wote walioshiriki katika Mkutano huu.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwatakia wote safari njema mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi na katika Majimbo yenu. Naamini kwamba, Mwenyezi Mungu atatulinda na kutuweka salama sote kama tulivyo hadi kukutana tena katika Mkutano ujao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 17 Machi, 2015 saa Tatu Asubuhi litakapokutana katika Mkutano wa 19 kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma. *(Makofi*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono. Kwanza kabisa naomba nikushukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba uliyotoa na pia napenda nitambue uwepo wa Mama Tunu Pinda ambaye amekuja kutuona tunapomaliza kikao chetu. *(Makofi)*

Pia napenda niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Bunge litaanza tarehe 17, mwezi wa Tatu, lakini nyinyi Waheshimiwa Wabunge mnatakiwa kuwepo Dar-es-Salaam, kuanza shughuli za Kamati tarehe 2 mwezi Machi, mpaka tarehe 13.

Sasa kazi ya Kamati safari hii itakuwa kwenda kutembelea miradi ambayo tuliipitishia fedha hapa kipindi kilichopita mwaka huu, kuona wamefikia hatua kiasi gani na kama utekelezaji ulikuaje, kwa sababu haya ni maandalizi ya kikao cha bajeti.

Tumewahi kufanya hivi kwa sababu, mwezi wa Nne ambapo mngefanya kazi hii, inawezekana kukawa na shughuli mbalimbali zingine kama za kura ya maoni. Kwa hiyo, tutafanya hivi halafu mtakuja tufanye Bunge la kawaida, tutakaporudi tunaingia moja kwa moja kuangalia *estimates* za Wizara mbalimbali. Kwa hiyo, kukagua miradi hii tunaanza tarehe 2 mpaka tarehe 13. Kwa hiyo, Makatibu wa Kamati zote wawaandalie Wabunge, ni wapi wanapokwenda na miradi gani ambayo wangependa kuiona na kuona hali halisi itakavyokuwa. *(Makofi*

Waheshimiwa Wabunge, pia nishukuru kwa kazi ambayo mmefanya, inaonekana siku zinakwisha lakini mnazidi kuimarika. Mnazidi kuimarika katika kufanya kazi zenu ndiyo kukua, kama ingekuwa hatukui, maana yake tungekuwa tumedumaa. Kwa hiyo, mmekua! Hata kama muda uliobakia ni mfupi kabisa, maana yake Bunge litakalokuja hili litakuwa la 19, linabakia moja tu.

Kwa hiyo, naamini kabisa mtakwenda kutumia vizuri wakati wenu, kwa mapenzi kabisa kwa juhudi sana, bila kuumizana wala kufanya vitu vibaya, kwa sababu Mungu ni lazima mumtangulize katika mambo yenu yote. Kwa hiyo, msifanye tu peke yenu, Mungu akipenda itakuwa hivyo, lakini mkafanye kazi kwa siku hizo chache, naziona chache sana. Kwa hiyo, mkafanye kazi mnayostahili.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema kwanza niwapongeze Mheshimiwa Lediana Mg'ong'o na Mheshimiwa Kidawa, kwa umahiri wao siku mbili walizokaa hapa mliona kazi zao ni nzuri, nawashukuru sana na sisi wenyewe wametusaidia kuweza kupumzika. Kidogo afya ya Naibu Spika haikuwa vizuri sana safari hii. Kwa hiyo, niwashukuru sana na niwatakie safari njema, huko mnakokwenda. *(Makofi*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, nitawahoji kuhusu hoja ya Waziri Mkuu, ya kuahirisha Bunge mpaka tarehe 17, Machi, 2015. *(Makofi*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Naomba tusimame kwa ajili ya Wimbo wa Taifa.

*(Wimbo wa Taifa uliimbwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wajumbe, tukae.

Waheshimwa Wabunge, sasa naahirisha kikao cha hiki cha Bunge mpaka tutakapokutana tena tarehe 17 Machi, 2013. Sasa nitawahoji.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Saa 7. 51 mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 17 Machi, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*